# Kiswahili
# kwa
# Shule za Rwanda
# Michepuo Mingine
# Kidato cha 6

Mwongozo wa
Mwalimu

# DIBAJI

**Mwalimu Mpendwa**

Bodi ya Elimu Rwanda inayo heshima kwa kutoa kitabu hiki cha somo la Kiswahili michepuo mingine kidato cha sita kitabu cha mwalimu .Kitabu hiki kitakuwa waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo .

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga katika kumpatia mlengwa uwezo katika kila ngazi ya Elimu kuweza kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira .

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha ubora wa Elimu Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa wa ujifunzaji . Mambo mengi yanayoathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa , namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao . Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahsusi wa yaliyomo,ubora wa walimu , mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo . Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unakuwezesha kuendeleza mawazo yako na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yawe ya binafsi au katika makundi ,kwa msaada wa walimu ambao majukumu yao ni kufanikisha ufundishaji.Utapata stadi zinazofaa kukuwezesha kutumia yale uliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi.Kwa kufanya hivyo , utaonyesha tofauti siyo tu katika maisha yako bali hata kwa Taifa .

HIi inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji,iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mwalimu.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo , ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu , stadi na maadili na mweneno mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi , hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa , kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema .

Aidha kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonysha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji .

Katika mtazamo huu jukumu lako litakuwa :

- Kuandaa majadiliano katika makundi ya ushirikano kwa wanafunzi ukizingatia umuhimu wa ushauri kuwa kujifunza hufanyika kwa ufanisi wakati mwanafunzi afanyapo kazi kwa kushirikiana na watu wanaomzidi maarifa na uzoefu.

- Wanafunzi washirikishe kwa kupitia kazi za ujifunzaji kama: njia ya uchunguzi, makundi ya mijadala, utafiti,mazoezi ya utafiti na kazi za binafsi.
- Toa fursa ya usimamizi kwa wanafunzi kwa kuendeleza uwezo wao kwa kuwapa ushindani tofauti na kutoa majukumu yanayoongeza tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatazo,ubunifu, na uvumbuzi,mawasiliano na ushirikiano.
- Toa msaada na kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kwa kutathmini mchango wa wanafunzi katika mazoezi ya darasani .
- Waongoze wanafunzi kuoanisha matokeo ya utafiti
- Hamasisha kila mmoja, rika na tathmini kazi iliyofanyika darasani kwa kutumia uwezo na mbinu sahihi za msingi.
- Kuwezesha katika mazoezi yako ya kufundisha, yaliyomo katika mwongozo huu wa mwalimu unaeleweka kiasi kwamba unaweza kutumiwa kwa urahisi.

Mwongozo huu umeganyika katika sehemu tatu (3)

Sehemu ya 1: Huelezea muundo wa kitabu hiki na kukupa mbinu na maelekezo ya ufundishaji.

Sehemu ya 2: Hukupa sampuli ya andalio la somo kama marejeleo ya mhakato wa kuandaa somo .

Sehemu ya 3: Hutoa mwongozo au maelekezo ya ufundishaji kwa kila dhana iliyotolewa ndani ya kitabu .

Napenda kutoa shukrani kwa wale wote walioshiriki kutoa mchango wa kuboresha kitabu hiki, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda (CTLR –REB) walioandaa mchakato wa kazi hii tokea ilipoanza .

Pongezi muhimu ziwaendee walimu chuo Kikuu cha Rwanda kwa msaada wao wa kutoa wataalamu ambao ni ,wahadhiri walimu wachoraji waliosaidia kusimamia , kuendeleza na kufanikisha uboreshaji wa kazi hii kuhusu picha na michoro sahihi . Maoni au mawazo yoyote yanakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo yatakayofuata .

**Dr Ndayambaje Irénée**

**Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Elimu Rwanda**

# SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki.Kitabu hiki kisingeliwezekana kufanikiwa bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki , jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati .

Shukrani zangu za kwanza ziwaendee wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda walioshiriki katika kuandaa na kuandika kitabu hiki .Napenda kutoa shukrani zaidi kwa walimu kutoka chekechea hadi chuo kikuu kwa ngazi zote kwa juhudi zao wakati wa utendaji wao ulio wa thamani .

Natoa shukrani kwa shule mbalimbali Rwanda zilizoweza kuwaruhusu walimu na wahadhiri katika kuandaa kitabu hiki hadi kuhaririwa kwake .

Napenda kutoa shukrani kwa wale wote walioshiriki kutoa mchango wa kuboresha kitabu hiki, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda (CTLR –REB) walioandaa mchakato wa kazi hii tokea ilipoanza .

**Joan Murungi**

**Mkuu wa idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana** (CTLR –REB)

**Hati milki**

*© **2019 Bodi ya Elimu Rwanda***
*Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Elimu Rwanda. Haki zote zimehifadhiwa.*
*Kimetayarishwa na Bodi ya Elimu Rwanda kwa idhini ya Wizara ya Elimu.*

*Chapa ya Kwanza 2019*

**Contents**


**DIBAJI** . . . . . ii

**SHUKRANI** . . . . . iv

**SEHEMU YA I: UTANGULIZI WA JUMLA** . . . . . 11

1.1 Muundo wa Kitabu cha Mwalimu . . . . . 11

1.2 Mwelekeo wa Ufundishaji . . . . . 11

**SEHEMU II: SAMPULI YA ANDALIO LA MASOMO YA KISWAHILI** . . . . . 15

**MADA NDOGO YA 1: MSAMIATI KATIKA MAZINGIRA YA BENKI** . . . . . 31

Uwezo Upatikanao katika Mada: . . . . . 31

Ujuzi wa Awali . . . . . 31

Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada . . . . . 31

Mwongozo kuhusu Kazi Inayotangulia Mada . . . . . 31

Orodha ya Masomo na Tathmini . . . . . 32

**SOMO LA 1: BENKI NA SHUGHULI ZAKE** . . . . . 33

1.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi . . . . . 33

1.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji . . . . . 34

1.3. Kazi za ujifunzaji . . . . . 34

1.4. Majibu . . . . . 34

1.4.1 Zoezi la Ufahamu . . . . . 35

1.4.2 Msamiati kuhusu Kifungu "Penye Nia". . . . . . 35

1.4.4. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi: . . . . . 36

1.4.5. Matumizi ya Lugha: . . . . . 38

1.4. 7. Utungaji: . . . . . 39

**SOMO LA PILI: MANUFAA YA BENKI.** . . . . . 40

2.1. Ujuzi wa Awali . . . . . 40

2.2. Zana au Vifaa vya Kujifunzia . . . . . 40

2.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunza . . . . . 40

2.4. Majibu . . . . . 41

2.4.1. Maswali ya Ufahamu. . . . . . 41

2.4.2. Msamiati kuhusu Benki. . . . . . 41

2.4.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi . . . . . 43

2.4.4. Matumizi ya Lugha . . . . . 45

2.4. 5. Kusikiliza na Kuzungumza . . . . . 45

2.4. 6. Utungaji: . . . . . 45

**SOMO LA 3 : AINA ZA BENKI** . . . . . 46

3.1. Ujuzi wa Awali/ Marudio/Utangulizi . . . . . 46

3.2 Zana za Kujifunzia . . . . . 46

3.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza . . . . . 46

3.4. Majibu . . . . . 47

3.4.1. Maswali ya Ufahamu . . . . . 47

3.4.2. Msamiati kuhusu Aina za Benki . . . . . 48

3.4.3. Sarufi kuhusu Mnyambuliko wa Vitenzi. . . . . . 48

3.4.4. Matumizi ya Lugha . . . 48
3.4.5. Kusilikiza na Kuzungumza . . . 49
3.4.6 Utungaji: . . . 49
**SOMO LA 4: WATUMISHI WA BENKI NA MAJUKUMU YAO . . . 50**
4.1 Ujuzi wa Awali/ Marudio/Utangulizi . . . 50
4.2 Zana za Kujifunzia . . . 50
4.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza . . . 50
4.4. Majibu . . . 51
4.4.1. Maswali ya Ufahamu . . . 51
4.4. 2. Msamiati kuhusu Watumishi wa Benki na Majukumu yao . . . 52
4.4.3. Sarufi kuhusu Mnyambuliko wa Vitenzi. . . . 53
4.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza . . . 54
4.4. 6. Utungaji . . . 54
**SOMO LA 5: KARATASI MAALUMU ZINAZOTUMIWA KATIKA BENKI . . . 54**
5.1 Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi . . . 54
5.2 Zana za Kujifunzia: . . . 55
5.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza . . . 55
5.4. Majibu . . . 56
5.4.1 Maswali ya Ufahamu . . . 56
5.4.2: Msamiati kuhusu Karatasi Maalum Zinazotumika katika Benki. . . . 56
5.3: Sarufi kuhusu Mnyambuliko wa Vitenzi . . . 57
5.4. 4 Matumizi ya Lugha . . . 58
5.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza . . . 60
5.4.6. Utungaji . . . 60
5.5. Muhtasari wa Mada . . . 60
5.6. Maelezo ya Ziada . . . 60
5.7. Tathmini ya Mada ya Kwanza . . . 61
5.8. Mazoezi ya Nyongeza . . . 62
5.8.1 Mazoezi ya Urekebishaji . . . 62
5.8.2. Mazoezi ya Jumuishi . . . 62
5.8.3. Mazoezi ya Wanafunzi wenye Ujuzi wa Hali ya Juu . . . 62
**SOMO LA 6: HADITHI FUPI . . . 63**
6.1 Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi . . . 63
6.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia . . . 63
6.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia . . . 63
6.4 Majibu . . . 64
**MADA NDOGO: TANZU ZA FASIHI ANDISHI KATIKA KISWAHILI . . . 71**
Uwezo Upatikanao katika Mada: . . . 71
Ujuzi wa Awali Katika shule za awamu . . . 71
Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada . . . 71
Maelekezo kuhusu Kazi . . . 71
Orodha ya Masomo na Tathmini . . . 72

**SOMO LA 7: USHAIRI WA KISWAHILI. . . . . 73**
7.1. Ujuzi wa Awali/ Marudio/Utangulizi . . . . . 73
7.2 Zana za Kujifunzia . . . . . 73
7.3 Mbinu za Kufundishia na kujifunzia. . . . . 73
7.4. Majibu . . . . . 74
7.4.1. Maswali ya Ufahamu . . . . . 74
7.4.2 Msamiati: Kuhusu Ushairi. . . . . 74
7.4.3 Sarufi kuhusu Matumizi ya virai. . . . . 75
7.4.4 Matumizi ya Lugha. . . . . 76
**SOMO LA 8: UFAFANUZI WA RIWAYA . . . . . 78**
8.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi . . . . . 78
8.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji . . . . . 78
8.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia . . . . . 78
8.4. Majibu . . . . . 79
8.4.1. Kidokezo . . . . . 79
8.4.3. Msamiati . . . . . 79
8.4.4. Sarufi: Vishazi Huru . . . . . 80
8.4.5. Matumizi ya Lugha . . . . . 81
8.4.6. Kusikiliza na Kuzungumza . . . . . 82
8.4. 6. Utungaji . . . . . 83
**SOMO LA 9: UFAFANUZI WA TAMTHILIA . . . . . 84**
9.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi . . . . . 84
9.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji . . . . . 84
9.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunza . . . . . 84
9.4. Majibu . . . . . 85
9.4.1 Zoezi la Ufahamu. . . . . 85
9.4.2 Msamiati . . . . . 86
9.4.3. Sarufi: Matumizi ya Vishazi . . . . . 88
9.1.4. Matumizi ya Lugha: Fani na Maudhui katika Tamthilia . . . . . 89
9.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza . . . . . 90
9.4.6. Kuandika . . . . . 90
9.5. Muhtasari wa Mada . . . . . 91
9.6. Maelezo ya Ziada . . . . . 91
9.7. Tathmini ya Mada ya Pili` . . . . . 97
9.8. Mazoezi ya Nyongeza . . . . . 97
98.1. Mazoezi ya Urekebishaji . . . . . 97
9.8.2. Mazoezi Jumuishi . . . . . 98
.9.8.3. Mazoezi ya Wanafunzi wenye Ujuzi wa Hali ya Juu. . . . . 98
**MADA NDOGO: HOTUBA NA UFUPISHO. . . . . 99**
Uwezo Upatikanao katika Mada: . . . . . 99
Ujuzi wa Awali. . . . . 99
Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada. . . . . 99

Maelekezo kuhusu Kazi ........ 99
Orodha ya Masomo na Tathmini ........ 100
**SOMO LA 10: HOTUBA ........ 101**
10.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi ........ 101
10.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji ........ 101
10.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia ........ 101
10.4. Majibu ........ 102
10.4.1 Zoezi la Ufahamu ........ 102
10.4.2 Msamiati kuhusu Kifungu cha Habari ........ 102
10.4.4. Sarufi : Uambishaji wa Vitenzi:........ 103
10.4.6. Kusikiliza na Kuzungumza ........ 106
**SOMO LA 11: MUUNDO WA HOTUBA ........ 106**
11.1 Utangulizi/Marudio ........ 106
11.2 Vifaa vya Kujifunzia ........ 106
11.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia ........ 107
11.4 Majibu ya Maswali........ 107
11.4.1 Maswali ya Ufahamu ........ 108
11.4.2. Msamiati........ 109
11.4.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi Awali Utendewa na Mzizi........ 109
11.4.4 Matumizi ya Lugha........ 110
11.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza ........ 110
11.4.6. Kuandika........ 111
**SOMO LA 12: UFUPISHO WA HOTUBA ........ 112**
12.1. Ujuzi wa Awali/ UtanguliziA........ 112
12.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 112
12.3. Mbinu za Kujifundishia na Kujifunzia ........ 112
12. 4 Majibu ........ 113
12.4.1 Ufahamu ........ 113
12.4.2 Msamiati ........ 114
12.4.3. Sarufi........ 115
12.4.4 Matumizi ya Lugha ........ 117
12.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza ........ 119
12.4.6 Kuandika: Kufupisha Kifungu cha Habari ........ 119
12.5. Mazoezi ya Nyongeza ........ 124
12.5.1. Mazoezi ya Urekebishaji........ 124
12.5.2 Mazoezi Jumuishi........ 124
12.5..3. Mazoezi ya Wanafunzi Wenye Ujuzi wa Hali ya Juu........ 124
**MADA NDOGO: MIDAHALO NA MIJADALA........ 125**
Ujuzi wa Awali........ 125
Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada........ 125
Maelekezo kuhusu Kazi........ 125
Orodha ya Masomo na Tathmini ........ 126

**SOMO LA 13: MDAHALO** .127
13.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi. .127
13.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji .127
13.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunza. .127
13.4. Majibu 128
13.4.1 Majibu kuhusu Ufahamu. 128
13.4.2 Msamiati 129
13.4.3. Sarufi: Uambishaji wa Maneno. 130
13.4. 4 Matumizi ya Lugha .131
13.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza 132
13.4.6 Kuandika: Utungaji 133
**SOMO LA 14: MJADALA** .133
14.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi 133
14.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji. 133
14.3. Mbinu za Kujifundishia na Kujifunzia 134
14.1. Mapendekezo ya Majibu ya Ufahamu 134
14.4.1 Kusoma na Ufahamu. 134
14.4.2 Msamiati kuhusu Mjadala 135
14.4.3 Sarufi: Uambishaji wa maneno kuhusu vivumishi na Vitenzi 136
14.4.4 Matumizi ya Lugha 137
14. 4.6. Utungaji:. 138
**SOMO LA 15: UHUSIANO NA TOFAUTI KATI YA MIDAHALO NA MIJADALA** 139
15.1 Utangulizi/Marudio 139
15.2 Vifaa vya Kujifunzia. 139
15.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia. 139
15.4 Majibu 140
15.4.1 Maswali ya Ufahamu. 140
15.4.2. Msamiati Kuhusu Kifungu cha Habari. 142
15.4.3. Sarufi. 143
15.4.4 Matumizi ya Lugha 143
15.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza 144
15.4.6. Kuandika 145
**MAREJEO** 149

# SEHEMU YA I: UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Muundo wa Kitabu cha Mwalimu

Kitabu hiki ni mwongozo wa mwalimu wenye maelezo kuhusu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji. Kimetayarishwa kuwaelekeza walimu wanaofundisha kidato cha sita michepuo mingine katika shule za sekondari nchini Rwanda. Kitabu hiki ni zana muhimu sana itakayomsaidia mwalimu kumudu ujifunzaji na ufundishaji unaozingatiwa katika mtaala uegemeao katika uwezo. Hivyo kitamfaa sana mwalimu ili aweze kuyafikia malengo ya kila somo kwa urahisi. Hivyo basi, itambidi mwalimu achunguze vizuri mazoezi na kazi mbalimbali zilizopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi. Mwongozo wa mwalimu huu umetokana na mada kuu nne zifuatazo:

1. Matumizi ya Lugha katika Mazingira Mbalimbali
2. Fasihi katika Kiswahili
3. Ubunaji
4. Ukuzaji wa Matumizi ya Lugha

## 1.2 Mwelekeo wa Ufundishaji

Katika mchakato wa ujifunzaji wa Kiswahili, uwezo wa jumla wa mwanafunzi unapewa kipaumbele sana. Uwezo huo wa jumla ni pamoja na tafakuri tunduizi, ubunifu, utafiti, utatuzi wa matatizo na ushirikino. Haya yote yanafanikishwa katika ufundishaji kwa lengo la kuhakikisha kuwa mahitaji ya mwanafunzi katika somo la Kiswahili yametoshelezwa. Hivyo basi, wanafunzi watapewa kazi mbalimbali zinazohitaji ushirikiano kati yao ili kufanya tafiti zao na kuwazoweza kushirikiana katika kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza maishani mwao.

### 1.2.1. Mwelekeo wa Kuendeleza Uwezo

Ili kuendeleza uwezo wa mwanafunzi, mwalimu anahitaji kuzingatia kuwa mtaala unaoegemea katika uwezo hutilia mkazo mambo yafuatayo:

- Kuendeleza maarifa, stadi, mwenendo mwema kulingana na wakati husika kwa kuhusisha mambo mbalimbali yanayojitokeza katika mazingira yake.
- Kuendeleza ujuzi na tekinolojia kulingana na maendeleo ya ujifunzaji wa kila mwanafunzi.

Kila somo lililoandaliwa linazingatia nafasi ya kumjengea mwanafunzi stadi sahihi za mawasiliano katika miktadha mbalimbali ya kimaisha kama mtu aliye na uwezo wa kuingiliana na watu mbalimbali katika miradi ya kijamii na kimaendeleo. Vile vile kitabu hiki kimezipendekeza mbinu za ujifunzaji na ufundishaji zinazojumuisha kwa pamoja maarifa, stadi, maadili na mienendo miema miongoni mwa wanafunzi. Uwezo unaotakiwa kumsaidia mwalimu kujenga uwezo imara wa mwanafunzi utajikita katika mazoezi ya kusoma, kuandika, kusikiliza na kuzungumza kama njia muhimu za kudumisha mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Ili kumwezesha mwanafunzi kupanua uwezo wake, mwalimu akumbuke kumshirikisha mwanafunzi kutumia teknolojia kama njia ya kisasa ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

### 1.2.2. Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka

Mwalimu aingize masuala mtambuka yote manane yanayojitokeza katika mtaala wa taifa. Hayo ni mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi, mazingira na maendeleo endelevu, usawa wa kijinsia, mafunzo kuhusu afya ya uzazi, mafunzo kuhusu amani na maendeleo, mafunzo kuhusu uzalishajimali, mila na desturi, na kuzalisha bidhaa kwa kuzingatia viwango, na mwisho ni elimu jumuishi. Baadhi ya masuala mtambuka yalihusishwa na masomo kwa kiwango cha kuonekana kuwa na uhusiano wa karibu, lakini mwalimu anaweza kuhusisha masomo na masuala mtambuka anapoamua kwamba ni lazima kulingana na ubunifu wake.

### 1.2.3. Uangalizi wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Katika kufundisha wanafunzi, mwalimu anatarajiwa kuhakikisha kwamba somo lake linaendelea bila ubaguzi wowote. Kwa hiyo, inambidi mwalimu kuyakumbuka na kuyahudumia makundi mbalimbali ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu au ya kipekee katika ujifunzaji wao. Hao ni kama vile wanafunzi wenye tatizo la kutoona, kutosikia, kutoandika, kutosoma, kutozungumza na matatizo mengine ya kiakili. Kwa kuwashirikisha wote, mwalimu hulazimishwa kutayarisha mazoezi ya kipekee kulingana na mahitaji ya kila mwanafunzi.

Mwalimu awapatie muda au fursa mwafaka wanafunzi hao kulingana na mahitaji yao ili waweze kukuza stadi zao za tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatizo, utafiti, ubunifu, ugunduzi, mawasiliano na ushirikiano. Awaelekeze kubaini kwa urahisi mambo muhimu yanayoweza kuthibitisha uwezo wao kulingana na masomo yaliyofundishwa.

### 1.2.4. Mwongozo wa Tathmini

Tathmini ni jambo muhimu sana katika ufundishaji na ujifunzaji. Malengo ya tathmini ni kupima maendeleo ya somo ambapo mwalimu huweza kuchagua aina ya tathmni kulingana na malengo yake na kupima uwezo wa wanafunzi baada ya somo.

#### Tathmini Endelezi

Tathmini endelezi hulenga kupima jinsi ufundishaji na ujifunzaji unavyoendelea au malengo ya ufundishaji na ujifunzaji yanavyofikiwa kwa kiwango fulani ili kuamua kuhusu maboresho ya somo ya baadaye. Tathmini hizi hufanywa wakati masomo yangali yanaendelea. Mwalimu huwahamasisha wanafunzi kufanya mazoezi na majaribio binafsi au mazoezi ya makundi kwa kutumia mbinu zinazoegemea kwenye uwezo, maadili na mwenendo mwema kulingana na kila somo.

#### Tathmini ya Jumla

Kila tathmini huwa na dhima yake katika ufundishaji na ujifunzaji. Tathmini hii hufanywa mwishoni mwa mada nzima kabla ya kutangulia mada nyingine. Aidha, tathmini inayofanyika mwishoni mwa muhula na mwishoni mwa mwaka itakuwa mojawapo ya tathmini ya jumla na wakati huu hulenga kurekodi ujuzi, uwezo, maadili na mwenendo mwema miongoni mwa wanafunzi kiasi kwamba walimu, viongozi wa shule na wazazi hupata na kuchunguza matokeo ya tathmini iliyofanywa.

Tathmni zilizopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi ni muhimu sana katika maendeleo ya somo la Kiswahili. Mwalimu kwa ubunifu wake atafute mbinu za kuwafanyisha wanafunzi wake tathmini hizo.

### 1.2.5 Mbinu na Mikakati ya Kuendeleza Ufundishaji na Ujifunzaji

Katika mtindo wa mwanafunzi kama mlengwa – mshiriki, mwalimu huwa na wajibu wa kutumia mbinu tofauti na mchanganyiko katika ufundishaji wake. Kwa kuendeleza ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu anahitaji kutumia mbinu zifuatazo:

- Kazi katika makundi: Wanafunzi zaidi ya wawili hujenga kundi na katika kundi hilo wanashirikiana kufanya kazi waliopewa kama mtu mmoja. Ni vizuri kujenga makundi yasiyozidi wanafunzi sita kwa kila moja.
- Ushirikiano kwa jozi: Mwanafunzi hushirikiana na mwenzake kujadiliana na kukubaliana juu ya jambo fulani ama kufanya kazi pamoja.
- Kazi binafsi: Mwanafunzi afanye kazi ya kibinafsi wakati wa kufanya zoezi lililopendekezwa kufanywa namna hiyo. Mwalimu asahihishe zoezi hili pamoja na kumwonyesha makosa ya kurekebisha.
- Tafakari binafsi: Mwanafunzi hupewa fursa ya kufikiri yeye binafsi na kutoa maoni yake juu ya jambo linalokusudiwa kuzungumziwa.
- Waza – Jozi – Wasilisha: Mwanafunzi hutafakari kibinafsi, kisha hushirikiana na mwenzie na baadaye hutoa kwa pamoja maoni yao hadharani.
- Mijadala au mdahalo: Katika zoezi la kuzungumza, wanafunzi hupewa mada au kauli fulani na kuijadilia kwa njia ya mdahalo au mjadala.
- Maigizo: Mwalimu huwasilisha somo kwa wanafunzi ambao hulicheza kama tamthilia darasani. Somo lenyewe huwa maigizo yanayochezwa na wanafunzi mbele ya wanafunzi wenzao.
- Utafiti: Mwanafunzi hupewa kazi fulani na mwalimu ili aende kujitaftia habari zaidi maktabani, kwenye mtandao wa intaneti au mahali pengine.
- Uchunguzi wa kimatembezi: Wanafunzi hufanya matembezi kwa ajili ya uchunguzi wa jambo fulani la kujifunzia somo au masomo maalumu pamoja na mwalimu wao.

### 1.2.6. Mbinu za Ufundishaji Zinazokuza Shughuli ya Ujifunzaji Shirikishi

Ili kufanikisha malengo ya somo lake, mwalimu anahitaji kuzingatia njia zifuatazo:

- Njia shirikishi ya makundi: Njia shirikishi ambayo hutumia makundi ya wanafunzi huwawezesha wanafunzi hao kushiriki katika kitendo cha ufundishaji na ujifunzaji. Jambo la kufanywa hapa ni kuwapatia wanafunzi wote fursa za kushiriki katika shughuli zinazopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi. Hali hii hutokana na mazingira yanayojengwa na mwalimu ambapo mwanafunzi huchukuliwa kama kiini cha ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo basi, wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya shughuli zote watakazoombwa na mwalimu.

- Njia shirikishi ya ubinafsi: Njia hii inahusu kazi binafsi za kila mwanafunzi ambapo atapewa kazi au mazoezi yake binafsi ili aweze kufikia kiwango cha umilisi wa lugha kinachotarajiwa.
- Maswali na majibu: Mara nyingi somo huchukua mwelekeo wa majadiliano kati ya wanafunzi au mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Kwa upande mwingine, wanafunzi watamwuliza mwalimu maswali naye atawajibu. Hapo ni vizuri kwamba mwalimu awape wanafunzi kwanza fursa ya kujibu maswali ya wenzao kabla yeye kujibu.
- Maelezo ya mwalimu: Mwanafunzi hupewa muda wa kushiriki yeye binafsi katika somo. Katika njia hii, mwalimu atakuwa mwelekezi na shughuli yake muhimu iatategemea kuwaongoza wanafunzi kupata ufahamu na uelewa unaofaa suluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

# SEHEMU II: SAMPULI YA ANDALIO LA MASOMO YA KISWAHILI

## ANDALIO LA SOMO

**ANDALIO LA SOMO**

**Jina la Shule:………………….                Jina la Mwalimu:…………………..**

| **Muhula** | **Tarehe** | **Somo** | **Kidato** | **Mada** | **Idadi ya masomo** | **Muda** | **Idadi ya wanafunzi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | 23/6/2018 | Kiswahili | 6 | 2 | 5/9 | Dakika 80 | 43 |

| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu pamoja na idadi yao:**<br>Mwanafunzi mwenye matatizo ya kuandika: 1 | |
|---|---|
| **Mada kuu** | FASIHI KATIKA KISWAHILI |
| **Mada ndogo** | UFAFANUZI WA TANZU ZA FASIHI ANDISHI KATIKA KISWAHILI |
| **Uwezo upatikanao katika mada** | Kuelewa tanzu za fasihi andishi ya Kiswahili kwa madhumuni ya kuimarisha sanaa na kuitumia kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani. |
| **Kichwa cha somo** | Sarufi : Virai nomino |
| **Malengo ya kujifunza** | Kupitia mifano katika kifungu cha habari, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kuchambua na kutumi virai nomino katika sentensi. |
| **Mahali ambapo somo litatolewa** | Darasani |
| **Zana au vifaa** | - Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,<br>- Kitabu cha mwanafunzi,<br>- Flip chart na kalamu zake husika. |

<table>
<tr><td>Marejeo</td><td colspan="3">-<br>arufi miundo ya Kiswahili Sanifu<br>-<br>amusi ya Kiswahili sanifu, toleo la tatu</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Muda na hatua</td><td colspan="2">Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji</td><td rowspan="2">Uwezo wa jumla na<br>Masuala mtambuka na maelezo mafupi</td></tr>
<tr><td colspan="2">Kwa kupitia kazi za kusoma kifungu , kutazama mifano, kufanya mazoezi katika makundi, wanafunzi wataelewa matumizi ya virai nomino katika sentensi.</td></tr>
<tr><td>Wajibu wa mwalimu</td><td>Wajibu wa mwanafunzi</td><td></td></tr>
<tr><td>1. Utangulizi<br>Dakika 7</td><td>- Mwalimu awaamkie wanafunzi.<br>- Mwalimu awaulize maswali kuhusu somo lililopita.<br>-Mwalimu atawaweka wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu.<br>-Mwanafunzi mwenye matatizo ya kuandika awekwe katika kundi pamoja na wanafunzi wengine.</td><td>-Wanafunzi wajibu salamu za mwalimu.<br>-Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kuhusu somo lililotangulia.<br>-Wanafunzi watajigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu</td><td rowspan="2">Uwezo wa jumla<br>Mawasiliano katika lugha rasmi.<br>Kupitia njia ya kujadiliana na kujibu maswali ya mwalimu katika makundi. wanafunzi wanatumia lugha rasmi ya Kiswahili.<br>Tafakuri tunduizi: wanafunzi kwa kutafuta maana ya matumizi ya virai</td></tr>
<tr><td colspan="3">2. Somo lenyewe</td></tr>
</table>

| | | | |
|---|---|---|---|
| Dakika 60 | | | nomino wanatafakari kwa kuchunguza maana.<br><br>**Ujifunzaji wa muda mrefu:** kwa kuelewa matumizi ya virai nomino walitumia ujuzi waliokuwa nao kuhusu sentensi<br><br>.<br><br>**Masuala mtambuka**<br><br>• **limu isiyo na ubaguzi:** katika makundi ya wanafunzi mwanafunzi mwenye matatizo ya kuandika alisaidiwa na mfano wa sentensi unaoonyesha kuwa elimu isiyo na ubaguzi |
| **2.1 Zoezi la ugunduzi** | -Mwalimu aandike sentensi ambamo kuna Virai nomino<br><br>-Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma sentensi na kujadili pamoja na kugundua virai nomino .<br><br>-Mwalimu amsogelee mwanafunzi mwenye matatizo ya kuandika na kumsaidia na kumwomba kuwakilisha kundi lake.<br><br>Mwalimu aombe wanafunzi kuwasilisha matokeo ya zoezi kwa kila kundi. | -Wanafunzi wasome sentensi ubaoni.<br><br>-Wanafunzi katika makundi yao waatndike sentensi zote kutoka kifungu zinazofanana na sentensi ya ubaoni. | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **2.2 Uwasilishaji wa wanafunzi** | | Kwa kuwasilisha, wanafunzi kutoka makundi waandike ubaoni sentensi zote walizosoma na kueleza aina ya maneno yaliyopigiwa mistari. | inashugulikiwa |
| **2.3 Uchambuzi** | Mwalimu awaombe kuchunguza maana ya maneno yaliyopigiwa mistari.<br><br>Mwalimu anatoa mifano mingine:<br><br>- **Mucyo na Mugabo** huuza | Katika makundi, wanafunzi watajaribu kueleza maana ya maneno yaliyopigiwa mistari. Kila kundi litatoa maelezo yake.<br><br>Wanafunzi katika makundi wanasaidiana kueleza maneno yaliyopigiwa | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | vitabu<br><br>**-Mfanyabiashari hodari** amempatia mama bidhaa.<br><br>**- Kijana yule mnene aliyeniletea karatasi** atakutembelea kesho<br><br>Mwalimu anawapa wanafunzi mazoezi tofauti kuhusu matumizi kirai nomino-<br><br>Mwalimu awaombe wanafunzi kuwasilisha kazi zao. Na kuwasaidia kutoa majibu sahihi. | mistari ni ya aina gani<br><br>**- Mucyo na Mugabo** ni kirai nomino ambacho kinaundwa na nomino mbili<br><br>**Mfanyabiashara hodari** ni kirai nomino kinachoundwa na nomino, kivumishi<br><br>**Kijana yule mnene aliyeniletea karatasi ni** kirai nomino kinachounndwa na Nomino, kivumishi na sentensi .<br><br>Wanafunzi katika makundi yao watafanya mazoezi waliopewa. | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Wanafunzi katika makundi yao, wawasilishe matokeo yao.. | |
| **3. Hitimisho** | -Mwalimu awaombe wanafunzi kutoa mhutasari wa somo .<br><br>-Mwalimu naye anatoa mhutasari. | -Wanafunzi watoe muhtasari wa somo kulingana na maelezo waliopewa. | |
| **4. Tathmini**<br><br>Dakika 13 | -Mwalimu atoe jaribio dogo.<br><br>-Mwalimu awaongoze wanafunzi kusahihisha jaribio.<br><br>-Mwalimu atoe kazi ya nyumbani. | -Wanafunzi binafsi wafanye jaribio kwenye madaftari yao.<br><br>-Wanafunzi wajaribu kusahihisha jaribio<br><br>-Wanafunzi waandike kazi ya nyumbani. | |
| **Tathmini ya mwalimu** | Baada ya somo mwalimu atahakikisha kwamba lengo la ufundishaji na ujifunzaji limefikiwa au la. | | |

ANDALIO LA SOMO

Jina la shule: ....................................Jina la Mwalimu: .....................................

| Muhula | Tarehe | Somo | Kidato | Mada | Idadi ya masomo | Muda | Idadi ya wanafunzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 20/7/2018 | Kiswahili | 6 | 2 | Masomo 5/9 | Dakika 80 | 45 |

| | |
|---|---|
| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao** | Hakuna |
| **Mada kuu** | Fasihi katika Kiswahili |
| **Mada ndogo** | Ufafanuzi wa tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili |
| **Uwezo unaopatikana katika mada** | Kuelewa tanzu tofauti za fasihi andishi ya Kiswahili kwa madhumuni ya kuimarisha sanaa na kuitumia kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani. |
| **Somo lenyewe** | Kusoma na kufahamu hadithi fupi "Penye nia" |
| **Malengo ya kujifunza** | Baada ya kusoma na kufahamu hadithi fupi, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kusema, kueleza na kujivunia uimarishaji wa sanaa kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani. |
| **Mahali somo litakapofundishiwa** | Darasani |
| **Vifaa au zana kwa wanafunzi wote** | Kitabu cha mwanafunzi, ubao, chaki, madaftari na kalamu |
| **Vitabu vya rejea** | Kitabu cha mwanafunzi kidato cha sita, Mwongozo wa mwalimu |

| | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia** | **Uwezo wa jumla na** |
|---|---|---|

| Muda na hatua | Kazi katika makundi: Mara nyingi wanafunzi watafanyia kazi yao katika makundi kwa kushirikiana ili wafanikiwe na mambo kadhaa.<br>**Kazi ya kibinafsi:** Wanafunzi watapata muda mfupi wa kufanya kazi ya kipekee. | | Masuala mtambuka na maelezo mafupi |
|---|---|---|---|
| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |
| **Utangulizi**<br>Dakika 5 | Mwalimu anachangamsha wanafunzi kwa kuwauliza maswali mawili kuhusu somo lililopita, na maswali mengine kuhusu mchoro unaotangulia mfano wa hadithi fupi. Mwalimu akiuliza, anachagua wanafunzi wa kujibu kwa kuchanganya wavulana na wasichana. | Wanafunzi wanajibu maswali yote yanayoulizwa na mwalimu. | **Uwezo wa jumla:** Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na mawasiliano katika lugha rasmi.<br>**Masuala mtambuka:** Usawa wa kijinsia. |
| **Somo lenyewe**<br>Dakika 62 | - Mwalimu anaunda makundi ya wanafunzi wanne wanne ya wavulana kwa wasichana. Baadaye, anawapa vitabu vya mwanafunzi na kuwaomba kusoma kimya hadithi fupi "Pana Nia Pana Njia." Anawaomba kutumia dakika kumi.<br>- Mwalimu anawaomba wanafunzi kusoma tena kifungu cha habari na kujibu | - Wanafunzi wanakaa katika makundi ya wanafunzi wanne wanne na kusoma kifungu wanachopewa kwa kutumia muda waliopewa.<br>- Wanafunzi wanasoma tena kifungu cha habari | **Uwezo wa jumla:** Tafakuri tunduizi.<br>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha.<br>Mawasiliano katika lugha rasmi.<br>Utafiti: Kwa kujibu maswali ndani ya makundi, wanafunzi wanafanya utafiti, wanashirikiana |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | maswali ya ufahamu katika dakika kumi.<br><br>- Mwalimu anawaomba wanafunzi kutafuta maneno mapya katika kifungu cha habari kwa dakika kumi, kisha anawaomba wanafunzi kutafuta kwenye kamusi maana ya kila neno na kutumia kwenye sentensi maneno magumu waliyopewa.Mwalimu anawaelekeza wanafunzi ili wafahamu vizuri maneno ambayo wanashindwa kuyafafanua na kuyatumia katika sentensi.<br>- Mwalimu anawapa wanafunzi mwongozo wa kusoma kifungu cha habari katika dakika kumi.<br><br>- Mwalimu anawapa wanafunzi muda wa kusoma kwa sauti kubwa hivi akiwasahihisha katika dakika kumi .<br><br>- Mwalimu anawaomba wanafunzi kujichagulia wasimamizi wa kuandika majibu ya maswali ya ufahamu | na kujibu maswali ya ufahamu.<br><br>- Wanafunzi wanatafuta maneno magumu na kuyaandika mahali fulani, kisha wanatafuta maana ya maneno hayo kwa kutumia kamusi, kisha wanafanya zoezi la kutumia maneno mapya waliyopewa kwenye sentensi.<br><br>- Wanafunzi wanamwambia mwalimu maneno yanayowashinda na kujaribu kuyafafanua pamoja na mwalimu.<br><br>-Wanafunzi wanasikiliza kwa makini namna mwalimu anavyosoma na kuiga mwenendo na lafudhi nzuri.<br>- Wanafunzi wanasoma mmoja baada ya mwingine kwa kubadilisha makundi. | kupata majibu, na kuchagua viongozi wa makundi hivi wakiwasiliana katika lugha rasmi.<br><br>**Masuala mtambuka:**<br>Usawa wa kijinsia: Wanafunzi wanafanya kazi pamoja; wasichana na wavulana na watapewa fursa sawa.<br><br>Mafunzo kuhusu amani na maadili: Kwa kufanyia kazi katika makundi, wanafunzi wanajadiliana hivi wakitoa na kupokea fikra tofauti kwa amani. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kwenye ubao kundi kwa kundi. Mwalimu atawaongoza wanafunzi ili majibu yanayofanana yasiandikwe mara mbili kwa kutumia muda vizuri. Dakika kumi na mbili zitatumiwa hapa. Mwalimu atasahihisha majibu ya wanafunzi ipasavyo. | - Wanafunzi wanaandika matokeo ya makundi yao yenye kujibu maswali ya ufahamu wa kifungu cha habari kundi baada ya kundi jingine, mvulana na msichana kimpango. Watafuatilia mwalimu iwapo kuna majibu ambayo yanahitaji sahihisho lake. | |
| **Hitimisho**<br>Dakika 13 | - Mwalimu anawapa wanafunzi maelezo muhimu kimuhtasari katika dakika tatu.<br><br>- Mwalimu anawapa wanafunzi maswali matano ya tathmini kuhusu somo ambayo yanatolewa majibu kwa dakika kumi. | - Wanafunzi wanamfuata mwalimu vizuri wakati wa kutoa maelezo.<br><br>- Wanafunzi wanajibu maswali hayo kwenye karatasi na kumpa mwalimu karatasi hizo ili azisahihishe. | **Uwezo wa jumla:** Tafakuri tunduizi na stadi ya utatuzi wa matatizo: wanafunzi watafikiri kwa upana na kujibu maswali wenyewe. |
| **Tathmini ya mwalimu** | | | |

**ANDALIO LA SOMO**

**Jina la shule: ....................................Jina la Mwalimu: ..............................**

<table>
<tr><td>Muhula</td><td>Tarehe</td><td>Somo</td><td>Kidato</td><td>Mada</td><td>Idadi ya masomo</td><td>Muda</td><td>Idadi ya wanafunzi</td></tr>
<tr><td>3</td><td>5 /9 /2018</td><td>Kiswahili</td><td>6</td><td>3</td><td>Masomo 12/15</td><td>Dakika 80</td><td>45</td></tr>
<tr><td colspan="5">Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao</td><td colspan="3">Hakuna</td></tr>
<tr><td colspan="2">Mada kuu</td><td colspan="6">Ubunaji</td></tr>
<tr><td colspan="2">Mada ndogo</td><td colspan="6">Hotuba na ufupisho</td></tr>
<tr><td colspan="2">Uwezo unaopatikana katika mada</td><td colspan="6">Kuelewa mtindo wa hotuba na kuizingatia katika mazoezi ya utungaji pamoja na ufupisho,kujua kuchanganua kitenzi kwa njia ya uambishaji.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Somo lenyewe</td><td colspan="6">Ufupisho</td></tr>
<tr><td colspan="2">Malengo ya kujifunza</td><td colspan="6">Kulingana na hotuba waliyopewa na kuisoma pamoja na kuielewa vizuri, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kuchanganua mawazo makuu na kuifupisha wakizingatia ujumbe wa awali bila ya kupotosha wala kupunguza.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Mahali somo litakapofundishiwa</td><td colspan="6">Darasani</td></tr>
<tr><td colspan="2">Vifaa au zana kwa wanafunzi wote</td><td colspan="6">Kitabu cha mwanafunzi, ubao, chaki, madaftari na kalamu</td></tr>
<tr><td colspan="2">Vitabu vya rejea</td><td colspan="6">Kitabu cha mwanafunzi kidato cha sita, Mwongozo wa mwalimu na vitabu vingine kama vile kamusi,n.k.</td></tr>
<tr><td colspan="2"></td><td colspan="4">Mbinu za kufundishia na kujifunzia</td><td colspan="2">Uwezo wa jumla na</td></tr>
</table>

| Muda na hatua | **Kazi katika makundi:** Mara nyingi wanafunzi watafanyia kazi zao katika makundi kwa kushirikiana ili wafanikiwe na mambo kadhaa yahusuyo somo Wanafunzi watachanganua mawazo makuu yanayojenga hotuba na kufanya ufupisho wa hotuba kufuatilia maelezo waliyopewa. | | Masuala mtambuka na maelezo mafupi |
|---|---|---|---|
| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |
| **Utangulizi**<br>Dakika 5 | Mwalimu anachangamsha wanafunzi kwa kuwauliza maswali mawili kuhusu somo lililopita, na maswali mengine yatakayomwezesha kuwaelekeza wanafunzi kuingia katika somo jipya. Mwalimu akiuliza, anachagua wanafunzi wa kujibu pande zote mbili, kwa upande wa wavulana na wa wasichana. | Wanafunzi wanajibu maswali yote waliyoulizwa na mwalimu. | **Uwezo wa jumla:** Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na mawasiliano katika lugha rasmi.<br>**Masuala mtambuka:** Usawa wa kijinsia. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Somo lenyewe**<br>Dakika 67 | - Mwalimu anawaelekeza wanafunzi wafanye makundi ya wanafunzi watatu watatu,wasichana na wavulana wajichanganye katika kundi moja. Baadaye, anawapa vitabu vya mwanafunzi na kuwaomba kusoma kimya Hotuba ya Daktari Mkuu aliyetembelea shule ya Sekondari."<br>- Mwalimu anawaomba wanafunzi kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali ya ufahamu.<br>- Mwalimu anawaomba wanafunzi kutafuta maneno magumu katika kifungu cha habari, kisha anawaomba wanafunzi kutafuta kwenye kamusi maana ya kila neno | - Wanafunzi wanakaa katika makundi ya wanafunzi wanne wanne na kusoma kifungu wanachopewa kwa kutumia muda waliopewa.<br>- Wanafunzi wanasoma tena kifungu cha habari na kujibu maswali ya ufahamu.<br>- Wanafunzi wanatafuta maaneno magumu na kuyaandika mahali fulani, kisha wanatafuta maana yake kwa kutumia kamusi, wanafanya zoezi kwa kutumia maneno magumu na kuyatumia katika sentensi.<br>- Wanafunzi wanamwambia | **Uwezo wa jumla:** Tafakuri tunduizi.<br>Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha.<br>Mawasiliano katika lugha rasmi.<br>Utafiti: Kwa kujibu maswali ndani ya makundi, wanafunzi wanafanya utafiti, wanashirikiana kupata majibu, na kuchagua viongozi wa makundi wakiwemo makatibu hivi wakiwasiliana katika lugha rasmi.<br>**Masuala mtambuka:**<br>Usawa wa kijinsia: Wasichana na wavulana wanashirikiana kufanya kazi pamoja na kupewa watapewa fursa sawa.<br>Mafunzo kuhusu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | magumu na kutumia maneno hayo katika sentensi ili atambue kuwa wakati wakufanya ufupisho hawatapotootosha ujumbe wa awali.<br><br>- Mwalimu anawaelekeza wanafanzi ili wafahamu vizuri maneno ambayo wanashindwa kuyafafanua na kuyatumia katika sentensi.<br>- Mwalimu anawapa wanafunzi mwongozo wa kusoma kifungu cha habari katika dakika tano.<br><br>- Mwalimu anawapa wanafunzi muda wa kusoma kwa sauti kubwa hivi akiwasahihishi<br><br>- Mwalimu anawaomba | mwalimu maneno yanayowashinda na kujaribu kuyafafanua pamoja na mwalimu.<br><br>-Wanafunzi wanasikiliza kwa makini namna mwalimu anavyosoma na kuiga mwenendo na lafudhi nzuri.<br>- Wanafunzi wanasoma mmoja baada ya mwingine kwa kubadilisha makundi.<br>- Wanafunzi wanajibu kwa kuirudia habari waliyoisoma wakizingatia mawazo makuu.<br><br>Wanafunzi wanaandika muhtasari kufuatilia maelezo na mwelekeo wa mwalimu bila kupoteza wala kupotosha ujumbe wa habari ya awali.<br>Wanafunzi wanasoma ufupisho walioufanya.<br><br>Wanafunzi wanafuata | amani na maadili: Kwa kufanyia kazi katika makundi, wanafunzi wanajadiliana hivi wakitoa na kupokea fikra tofauti kwa amani,kila mmoja anaheshimu hoja la mwenziwe. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wanafunzi kujibu maswali kwa kusema. Kisha mwalimu awaulize wanafunzi ikiwa kuna mwanafunzi ambaye anaweza kuyarudia waliyoyasoma kwa machache akizingatia mawazo makuu na kutumia maneno yake.<br><br>- Mwalimu anawaomba wanafunzi kufanya muhtasari wa habari akiwaelekeza ili wafanye kazi vyema.<br><br>- Mwalimu anawaomba wanafunzi wa makundi mawili kusoma kazi waliofanya na wenzio wakatega masikio.<br><br>- Mwalimu anawaelekeza | mwalimu na kusahihisha makosa wakifufuatilia maelezo muhimu na mwelekeo wa mwalimu.<br>- Wanafunzi wanafanya ufupisho wa Habari waliyopewa kwa nji ifaayo.. | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wanafunzi wasahihishe makosa kwa kufuatilia maelezo muhimu yanayozingatia mbinu za kufanya ufupisho. | | |
| **Hitimisho**<br>Dakika 13 | - Mwalimu anawaelezea tena kuhusu maelezo muhimu yanayohusu ufupisho.<br>- Mwalimu anawatolea wanafunzi kifungu kingine cha hotuba ili wakifupishe.<br>- Mwalimu anakosoa | - Wanafunzi wanamfuata mwalimu vizuri akitoa maelezo kisha wakafanya zoezi walilopewa.<br>- | **Uwezo wa jumla:** Tafakuri tunduizi na stadi ya utatuzi wa matatizo: wanafunzi watafikiri kwa upana na kujibu maswali wenyewe. |
| **Tathmini ya mwalimu** | Lengo la mwalimu limefikiwa. | | |

## SEHEMU YA III: UUNDAJI WA MADA

# MADA KUU YA 1: Matumizi ya Lugha Katika Mazingira Mbalimbali

1

## MADA NDOGO YA 1: MSAMIATI KATIKA MAZINGIRA YA BENKI

**Uwezo Upatikanao katika Mada:** Kusikiliza kwa makini, kusoma vifungu vya habari na kutumia msamiati muhimu katika mazingira ya benki.

### Ujuzi wa Awali

Katika mada zilizotangulia wanafunzi walisoma masomo yenye uhusiano na mada hii kama vile, katika kidato cha pili walisoma kuhusu kilimo na ufugaji, utalii, kidato cha nne somo kama faida za michezo pamoja na msamiati katika mazingira ya hospitali. Baada ya kusoma masomo haya, wanafunzi wana ujuzi utakaowasaidia kuelewa masomo yanayozingatia mambo yafuatayo:

- Uinuaji wa uchumi kwa kujiunga na benki.
- Ukuzaji wa matumizi ya lugha kimazungumzo.
- Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali.

### Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada.

Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, michoro au picha, utumiaji wa msamiati katika sentensi, matumizi ya lugha na katika mazoezi au kazi na sarufi mwalimu aingize masuala mtambuka yafuatayo:

1. Mafunzo kuhusu uzalishaji mali
2. Mafunzo kuhusu amani na maadili
3. Mazingira na maendeleo endelevu
4. Usawa wa kijinsia
5. Elimu jumuishi: Mwalimu lazima atafute mbinu za kuwasaidia wanafunzi wenye matatizo maalumu.

### Mwongozo kuhusu Kazi Inayotangulia Mada

- Mwalimu awape wanafunzi mwelekeo wa kutoa majibu kwa kazi.
- Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni. Wakati huo mwalimu awasaidie kufanikiwa kwa kupitia kazi nyingine zilizotayarishwa au masomo ya mada yote.

## Orodha ya Masomo na Tathmini

| Masomo | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza: maarifa na ufahamu, stadi, maadili na mwenendo mwema | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | Benki na shughuli zake | Maarifa na ufahamu: Kuelezea jinsi ya kupelekea na kutoa pesa katika benki.<br><br>Stadi: Kuchagua msamiati wa kutumia katika mazingira ya benki.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kujivunia fahari juu ya ushirikiano kati ya meneja na benki katika njia ya maendeleo ya nchi. | 8 |
| 2 | Manufaa ya benki | Maarifa na ufahamu:Kujadili umuhimu wa benki<br><br>Stadi : Kulinganisha na kutofautisha manufaa mbalimbali ya benki<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kutimiza wajibu wa kujitegemea na kujitafutia ajira kwa ushirikiano na benki. | 12 |
| 3 | Aina za benki | Maarifa na ufahamu: Maana ya benki<br><br>Stadi: kutofautisha na kulinganisha benki mbalimbali<br><br>Maadili na mwenendo mwema: Kutumia wajibu wa kujitafutia ajira kwa kushirikiana na benki fulani. | 8 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4.Watumishi wa benki na majukumu yao | | Maarifa na ufahamu: Kubaini mahusiano ya watu wanaopatikana benkini.<br><br>Stadi: Kutofautisha na kuhusisha majukumu ya watumishi wa benki.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: Kubainisha majina ya watu mbalimbali na kazi zao katika benki. | 8 |
| 5. Karatasi maalum zinazotumiwa katika benki. | | Maarifa na ufahamu: Kutambua viambishi vya kitenzi kwa kutumia mnyambuliko wa vitenzi.<br><br>Stadi: Kulinganisha aina za karatasi maalum zinazotumiwa katika benki.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: Kutimiza wajibu wake wa kutumia karatasi hizo. | 8 |
| Tathmini ya mada | | | |
| Vipindi vyote vya mada ya kwanza | | | 44 |

## SOMO LA 1: BENKI NA SHUGHULI ZAKE

### 1.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi

Mada hii inajikita kwenye msamiati kuhusu mazingira ya benki. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza habari ili ajue hali yao. Wanafunzi nao wanamwamkia mwalimu kisha mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu ujuzi wa benki na shughuli zake.

Mwalimu anaweza kutumia maswali yafuatayo:

a. Je, miongoni mwenu, kuna aliyefika benki?

b. Je, mkitaka kununua vifaa vya shule mnatumia nini?

c. Mkiwa na pesa na mkitaka kuzihifadhi kwa usalama, mtazihifadhi wapi?

d. Benki ni nini?

e. Elezeni umuhimu wa benki.

## 1.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Vifaa vitakavyomsaidia mwalimu ni kama hivi:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- Kitabu cha mwanafunzi
- Pesa
- Magazeti na majalida mbalimbali
- Ubao, chaki
- Michoro kuhusu benki, n.k.

Inamlazimu mwalimu kuandaa vifaa tofauti vitakavyomsaidia kufanikisha somo lake vizuri bila kusahau wanafunzi ambao wana matatizo fulani. Ubunifu wa mwalimu katika maandalio ya zana za ufundishaji na ujifunzaji ni muhimu sana.

## 1.3. Kazi za ujifunzaji

Katika kufundisha somo hili mwalimu atatumia mbinu zinazofuata katika mistari ya hapo chini:

- **Utumiaji wa kazi za makundi:** Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne, n.k. Ni vizuri mwalimu kutozidi wanafunzi watano katika kundi moja ili kila mwanafunzi ashiriki katika kazi bila kuzembea. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini ili afuate jinsi kazi inavyofanyika katika makundi hayo. Mwalimu ahakikishe kuwa muda unatumiwa ifaavyo na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yaundwe kwa kuwachanganya wasichana na wavulana.
- **Mihadhara:** Mwalimu atumie njia ya kuwapa fursa ya kutoa hoja kuhusu benki. Wanafunzi wawasilishe kazi walizozifanya mbele ya darasa. Mwalimu aongoze kazi hiyo na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanatega sikio na kuuliza maswali wenzao papo hapo. Mwalimu awasaidie ajibu maswali magumu kwa wanafunzi.
- **Kazi binafsi:** Mwalimu awape kazi binafsi ili ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ameelewa somo vizuri na kuhakikisha kuwa lengo la somo limetimizwa. Kila mwanafunzi ajibu maswali pekee yake.
- **Maelezo ya mwalimu:** Mwalimu kwa tajiriba yake awaelezee wanafunzi pale ambapo anaamua kwamba wanahitaji maelezo zaidi kutoka kwake.
- **Uchunguzi wa kimatembezi:** Wanafunzi pamoja na mwalimu watatembelea benki katika eneo la karibu na shule yao.

## 1.4. Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watazame mchoro kwenye ukurasa husika kisha watoe maoni yao kuhusu kifungu "Penye nia pana njia".*

### 1.4.1 Zoezi la Ufahamu

***Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wanafunzi washirikiane kwa kutoa majibu:***

1. Familia inayozungumziwa katika kifungu hiki ni ya na Bwana Migambi na Bibi Shirubute..
2. Shirubute alikuwa na tatizo la kwenda kujifungua .
3. Migambi aliwatembelea marafiki zake kwa lengo la kuwaomba mkopo wa fedha.
4. Baada ya kutoka zahanati, Migambi na mkewe walipanga kujiunga na benki.
5. Baada ya kukubaliana na mkewe Migambi aliamua kupanga miradi na kwenda benki kuomba mikopo.
6. Migambi alielezewa kuhusu huduma za benki.
7. Msimamo wa bwana Migambi ulikuwa ni kufungua akaunti katika benki.
8. Mwalimu atathmini maelezo yanayotolewa na wanafunzi kuhusu mapokezi ya afisa wa huduma kwa wateja. Anawapokea wageni kwa tabasamu na bashasha na kuwaonyesha wanapoweza kuhudumiwa.
9. Mwalimu atathmini majibu yaliyotolewa na wanafunzi kwa kutumia msamiati unaoonyesha jinsi benki inavyoboresha maisha ya wateja wake.

   Kwa mfano kuwapa mikopo ya kutimiza miradi yao, kupitishia mishahara kwa wafanya kazi wengine, n.k
10. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu somo wanalopata katika kifungu walichosoma.

    Kwa mfano: Kupanga mradi vizuri na kuenda benki kuomba mkopo kwa ajili ya kujistawisha.

### 1.4.2 Msamiati kuhusu Kifungu "Penye Nia".

**Zoezi la 2:*(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutoa maana ya maneno waliyopewa kuhusu kifungu.*

**Majibu:**

| Maneno | Maana. |
|---|---|
| 1. benki | a. shirika la fedha linalohifadhi na kukopesha fedha. |
| 2. mteja | b. Mtu anayekwenda kupata huduma kwenye benki. |
| 3. mkopo | c. Fedha zipatikanazo kwa makubaliano ya kuzirudisha pamoja na riba. |
| 4. fedha | d. pesa au faranga. |
| 5. bima ya afya | e. Mkataba wa kulipa fedha katika shirika la afya ili mtu aweze kupata matibabu kwa urahisi. |
| 6. keshia | f. Karani mtunza fedha na anayeshughulikia upokeaji na ulipaji wake. |
| 7. mwelekezaji | g. Mtumishi wa benki mwenye majukumu ya kupokea wateja wa benki. |
| 8. taasisi | h. Shirika au kampuni inayoshughulikia kazi fulani. |
| 9. mradi | i. Mpango fulani wa maendeleo |
| 10. riba | j. Faida anayoipata mtu aliyekopesha watu fedha. |
| 11. raia | k. Mtu mwenye haki ya kisheria kwa sababu ya kuzaliwa au kujiandikisha katika taifa fulani na anayeweza kushiriki katika shughuli za taifa hilo. |
| 12. Kampuni. | l. Shirika la kufanya biashara au shughuli nyingine. |

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika utungaji wa sentensi walizoziunda kwa kutumia msamiati waliopewa. Mwalimu achunguze kuwa wanafunzi wanatumia msamiati huo kwa njia ifaayo.*

**Kwa mfano:** 1. Migambi aliamua kufungua akaunti benki.

2. Ni muhimu sana kuhifadhi pesa benki.

### 1.4.4. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi:

Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili wachunguze mifano ya sentensi walizopewa kwa kutambua kauli zilizomo. Mwalimu awaelekeze ikiwa kuna swali awasaidie.

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kwa kujaza nafasi wazi kwa kutumia vitenzi vyenye kauli husika.*

1. alimkopesha
2. alipata
3. analimisha
4. alipelekwa
5. lilitendwa.

**Zoezi la 5 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kwa kutunga sentensi moja moja katika nafsi ya tatu umoja zenye kauli ya kutenda, kutendwa, kutendesha, kwa kutumia viambishi wanavyopewa.*

Kwa mfano:

1. Mwalimu alitenda jambo jema.
2. Migambi alipanga mradi vizuri
3. Wema hutendesha jambo zuri
4. Fulani anapangisha nyumba yake.
5. Tendo hili lilitendwa vizuri sana.
6. Mradi huu ulipangwa kwa uangalifu.

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaongoze kusoma maelezo kuhusu mnyambuliko wa vitenzi.

**Zoezi la 6: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawiliwawili, wanyambue vitenzi walivyopewa kwa kujaza jedwali na kuonyesha hali mwafaka. Mwalimu awaelekeze ikiwa kuna tatizo awasaidie.*

| Hali ya kutenda | Hali ya kutendea | Hali ya kutendesha | Hali ya kutendwa | Hali ya kutendana | Hali ya kutendewa | Hali ya kutendeana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kusoma | kusomea | kusomesha | kusomwa | Kusomana | kusomewa | kusomeana |
| Kucheza | Kuchezea | kuchezesha | kuchezwa | Kuchezana | kuchezewa | kuchezeana |
| Kupiga | Kupigia | Kupigisha | Kupigwa | Kupigana | Kupigiwa | Kupigiana |
| Kujenga | Kujengea | Kujengesha | Kujengwa | Kujengana | Kujengewa | Kujengeana |
| Kupenda | Kupendea | Kupendesha | Kupendwa | Kupendana | Kupendewa | Kupendeana |
| Kuimba | kuimbia | Kuimbisha | Kuimbwa | Kuimbana | Kuimbiwa | Kuimbiana |

**Zoezi la 7: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze wanafunzi kusahihisha sentensi walizopewa. Ikiwa kuna tatizo mwalimu awasaidie.*

1. Mwanafunzi yule anasomea kwenye shule yetu.
2. Mwalimu alimtendea Migambi jambo jema.

3. Benki inakopesha pesa wateja wake.
4. Mkulima alinufaishwa na mkopo wa benki.
5. Kiswahili kinafundishwa nchini Rwanda.
6. Akaunti inafunguliwa kwenye benki.
7. Migambi alifungua akaunti ya hundi.

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili wachague majibu sahihi kutoka parandesi kwa kujaza sentensi walizopewa, mwalimu awaelekeze, ikiwa kuna tatizo awasaidie.*

1. kufungua
2. amekubaliwa
3. alijijengea
4. Kinafundishwa
5. Wanapendana
6. Wanawapatia
7. walijitajirisha.

### 1.4.5. Matumizi ya Lugha:

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika makundi wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kujibu maswali kulingana na maelezo waliyopewa ikiwa kuna tatizo mwalimu awasaidie.

1. Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu namna benki inavyoweza kuchunga usalama wa fedha za mwekaji.

Kwa mfano kama kumuepusha mwekaji kutembea na pesa nyingi mkononi kila anapokwenda.

2. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu faida mteja anazoweza kupata kutoka benki.

Kwa mfano: Kupewa mkopo wa kuendesha mradi wake.

Kuhifadhiwa pesa zake mahali salama.

3. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu miradi inayopelekwa kwenye benki na kupewa mikopo.

Mfano: Mradi kama wa kilimo na ufugaji uliopangwa vizuri.

Mradi wa bishara.

4. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu namna benki inaimarisha uchumi na maendeleo ya raia.

**Kwa mfano:**

Benki inawakopesha fedha raia wakawa na uwezo wa kujitajirisha.

Benki inawatolea riba wale inayowahifadhia pesa.

5. Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu manufaa ya kuunganisha huduma za benki na mitandao ya simu ya mkononi.

**Kwa mfano:**

Mteja anaweza kutoa pesa kwenye akaunti yake kwa kutumia simu ya mkono akiwa kwake.

Huduma hii inarahisisha matumizi ya muda.

**Zoezi la 10 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu atathmini maneno yanayohusiana na benki ambayo wanafunzi waliyoandika.*

**Mfano:**

1. Akaunti
2. Mteja
3. Meneja
4. Hundi
5. Riba
6. Mkopo
7. Mhasibu
8. Afisa wa mikopo
9. Pesa
10. Keshia.

### 1.4.6.. Kusikiliza na Kuzungumza.

Mwalimu awaambie wanafunzi kujadiliana katika makundi ya wawili wawili kuhusu mada zilizotolewa:

1. Huduma zinazotolewa na benki kwa wateja wake
2. Benki kama njia mojawapo ya kujitajirisha.

Baada ya majadiliano, wanafunzi wawasilishe mbele ya wenzao.

### 1.4. 7. Utungaji:

Mwanafunzi atunge kifungu cha habari chenye aya nne kuhusu mada liyotolewa:

'Benki ni Taasisi Muhimu katika Kuinua Uchumi wa Wananchi'

Mwalimu atathmini namna wanafunzi wanavyoandika kifungu hicho na kuwasaidia ikiwa wanakutana na tatizo lolote.

## SOMO LA PILI: MANUFAA YA BENKI.

### 2.1. Ujuzi wa Awali

Mwalimu awaulize mwanafunzi mmoja mmoja maswali tofauti kuhusu somo lililotangulia kwa lengo la kutambua ikiwa wanafunzi wa wanayakumbuka yahusuyo benki na shughuli zake. Baada ya kujibu maswali hayo, mwalimu awambie wanafunzi wachukue vitabu vya Kiswahili na kutazama mchoro uliopo.

Kisha mwalimu awaulize wanafunzi kuhusu mchoro wanaoutazama. Anaweza kuwauliza maswali kama yafuatayo:

- Elezea kuhusu wahusika unaowaangalia kwenye mchoro
- Watu unaowatazama kwenye mchoro wana fikra gani?
- Watu unaowaona wanaenda wapi?
- Kuna uhusiano wowote kati ya kichwa cha habari na mchoro?

Kutokana na majibu ya wanafunzi kuhusu maswali waliyojibiwa, mwalimu awaombe wanafunzi kubainisha somo hili linaitwaje..

### 2.2. Zana au Vifaa vya Kujifunzia.

- Mchoro wa watu wanaoenda benki.
- Kitabu cha mwanafunzi
- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- Magazeti na majarida mbalimbali
- Ubao, chaki, kalamu, kamusi ya Kiswahili sanifu na vifaa vinginevyo vinavyoweza

kumsaidia mwanafunzi kuelewa somo vizuri na kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji msaada maalum.

### 2.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunza.

Mwalimu aandike kichwa cha masomo ubaoni, pamoja na malengo mahususi ya somo husika. Baada ya kuwagawa wanafunzi katika makundi kulingana na idadi ya vitabu vya wanafunzi, mwalimu awaombe wanafunzi wafunue kwenye ukurasa husika na kusoma kifungu cha habari kwa kimya'**Manufaa ya Benki'** na kuandika msamiati mpya wanaokutana nao. Kisha mwalimu awaulize maswali mbalimbali yahusuyo kifungu walichosoma kwa kuthibitisha ikiwa wamekielewa. Baada ya mwalimu kutambua namna wanafunzi wamesoma kimya na kuelewa kifungu, awaombe wanafunzi mmoja mmoja kusoma kwa sauti inayosikika na wengine wafuate mwenzao anayesoma. Mwalimu awaongoze wanafunzi kuelewa maana ya msamiati mpya. Halafu mwalimu awaongoze wanafunzi wafanye mazoezi yapatikanayo kwenye kitabu cha mwanafunzi wangali katika makundi ya wawili wawili. Mwalimu atoe msaada kunapohitajika. Wanafunzi wasahihishe kazi katika makundi yao kulingana na muda waliopewa kisha mwalimu awaombe kuandika majibu ubaoni chini ya mwongozo wake.

## 2.4. Majibu

**Zoezi la 1 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)*:** *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watazame mchoro kwenye ukurasa husika kisha watoe maoni yao kuhusu* manufaa ya benki. 1. Migambi na Izere.

2. Walikuwa na safari ya kwenda benki.
3. Walikuwa wanaenda kuomba mikopo.

### 2.4.1. Maswali ya Ufahamu.

***Majibu ya ufahamu.***

**Zoezi la 2 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)*:** *Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kujibu maswali ya ufahamu.*

1. Kilichosababisha ni mahitaji ya kupata fedha nyingi zitakazowawezesha kuanziasha miradi mikubwa
2. Masharti muhimu yanayomfanya mtu aweze kupewa mkopo ni pamoja na: kuwa mteja wa benki husika, kuwa na akaunti hai,. Kuwa na dhamana ya mkopo unaoombwa, nakala za vitambulisho vya mwombaji, pamoja na barua ya maombi ya mkopo iliyoandikwa kwenda kwa meneja wa benki husika. Barua hiyo inapaswa pia kuambatanishwa pamoja na pendekezo la mradi unaokusudiwa kutekelezwa kutokana na mkopo huo.
3. Kwa kuwa walijua kuwa wanakidhi masharti yote ya mtu kuweza kupewa mkopo katika benki hiyo.
4. Walikuwa na akaunti za akiba
5. Maombi yao yalikubaliwa na benki.
6. Gakire alikuwa na mradi wa kujenga nyumba na kununua pikipi ya kubebea abiria. Izere yeye alikuwa na mradi wa duka la kuuza nguo zilizotengenezwa nchini Rwanda.
7. Gakire na Izere walihesabiwa kuwa ni watu wenye kuaminika kwa kuwa walikua na akaunti ambazo walikuwa wamezitumia kwa muda mrefu pasipo kuacha. Pia walikidhi vigezo vingine vyote..
8. Chanzo cha utajiri wao ni miradi waliyoianzisha baada ya kupata mikopo toka benki..
9. Vyama vya ushirika vina manufaa makubwa sana. Kwani vinawasaidia wanajamii kutatua shida ndondogo na kupata uzoefu wa namna bora ya matumizi ya pesa zao. Zaidi ya hivyo vinampa mtu nafasi ya kupata pesa ya kutunza benki.
10. Funzo ninalolipata ni kuwa ni muhimu kuzitumia benki kupata mitaji ya kuweza kuanzisha miradi mbalimbali.

### 2.4.2. Msamiati kuhusu Benki.

**Zoezi la 2: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaongoze kutoa maana ya maneno waliyopewa.*

1. Manufaa: Faida inayopatikana kutokana na kazi ama umuhimu wa kitu fulani.
2. Mchango: kusanyo la fedha.
3. Mgawo: ni kama fungu la vitu analopewa kila mtu anayehusika.
4. Kusuluhisha: Kuamua.
5. Mshiriki: Mtu anayejiunga na shirika ama idara fulani.
6. Dhamana: Kitu kitolewacho ndipo upewe mkopo katika benki.
7. Kutimiza ahadi: Kufuata mkataba.
8. Mashuhuri: -enye sifa na kujulikana sana.
9. Tajiri: mtu mwenye mali nyingi.
10. Kuhimiza: Kutia moyo mtu ili awahi kufanya haraka.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaongoze kwa kutunga sentensi zenye maana kamili wakitumia maneno waliyopewa na kutathmini majibu yao.*

**Kwa mfano:**

1. Ukiwa na pesa za kutosha unaweza kununua gari zuri.
2. Wakubwa kwa wadogo ni lazima kujilinda na Ukimwi.
3. Muzungu alipewa fungu lake.
4. Sisi sote tujiepushe na umaskini.
5. Kalisa aligundua umuhimu wa benki.
6. Shirika letu linahudumia vizuri.
7. Mwalimu ametatua tatizo la mwanafunzi.
8. Wanafunzi hawa ni marafiki sana.
10. Walienda sokoni kwa kukaza mwendo

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wajaze sentensi walizopewa, mwalimu awaongoze na kuwasaidia ikiwa kuna tatizo wanalolikuta.*

1. rika
2. walitolewa
3. Walipokewa
4. Mgawo
5. Afisa wa mikopo
6. Ukumbi
7. Zilizotengenezwa
8. Pato

9. Faida
10. benki.

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wawili wawili, wanafunzi wayahusishe maneno kutoka safu A na maana yake kutoka safu B. Mwalimu awaongoze kwa makini.*

1. C
2. E
3. B
4. H
5. D
6. I
7. A
8. F
9. G

**Zoezi la 6:** *(ukurasa wa 26)*

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kwa kujaza sentensi walizopewa.*

1. Biashara
2. Benki
3. Pikipiki
4. Barua
5. Afisa wa huduma kwa wateja.
6. Faida
7. Fedha.
8. Manufaa
9. Meneja.
10. Muda.

### 2.4.3. Sarufi: Mnyambuliko wa Vitenzi

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi waeleze viambishi vinavyounda vitenzi walivyopewa, mwalimu awaongoze katika kazi hiyo na kuwatolea msaada panapohitajika.*

1. Wanapendana: wa- na- pend-an-a
    - **Wa-:** Kiambishi awali cha nafsi.

- **na-:** kiambishi kati cha wakati ama cha njeo
- **pend-:** Mzizi wa kitenzi
- **an-:** kiambishi tamati tendana.
- **a:** kimalizio ama mwisho wa kitenzi.

2. Utapigwa: u- ta-pig-w-a
   - **u- :** Kiambishi awali cha nafsi
   - **ta-:** kiambishi cha kati cha wakati ama cha njeo
   - **pig-:** mzizi wa kitenzi
   - **w-:** Kiambishi tamati tendwa.
   - **a:** Kiambishi taamati ama kimalizio.

3. Alisimamisha: a-li-simam-ish-a
   - **a-:** Kiambishi awali cha nafsi.
   - **li-:** Kiambishi kati cha wakati.
   - **simam-:** mzizi wa kitenzi
   - **ish-:** kiambishi tamati tendesha
   - **a:** Kimalizio.

4. Alisomea: a-li-som-e-a
   - **a-:** Kiambishi awali cha nafsi
   - **li-:** Kiambishi kati cha wakati
   - **som-:** mzizi wa kitenzi
   - **e- :** Kiambishi tamati tendea
   - **a:** Kimalizio

5. Imevunjika: i-me-vunj-ik-a
   - **i-:** Kiambishi awali cha nafsi
   - **me-:** kiambishi kati cha wakati
   - **vunj-:** mzizi wa kitenzi
   - **ik-:** kiambishi tamati tendeka.
   - **a:** kimalizio

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu mwalimu awaelekeze kwa kutunga sentensi 5 kwa kutumia kitenzi 'kusoma' katika kauli walizopewa.*

1. Mwalimu anasomesha wanafunzi kitabu.
2. Gasaro anasomea shuleni kwetu..
3. Kitabu hiki kinasomeka kwa urahisi.

4. Habari ilisomwa jana.

5. Wanafunzi wawili wawili wanasomana kitabu.

### 2.4.4. Matumizi ya Lugha.

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili mwalimu awaelekeze kusoma maelezo na kujibu maswali husika.*

1. Mwalimu atathmini majibu yanayotolewa na wanafunzi kama mfano:

kupata mikopo kutoka benki, kupata riba, usalama wa pesa, n.k.

2. Mwalimu atathmini majibu yanayotolewa na wanafunzi.

**Kama mfano:**- Benki husaidia watu kupata mikopo ya kufanya biashara kama fedha . Kwani kama ambavyo maisha hayawezi kuendelea pasipo damu ndivyo ambavyo, biashara pia inahitaji pesa.

3. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu miradi inayoweza kupewa mikopo na benki kwa urahisi.

**Kwa mfano:** Kufanya biashara, kilimo na ufugaji, kujenga nyumba, kununua magari ya aina mbalimbali, n.k.

5. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu huduma mbalimbali za benki kwa wateja wake. Mfano: Kuwapa mikopo, kuwahifadhia pesa, kutuma pesa, , n.k.

### 2.4. 5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 10 :** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi, wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaambie wajadiliane kuhusu:*

1. Kujiunga na benki humaanisha kutajirika.

2. Faida za kuwa na akaunti katika benki.

### 2.4. 6. Utungaji:

**Zoezi la 11.** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wachague mada moja kati ya mada zinazopendekezwa, kisha watunge kifungu cha habari kwa kutoa hoja na maelezo kamili.*

1. Nafasi ya benki kwa kuimarisha usawa wa kijinsia nchini.

2. Umuhimu wa mikopo ya benki kwa wateja wake.

## SOMO LA 3 : AINA ZA BENKI

### 3.1. Ujuzi wa Awali/ Marudio/Utangulizi

Mada hii inajishughulisha na aina za benki. Wanafunzi wana ujuzi kutokana na masomo waliyotangulia kusoma katika mada hii ambayo yana uhusiano wa karibu sana na somo hili kama vile "Benki na shughuli zake na Manufaa ya benki. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi.

Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya. Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu aina za benki kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama mchoro ulioko kwenye kitabu cha mwanafunzi. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: Angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo:

- Elezea majengo unaoyaona kwenye mchoro huu
- Unafikiri nini kuhusu huduma zinazotolewa katika majengo yale?
- Kuna uhusiano gani kati ya mchoro na kichwa cha habari?

### 3.2 Zana za Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake,.ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufundisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili, Zana muhimu ni:

- KItabu cha mwanafunzi
- Mwongozo wa mwalimu

Michoro ya majengo mbalimbali.

……….. ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum kama wanafunzi wenye ulemavu.

Vifaa hivi vitaangaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu, ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

### 3.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atatilia mkazo kwenye:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** Kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji, ni lazima mbinu itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi wanatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi / mazoezi yake binafsi (Kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani.)
- **Maswali na majibu:** Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vile vile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumuuliza mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu.

  Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.

**Maelezo ya mwalimu:** Mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

## 3.4. Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswali wanayopewa kuhusu aina za benki.*

### 3.4.1. Maswali ya Ufahamu

1. Walikuwa wanazihifadhi ndani ya magodoro, chini ya mawe, katika shimo, katika pembe la ng'ombe na katika makasha ya miti.
2. Wanazihifadhi kwenye benki.
3. Inawapatia mikopo, Inawarahisishia kutuma pesa kwa haraka na usalama,, inawahifadhia pesa kwa usalama.
4. Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Taifa , Benki za Biashara na mashirika na vyama vya kifedha.
5. Watu wa rika zote.
6. Ina nafasi muhimu sana kwani inawapati mikopo na kuwawezesha kujiletea maendeleo.
7. Kuna akaunti ya Hundi, akaunti ya akiba na akaunti ya amana.
8. Inachunguza na kukagua matumizi yote ya fedha na kutunga sheria zihusuzo fedha na matumizi yake.
9. Inatoa mikopo na kuhifadhi pesa, kutuma pesa, .
10. nasaidia maendeleo ya nchi za dunia kwa njia mbalimbali.

### 3.4.2. Msamiati kuhusu Aina za Benki

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kwa kutunga sentensi zenye maana kamili kwa kutumia maneno wanayopewa*

1. Baba yangu alijiunga na benki ili arahisishe kazi za biashara yake.
2. Nitafungua akaunti katika benki ya wananchi.
3. Benki za kibiashara zinawakopesha wafanyabiashara
4. Shirika za fedha ni muhimu kwa raia.
5. Nitajiletea maendelea kwa kujiunga na benki.
6. Benki zinahifadhi pesa ya wananchi.
7. Serikali inahimiza watu wote kuwa na akaunti.
8. Dada alifungua akaunti .
9. Mfanyabishara yule ni mtu mwema.
10. Mteja atalipa deni baada ya mwaka

### 3.4.3. Sarufi kuhusu Mnyambuliko wa Vitenzi.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawli wawili wajibu maswali kwa kukamilisha sentensi wakitumia mnyambuliko wa vitenzi katika kauli ya kutendwa ,kutendeka na kutendea, mwalimu awaongoze kwa kujibu maswali hayo.*

1. wanafanyia
2. imejengeka/ilijengeka
3. lililimwa
4. Kiliandikwa
5. zinazofundishwa
6. alimlipia
7. Unapikika
8. Iliwanyeshea
9. ilifanywa
10. lililimika

### 3.4.4. Matumizi ya Lugha.

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaambie kusoma maelezo kwa makini kisha wajibu maswali husika.

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu

1. Benki inasaidia wateja kupata mikopo, kuwahifadhia pesa kwa usalama na kuwasaidia kutuma au kuhamisha fedha..

2. Inachunguza na kukagua matumizi ya kifedha nchini na kutunga sheria zihusuzo fedha

3. Inasaidia nchi za Afrika kujiendeleza.

4. Inasaidia nchi za dunia kujiendeleza

**Zoezi la5: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kwa kupanga maneno wanayopewa ili waunde sentensi zenye maana kamili.*

1. Vijana wa siku hizi wanapenda kuzurura mjini.
2. Tunapenda kusoma Kiswahili sana.
3. Mti uliangushwa na mvua kali.
4. Usafi unahitajika nchini kote.
5. Benki zina umuhimu sana kwa kuinua maendeleo.
6. Kuna aina mbalimbali za benki.
7. Nchini Rwanda kuna mahali pengi pa kuvutia.
8. Kila mtoto anapaswa kwenda shuleni.
9. Wazazi wangu walinifungulia akaunti.
10. Nyimbo zinafurahisha sana.

### 3.4.5. Kusilikiza na Kuzungumza.

**Zoezi la 6: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kujadiliana kuhusu mada wanazotolewa.*

1. Umuhimu wa benki kwa jamii.
2. Nafasi ya benki kwa kupunguza uhaba wa kazi. Kwa vijana

### 3.4.6 Utungaji:

Mwalimu awaambie wanafunzi kila mmoja atunge.kifungu cha aya tatu kuhusu mada wanayopewa.

‘Nafasi ya benki katika kuimarisha uchumi vijijini

## SOMO LA 4: WATUMISHI WA BENKI NA MAJUKUMU YAO.

### 4.1 Ujuzi wa Awali/ Marudio/Utangulizi

Mada hii inajishughulisha na watumishi wa benki na shughuli zao. Wanafunzi wana ujuzi kutokana na masomo yaliyotangulia yenye uhusiano na mada hii ambayo yana msamiati unaojikita katika mambo ya benki. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi.

Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya. Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu watumishi wa benki na majukumu yao. Mwalimu afanye chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama mchoro ulioko kwenye kitabu cha mwanafunzi. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: Angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo:

- Elezea wahusika unaowaona kwenye mchoro huu
- Unafikiri nini kuhusu huduma zinazotolewa katika benki?
- Kuna uhusiano gani kati ya mchoro na kichwa cha habari?

### 4.2 Zana za Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake,.ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufundisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili, Zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi
- Mwongozo wa mwalimu

Michoro ya watumishi wa benki .

……….. ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum kama wanafunzi wenye ulemavu.

Vifaa hivi vitaangaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu awe mbunifu, ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

### 4.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atatilia mkazo kwenye:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** Kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi wanatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi / mazoezi yake binafsi (Kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani.)
- **Mswali na majibu:** Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vile vile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumuuliza mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu.

  Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.

**Maelezo ya mwalimu:** Mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

## 4.4. Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswali wanayopewa kuhusu aina za benki.*

### 4.4.1. Maswali ya Ufahamu

1. Meneja.
2. Mhasibu, Afisa wa mikopo, keshia na afisa wa huduma kwa wateja.
3. Kutumia muda vizuri, kuhifadhi taarifa za akaunti ya mteja, kuhamisha pesa kwa haraka, kuunganisha na mitandao ya simu., n.k.
4. Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Taifa, benki za biashara.
5. Benki inatoa mikopo inayoweza kuleta maendeleo kwa jamii, kuwafundisha wanajamii miradi mbalimbali ya kimaendeleo, kuhamasisha matumzi mazuri ya pesa, kuhamasisha utunzaji mzuri wa pesa,, kuhifadhi pesa
6. Afisa wa huduma kwa wateja ni mtumishi muhimu, kwa sababu anawaelekeza wateja ili wapewe huduma wanayoihitaji kwa urahisi.
7. Mwalimu ahakikishe wanafunzi wanafanya mjadala na watoe majibu mengi kabisa: Wanajamii wanaopewa mikopo huweza kupata maendeleo, kupunguza uhalifu hasa wa uporaji wa fedha hasa kwa watu waliokuwa wakitembea na kiasi kikubwa cha fedha.pesa huhifadhiwa vizuri katika mazingira salama.

### 4.4. 2. Msamiati kuhusu Watumishi wa Benki na Majukumu yao

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kujibu maswali wanaopewa kuhusu msamiati wa watumishi wa benki na majukumu yao.*

1. Afisa kwa huduma kwa wateja
2. Meneja
3 Afisa wa mikopo
4. Mhasibu.
5.Keshia
6. Kuhudumia wateja
7. kufungua

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno waliyopewa.*

1. Watumishi wa benki wana majukumu tofauti.
2. Watumishi wa benki wanapokea watu vizuri.
3. Wajibu wa wazazi ni kulea watoto vizuri.
4. Mteja alifurahia huduma za benki.
5. Benki hii ina tawi moja mjini.
6. Siku hizi wanajamii wengi walifungua akaunti benkini.
7. Makeshia wanaripoti matumizi ya pesa.
8. Afisa wa huduma kwa wateja anapokea wateja kwenye benki.
9. Meneja anapiga sahihi kwenye faili la mteja.
10. Makao makuu ya Benki ya Taifa ya Rwanda yapo mjini Kigali.

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi, wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kwa kujaza sentensi walizopewa:*

1. Watimize
2.Faida
3. Vitengo
4. Mhasibu
5. kusimamia
6. Zinatoa Mchango

### 4.4.3. Sarufi kuhusu Mnyambuliko wa Vitenzi.

**Zoezi la 5: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi, wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze kutunga sentensi zenye maana kamili kwa kuzingatia hali ya kutendwa.*

1. Mpira unachezwa mahali popote.
2. Kiswahili kinasemwa na wanafunzi.
3. Ujumbe umetumwa kwa njia ya simu.
4. Nyimbo hizi zinaimbwa kanisani.
5. Akaunti yake ilifungwa jana.
6. Kiswahili kinazungumzwa na watu wengi.
7. Shamba lile lililimwa na watu wengi.
8. Vyombo hivi vitasafishwa na dada.
9. Nguo hii ilifumwa na nyanya.
10. Kiazi hiki kilichomwa na dada.

**Zoezi la 6: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwanafunzi afanye zoezi ,mwalimu amuelekeze kufika kwenye jibu sahihi.*

1. Alifungua
2. Waliofukua
3. Aliezua
4. Anaziba.

**Zoezi la 7: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika makundi , wanafunzi wawili wawili ,mwalimu awaelekeze waunganishe vifungu vya maneno kutoka sehemu A na maana yake katika SehemuB.

1. c
2. a
3. e
4. d
5. b
6. i
7. j
8. g
9. h
10. f

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kupanga maneno waliyopewa ili waunde sentensi sahihi.*

1. Simba ni mnyama mwenye nguvu.
2. Maji yakimwagika hayazoleki.
3. Izere anauzaa nguo zinazotengenezewa nchini Rwanda.
4. Utafanya mtihani wa Kiswahili lini?
5. Ni vizuri kuheshimu watu wote.
6. Wanaume na wanawake wanalingana nchini mwetu.
7. Kukopa harusi kulipa matanga
8. Mwindaji anaharibu mazingira.
9. Utafanya mazoezi haya kesho asubuhi.
10. Kiswahili kinatumiwa sana katika Afrika ya Mashariki.

### 4.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze watunge kifungu chenye mazungumzo kati ya afisa wa mikopo na mteja.

### 4.4. 6. Utungaji

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze watunge kifungu kuhusu mada waliyopewa.

'Huduma za benki uliyoitembelea na majukumu ya watumishi wake'

## SOMO LA 5: KARATASI MAALUMU ZINAZOTUMIWA KATIKA BENKI

### 5.1 Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi

Mada hii inajishughulisha kuhusu karatasi maalum zinazotumiwa katika benki. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya. Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu karatasi maalum zinazotumiwa katika benki, kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Mwalimu anaweza kuuliza wanafunzi maswali yanayohusiana na karatasi maalum zinazotumiwa katika benki.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama mchoro uliko kwenye kitabu cha mwanafunzi.Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro.

Anaweza kuwaambia angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo.

- Elezea wahusika unaowaona kwenye mchoro.
- Matukio haya yanafanyika wapi?
- Ni shughuli zipi unazoziona kwenye mchoro?
- Kuna uhusiano gani kati ya kichwa cha habari na mchoro?

## 5.2 Zana za Kujifunzia:

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi
- Mwongozo wa mwalimu
- Michoro ya watumishi wa benki , .
- ubao, chaki, karatasi kama hundi, stakabadhi na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum. Vifaa hivi vitaangaliwa kulingana na mazingira ya shule.

Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu, ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

## 5.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atatilia mkazo kwenye:

-Utumiaji wa makundi ya wanafunzi: Kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi wanatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi / mazoezi yake binafsi(Kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani.)
- **Maswali na majibu:** Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vile vile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumuuliza mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu.

Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.

**Maelezo ya mwalimu:** Mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele

Katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

Vifaa hivi vitaangaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu, ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

## 5.4. Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kutazama mchoro kisha wajibu maswali husika.*

### 5.4.1 Maswali ya Ufahamu

1. Akaunti ya mteja ilifungwa kutokana na kutotumika kwa muda mrefu
2. Hundi hutumiwa kuchukulia na kuwekea pesa benki.
3. Jina la mtu atanayetoa pesa, kiasi cha pesa, na sahihi .
4. Kadi inarahisisha kupata huduma ya kuchukua pesa wakati wowote hata kama sio muda wa kazi kwa wafanyakazi wa benki..
5. Kujaza jina lake kwa usahihi na nambari yake ya kitambulsiho pamoja na tarehe. Baada ya hapo huweka saini yake nyuma ya hundi aliyopewa..
6. Hundi hutumiwa kuchukulia na kuwekea pesa benkini, stakabadhi nayo huweza kutumiwa kwa kuweka na kutoa pesa kwenye akaunti ya mteja, Kadi ya benki nayo hutumiwa kwa kuchukulia pesa benkini.
7. Kibarua chake kilikuwa kikimalizika kwa hiyo mshahara wake ukasimama.
8. Alipokewa kwa ukarimu na meneja kisha akaelezewa yote kuhusu benki na akaunti yake ikafunguliwa tena.
9. Ndiyo. Lilitatuliwa kwani akaunti yake iliamshwa na kuendelea kuitumia.
10. Meneja alimwambia angoje ili akaunti yake ifunguliwe.

### 5.4.2: Msamiati kuhusu Karatasi Maalum Zinazotumika katika Benki.

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze watunge sentensi kwa kutumia maneno waliyopewa.*

1. Mteja alihitaji kutumia hundi.
2. Kadi ya benki hurahisisha huduma za kibenki.
3. Kijana yule alifungua akaunti benki.
4. Akaunti yake ilifungwa mwaka jana.
5. Mteja alipata uamuzi mzuri.

6. Kibarua chake kilimalizika.
7. Mama anapitishia mshahara wake benki.
8. Stakabadhi ni karatasi maalum ya kupokea au kutolea fedha.
9. Mteja alisahau nenosiri la kadi yake ya benki.
10. Keshia alipiga sahihi kwenye hundi ya mteja.

**Zoezi la 3: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wasome kifungu walichopewa kisha wajaze mapengo kwa kutumia maneno waliyopewa.*

1. Benki
2. Kuinua
3. Kujiunga
4. Akaunti
5 Kutoa
6. Kuomba
7. Wateja
8. Meneja
9. Mhasibu
10. Hundi

## 5.3: Sarufi kuhusu Mnyambuliko wa Vitenzi.

**Zoezi la 4: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wasome sentensi kisha wajibu maswali waliyopewa.*

| Hali yakinishi | Hali ya kanushi |
|---|---|
| 1 wanafunzi wote wanasoma Kiswahili | Wanafunzi wote hawasomi Kiswahili |
| 2. Watoto wanapigana | Watoto hawapigani |
| 3. Wazee wanashindana katika mbio zozote | Wazee hawashindani katika mbio zozote. |
| 4. Hadithi ilisimuliwa na bibi yangu | Hadithi haikusimuliwa na bibi yangu |
| 5. Mvua imemnyeshea Fulani | Mvua haijamnyeshea Fulani. |

| | |
|---|---|
| 6. Ng'ombe wanafugwa nchini kote | Ng'ombe hawafugwi nchini kote |
| 7. Mkulima yeyote anaboresha shamba kwa hali ya juu. | Mkulima yeyote haboreshi shamba kwa hali ya juu. |

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwanafunzi asome sentensi kwa makini, mwalimu amuelekeze achague jibu sahihi la kujaza nafasi.*

1. Wanapewa
2. Amenifulia
3. Kimevunjika
4. Walisalimiana
5. Kupendwa
6. Ameninunulia
7. Kusoma
8. Wanafurahia
9. Anapendwa
10. Haulizwi

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwanafunzi atunge sentensi tatu tatu kwa kutumia mnyambuliko wa vitenzi alivyopewa.*

*Kauli ya kusababisha:*

1. Mwalimu alitufundisha kulinda mazingira
2. Mteja alionyesha msimamo wake mzuri.
3. Mtoto anaandikisha kalamu.

Kauli ya kutendwa

1. Miti hii ilipandwa mwezi uliopita.
2. Bima ya afya inalipwa kila mwaka.
3. Barabara hii ilitengenezwa vizuri.

### 5.4. 4 Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze waangalie mraba kwa makini kisha watafute maneno yanayohusiana na benki.*

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | T | A | K | A | B | A | D | H | I | P |
| Y | O | T | E | K | A | D | I | A | H | E |
| M | T | E | J | A | N | A | O | T | I | S |
| K | A | L | O | U | K | B | P | A | L | A |
| N | N | E | F | N | A | N | I | A | A | O |
| B | A | M | O | T | B | E | N | K | I | Y |
| G | Y | K | I | I | N | I | H | U | S | U |
| T | A | R | A | K | I | L | I | S | H | I |
| K | U | T | A | N | B | U | A | A | N | O |
| T | U | M | I | K | A | V | I | Z | A | B |
| H | U | N | D | I | N | A | F | A | S | I |

**Majibu:**

1. Pesa
2. Stakabadhi
3. Mteja
4. Benki
5. Tarakilishi
6. Hundi
7. Kadi
8. Akaunti

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika makundi wanafunzi wachague moja kati ya mada wanazopewa, mwalimu awaelekeze, kisha watunge kifungu cha aya tatu

1. Umuhimu wa nyaraka zinazotumiwa benki.

### 5.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

Katika makundi wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze, wajadiliane kuhusu mada walizopewa.

'Umuhimu wa kutoa huduma nzuri kwa wateja wa benki.'

### 5.4.6. Utungaji

Mwalimu amuelekeze mwanafunzi kutunga kifungu cha aya tatu kuhusu mada aliyopewa.

"Umuhimu wa kuwa na akaunti benki"

### 5.5. Muhtasari wa Mada

Mada hii ya kwanza**"Msamiati katika mazingira ya benki"** ina masomo matano yanayohusiana na mada husika. **Somo la kwanza** linawahimiza watu kujiunga na benki kutokana na umuhimu wake. **Somo la pili** linashughulikia umuhimu wa benki kwa kuinua uchumi na maendeleo ya wananchi. **Somo la tatu** linatoa maelezo kuhusu benki mbalimbali na matumizi yake kwa kuboresha maisha ya wananchi.. **Somo la nne** linaeleza watumishi wa benki na majukumu yao. **Somo la tano** linaelezea kuhusu nyaraka maalum zinazotumiwa katika benki na namna ya kuzitumia. Kila kipengele kinaundwa na vipengele vidogo vidogo kama vile maswali ya ufahamu, msamiati, matumizi ya lugha na sarufi.

### 5.6. Maelezo ya Ziada

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada. Ni ya kumsaidia mwalimu katika ujuzi wa masomo anayoyafundisha. Maelezo ni haya:

- Benki ni taasisi au shirika la fedha linalohifadhi na kukopesha fedha kwa wateja wake wanaotaka kuendesha miradi yao mbalimbali.
- Miradi hiyo huweza kuwa ya kuzalisha mali kama vile kufanya biashara, kushughulikia kilimo na ufugaji, ufinyanzi, kufyatua matofali, kununua magari ya abiria na kubeba mizigo, kujenga nyumba za kupangisha, n.k.
- Benki ina lengo la kuimarisha uchumi na maendeleo ya raia.
- Benki inaweza kuwa njia moja ya kujitajirisha kwa kupewa mkopo na kuutumia ifaavyo.
- Ukipewa mkopo wa benki unaurudisha pamoja na riba.
- Benki hushauri watu wote kuipeleka pesa zao ili izihifadhi kwa usalama.
- Benki inamtoa mtu katika hatari ya kubeba fedha chungu nzima kila mahali alipo.
- Kulingana na maendeleo ya teknolojia, huduma za benki kwa wateja zilirahisishwa sana hata kuunganishwa na mitandao ya simu za mkononi.

Kuna aina mbalimbali za benki kama vile mfano wa Benki ya Taifa ambayo ni benki kuu nchini inayochunguza na kupanga sheria za kifedha nchini. Kuna benki za biashara ambazo hutolea mikopo wafanyabiashara ili wajiendeleze katika nyanja ya uinuaji uchumi wao. Kuna tena vyama vya kifedha na mashirika ya kifedha ambayo husaidia watu kujiepusha na umaskini.

Kuna benki zisizo za kawaida kama vile BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA AfDB ambayo majukumu yake ni kuwasaidia wanachama kujiendeleza kiuchumi. Kuna BENKI ya DUNIA: Benki hii ni taasisi ya kimataifa yenye malengo ama shabaha ya kusaidia maendeleo ya nchi za dunia. Siyo benki ya kawaida. Hii inashirikiana na umoja wa kimataifa na hasa shirika la kifedha la kimataifa. Haitumiki chini ya Umoja wa kimataifa bali ni mali ya wanachama 184. Makao makuu yake yapo mjini Washington DC nchini Marekani.

Kwa upande mwingine, benki inapaswa kuwa na watumishi wenye majukumu mbalimbali ambao wanatumia vifaa mbalimbali kwa kuhudumia wateja. Vifaa hivo ni vya aina mbalimbali kama vile hundi, stakabadhi, kadi ya benki, n.k. Nyaraka hizi hutumiwa na wateja wa benki na hujazwa kwa kutoa au kupewa huduma tofauti za benki.

## 5.7. Tathmini ya Mada ya Kwanza

Hii ni sehemu ya majibu ya tathmini ya mada ya kwanza kutoka katika kitabu cha mwanafunzi.

1. Benki ya Taifa, Shirika za Kifedha.

2. Nyaraka hizo ni pamoja na hundi, na stakabadhi za kuwekea au kutolea pesa.

3. Meneja kiongozi mkuu wa tawi la benki,

Mhasibu huhusisha uwekaji hesabu wa pesa ,

Afisa wa mikopo huajibika kwa kupokea faili za kuomba mikopo na mambo yote yahusuyo mikopo.

Keshia ni karani mtunza fedha anayeshughulikia upokeaji na ulipaji fedha.

Afisa wa huduma kwa watejani yule anayepokea vyema watu wote wanaokuja benki.

4. Inarahisisha huduma,kutumia muda ifaavyo, kutotembea na pesa chungu nzima mkononi.

5. Inasaidia raia kujiendeleza kimaisha kupitia njia za mikopo wanayopewa.

## 5.8. Mazoezi ya Nyongeza

### 5.8.1 Mazoezi ya Urekebishaji

1. Eleza maana ya benki.
2. Eleza umuhimu wa benki kwa raia.
3. Jadili kuhusu aina za benki nchini Rwanda.
4. Jadili kuhusu watumishi wa benki na majukumu yao.

### 5.8.2. Mazoezi ya Jumuishi

1. Tofautisha karatasi maalum zinazotumiwa benki.
2. Changanua huduma zinazotolewa katika benki.

### 5.8.3. Mazoezi ya Wanafunzi wenye Ujuzi wa Hali ya Juu

1. Wewe ni meneja wa benki fulani, himiza watu wasiojiunga na benki umuhimu wa kuwa mteja wa benki.

## SOMO LA 6: HADITHI FUPI

### 6.1 Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi

Somo hili linahusu hadithi fupi za fasihi andishi na linagusia vishazi huru katika sehemu ya sarufi. Wanafunzi wana ujuzi wa awali ambao utawasaidia kusoma somo hili. Katika vidato vilivyotangulia na katika masomo ya kidato cha sita yaliyotangulia somo hili wanafunzi walisoma :

- Hadithi za fasihi simulizi
- Msamiati katika mazingira mbalimbali
- Ushairi
- Virai

Katika somo hili, mwalimu aanze kwa kuwauliza wanafunzi maswali ambayo yatawasaidia kukumbuka pamoja na kuzingatia masomo waliyoyasoma yaliyotangulia. Kisha mwalimu awachangamshe wanafunzi na awapatie wanafunzi kazi ambazo zitawaingiza katika somo jipya. Awaulize maswali kwenye makundi ili wanafunzi pekee wagundue somo ambalo linatarajiwa kusomwa.

Kazi ya kuwaingiza wanafunzi katika somo husika ifanywe kwa kuwaomba wanafunzi kutazama michoro inayohusiana na mdahalo na mjadala inayopatikana kwenye kitabu cha mwanafunzi, kisha wajibu maswali yanayoambatana na michoro, kutokana na mitazamo pamoja na majibu tofauti kutoka kwa wanafunzi, mwalimu ajiegemeze kwenye maoni na mitazamo tofauti ya wanafunzi, aanzishe somo jipya.

### 6.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia

Mwalimu atafute na atumie ipasavyo vifaa ambavyo vitamsaidia kutimiza malengo ya somo. Baadhi ya vifaa ni pamoja na:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Majarida,
- Rikoda,
- Vinasa sauti,
- Simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati, mtandao wa intaneti na vinginevyo.

Mwalimu anaweza kutafuta zana nyingine ambazo hazikuorodheshwa hapo juu kulingana na upatikanaji wa zana hizo.

### 6.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia

Katika kipindi hiki, mwalimu atafute mbinu mwafaka zinazomwezesha kufanikisha malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atumie baadhi ya mbinu hizi:

- **Njia shirikishi:** Wanafunzi wagawanywe katika makundi na mchango wa kila mwanafunzi katika kundi udhihirike. Mbinu hii itumike kwa sehemu ya kusoma hadithi, maswali ya ufahamu, maelezo muhimu pamoja na sarufi.

- **Njia isiyo shirikishi:** Kila mwanafunzi apewe kazi yake binafsi kwa kufanya kazi ya nyumbani, kutunga sentesi, kujibu maswali kuhusu sarufi na utungaji.
- **Maswali na majibu:** wanafunzi waulizane maswali kati yao na kuyatolea majibu wao wenyewe kwa kusaidiwa na mwalimu, mwalimu naye awaulize wanafunzi maswali na wayatolee majibu hasahasa kwenye sehemu ya ufahamu, sarufi na matumizi ya lugha.
- **Majadiliano:** Wanafunzi wapewe mada tofauti na wazijadili katika makundi madogomadogo wakielekezwa na mwalimu.

## 6.4 Majibu

Mwalimu amuombe kila mwanafunzi ajibu maswali haya kwa kushirikiana na mwenzake katika jozi.

### 6.4.1 Majibu ya Ufahamu

1. wanakijiji wote waliskitishwa na tabia za Ndishoboye kwa sababu alikuwa na majivuno , na alikuwa anawakejeli wanakijiji wengine na hakutaka kushirikiana nao katika shughuli za kuendeleza kijiji.

2. Ndishoboye alikuwa anaishi katika kijiji cha Ubwiza. Mke wake alikuwa anaitwa Subira.

3. Mke wake Ndishoboye alikuwa mwanamke mwenye utulivu na aliwajibika kwa kila kazi iliyomsubiri mpaka ikamalizika.

4. Ndishoboye alipowaalika wanakijiji, hawakuja, wengi walimjibu kwamba wangekuja siku nyingine.

5. Kilichowafanya waalikwa wa Ndishoboye kushikwa na bumbuwazi na kuondoka mmoja baada ya mwingine ni maneno mabaya yanayojaa matusi na majivuno waliyoambiwa na Bwana Ndishoboye.

6. Wafanyakazi wa Ndishoboye wakati walipoelemewa na ukatili wake waliamua kwenda zao na kutafuta kazi kwa majirani wengine.

7. Ndishoboye alipoishiwa na mali yake, alibaki na gari. Hakutaka kuliuza kwa sababu ya majivuno yake.

8. Wakati Mugenzi alipofika mahali Bwana Ndishoboye alipopatwa na ajali alisimamisha gari lake na kumpeleka hospitalini.

9. Ndishoboye alipendekeza kuhamia katika kijiji kingine kwa sababu alikuwa hataki kuvumilia aibu mahali alipostahili kupewa heshima.

10. Mwishoni, Ndishoboye alibadilika,ili kufuta dalili ya tabia zake mbaya aliwaahidi wanakijiji kwamba hangemtendea mtu yeyote jambo baya.

### 6.4.2. Msamiati kuhusu Hadithi

**Zoezi la tatu:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno waliyopewa kwa kuchunguza matumizi yake katika kifungu « Penye Nia Pana Njia ».*

**Baadhi ya sentensi pendekezwa :**

1. Ndishoboye alizoea **kudharau** wanakijiji wengine lakini mwishoni alibadilika.
2. Wanakijiji wa Ubwiza hawakufurahishwa na tabia mbaya za Ndishoboye za **kunyanyasa** watu.
3. Mume alipoanza kuzingatia **pendekezo** la mkewe, alianza kupata manufaa.
4. Wanakijiji wa kijiji cha Ubwiza walikuwa **watu wenye utu** kwa sababu walidumisha amani na ushirikiano miongoni mwao.
5. Wauguzi walimtunza mume wa Subira mahali pasafi mpaka alipoanza **kupata nafuu.**
6. Mambo mabaya aliyoyatenda yalimsababisha **kuona haya** akaamua kurekebisha tabia zake mbaya.
7. Alipokubali kosa,**alisamehewa** akashirikiana na wengine katika shughuli za kuendeleza kijiji.
8. Subira alipata **uamuzi** wa kuhifadhi pesa zake benki ili zisitumiwe ovyo.
9. Mugenzi alikuwa **mtu mwemakw**a sababu alimpeleka mnyonge hospitalini.
10. Kila mtu analazimika kushirikiana na **majirani** katika kutekeleza shughuli za kujiendeleza na kuendeleza nchi kwa ujumla.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi waelekezwe jinsi ya kufanya kazi hii kwa kutumia mshale na kuhusisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B.*

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| **B** | E | g | j | a | H | c | i | f | b | d |

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kila mwanafunzi ajaze sentensi kwa kutumia maneno aliyopewa kwa kuzingatia maana ya kila neno. Mwalimu awaelekeze wanafunzi na ahakikishe ikiwa kila mwanafunzi anafanya zoezi.*

**Majibu** kushukuriwa, maumivu, msamaha, tajiri wa kupindukia, kujuta, maisha mapya, alisikitishwa, alihesabu, kumkejeli, aliandaa

1. **Tajiri wa kupindukia** analazimika kushiriki katika miradi mikubwa ya kuendeleza kijiji chake pamoja na nchi.

2. Mwanakijiji mmoja **alisikitishwa** na tabia za baadhi ya wanakijiji wasiokubali kushirikiana na wengine.

3. Mtu ambaye ana mwenendo mwema anastahili **kushukuriwa.**

4. Ndishoboye **alihesabu** siku zilizopita bila kufanya jambo zuri akajuta.

5. Kama wewe ni tajiri, si vizuri **kumkejeli** mtu ambaye hana uwezo wa kiuchumi.

6. Alipopata **maumivu,** jirani yake alimsaidia na kumpeleka hospitalini.

7. Walipoanza kushirikiana na wengine, walipata amani kisha wakaishi **maisha mapya.**

8. Ili aendeleze amani na maadili katika kijiji chake, yeye **aliandaa** sikukuu nyumbani kwake.

9. Mume alipoona pesa zilizohifadhiwa na mke wake alianza **kujuta** kwa sababu ya mambo mabaya aliyokuwa anayatenda kwa mke wake.

10. Ndishoboye aliomba **msamaha**, tangu wakati huo aligeuka mtu mwema kijijini.

### 6.4.3 Sarufi : Virai nomino

**Zoezi la 5** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaombe wanafunzi kutazama sentensi katika vitabu vyao, wajibu maswali mmoja baada ya mwingine. Zoezi hili lifanyike kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili. Wanafunzi wawasilishe kazi. Mwalimu awaelekeze kwa majibu sahihi.*

**Zoezi la 6** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kazi hii ifanyike kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Baada ya maoni kutoka kwa wanafunzi, mwalimu awaelekeze kwenye ukurasa wa maelezo ya ziada katika kitabu cha mwanafunzi.*

**Majibu pendekezwa**

1. **Duka kubwa** linajaa vitabu.
2. **Mtoto aliyetusimulia hadithi jana** ameingia ukumbini.
3. **Mimi na dada** tulianza mazoezi ya kutunga riwaya.
4. **Mucyo na Mugabo** huwapokea wageni vizuri.
5. **Adili na Nduguze** ni riwaya iliyoandikwa na Shaaban Robert.
6. **Watoto wengine wenye maadili mema** wametutembelea.
7. **Mgeni mpole** amemtembelea rafiki yangu.
8. **Mwenyekiti na katibu** huongoza mdahalo.

### 6.4.4. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu aombe wanafunzi wawili wawili watafute kwenye jedwali maneno ya Kiswahili sanifu yanayotumiwa katika hadithi, kisha mwalimu awaombe wanafunzi kuandika majibu ubaoni (mwanafunzi mmoja baada ya mwingine).

**Majibu pendekezo:**

1. MWANDISHI
2. WASOMAJI
3. NOVELA
4. MUUNDO
5. MAZINGIRA
6. MBIO
7. IMARA
8. ORODHESHA
9. RANCHI
10. GHAIDHI

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma tena hadithi fupi " Penye Nia Pana Njia". Kila kundi lipewe swali moja kati ya haya yanayofuata:*

1. Toa maana ya hadithi fupi.
2. Unaionaje fani ya hadithi ile?
3. Kwa kujiegemeza kwenye hadithi fupi uliyoisoma, eleza maana ya dhamira katika hadithi.
4. Tofautisha fani na maudhui.
5. Eleza dhima ya hadithi fupi katika jamii.

Kila kundi lipewe dakika tano za kuwasilisha waliyoyafanya. Mwalimu ajiegemeze kwenye majibu yatakayotolewa ili aelekeze wanafunzi kupata ufahamu, stadi na maadili kuhusu hadithi fupi za fasihi andishi.

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili wasome maelezo muhimu kisha wajibu maswali kuhusu hadithi fupi. Mwalimu awaelekeze katika kuyasoma, kujibu maswali na kutoa suluhisho kuhusu matokeo ya zoezi.

**Majibu pendekezo:**

1. Hadithi fupi ni hadithi za kubuni kutoka tatika mazingira ambazo huhusishwa na matukio au mambo mbalimbali katika maisha ya watu. Hadithi hizi hukusudiwa kusomwa kuliko kuandikwa.

2. Katika hadithi fupi, maudhui ni jumla ya mawazo yote yanayozungumziwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu ya mawazo hayo. Maudhui hujumuisha mawazo pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma mwandishi kuandika kazi ya fasihi.

3. Tofauti kati ya aina na tabia za wahusika.

| Aina za wahusika | Tabia za wahusika. |
|---|---|
| Wahusika wakuu: Mhusika mkuu ni mhuska mmoja au wawili ambao hujitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi fupi.<br><br>Wahusika wadogo: Ni aina ya wahusika muhimu sana ambao humsaidia mhusika mkuu kuipa hadithi mwelekeo wa kisanaa na kimaudhui. | Wahusika bapa: Ni aina ya wahusika ambao hawabadiliki kitabia kutoka mwanzoni mpaka mwishoni mwa hadithi fupi.<br><br>Wahusika duara: Ni wahusika ambao wanabadilika kitabia kutokana na mabadiliko ya mazingira.<br><br>Wahusika foili: Ni wahusika wenye tabia zinazobadilika kinusu. Wako kati ya wahusika bapa na wahusika duara. |

4. Eleza sifa za hadithi.
    - Huwa fupi.
    - Huwa na wahusika wachache.
    - Hurejelea wazo au kisa kimoja tu.
    - Huandikwa kwa lugha ya moja kwa moja.
    - Huwa na muundo rahisi kueleweka.
    - Hufanyika katika mandhari au mazingira moja tu au chache.
    - Huwa na sifa ya kubuniwa.
    - Huwa na mhusika mkuu mmoja anayejitokeza sana kuliko wengine katika hadithi.
    - Huwa na wazo moja lililopewa uzito kuliko jingine lolote.
5. Dhima ya hadithi fupi katika jamii:
    - Hadithi fupi huelimisha.
    - Hadithi fupi huburudisha.
    - Hadithi fupi huadibu na hunasihi jamii. Kuna hadithi fupi ambazo hutungwa kwa madhumuni ya kuasa na kuadibu juu ya mambo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii.
    - Hadithi fupi hupiga vita kwa hali na mali mazingira yote ya ujinga, maradhi, njaa na umasikini.
    - Kuna hadithi fupi ambazo husaidia katika kujenga misingi ya demokrasia miongoni mwa umma wa wakulima, wafugaji na wafanyakazi wengine.
    - Hadithi fupi huwakosoa watu katika vipengele mbalimbali vya maisha yao.

### 6.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 10** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, kila kundi lichague mada moja kati ya mada mbili kisha waijadili kwa kuzingatia nafasi ya hadithi fupi katika fasihi andishi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuhakikisha ikiwa zoezi linafanyika ipasavyo. Kundi moja kwa kila mada lipewe muda wa kuwasilisha na mwalimu atoe suluhisho lake.*

1. Umuhimu wa hadithi katika jamii.

**Mawazo makuu pendekezo**

- Hadithi fupi huelimisha jamii.
- Hadithi fupi huburudisha.
- Hadithi fupi huadibu na hunasihi jamii. Kuna hadithi fupi ambazo hutungwa kwa madhumuni ya kuasa na kuadhibu juu ya mambo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii.
- Hadithi fupi hupiga vita kwa hali na mali mazingira yote ya ujinga, maradhi, njaa na umasikini.
- Kuna hadithi fupi ambazo husaidia katika kujenga misingi ya demokrasia miongoni mwa umma wa wakulima, wafugaji na wafanyakazi wengine.
- Hadithi fupi huwakosoa watu katika vipengele mbalimbali vya maisha yao.

2. Nafasi ya fasihi andishi katika kujikinga na magonjwa yanayoambukizwa.

**Mawazo pendekezo :**

- Hadithi fupi huweza kuzingatia ujumbe wa kuwaelezea watu namna magonjwa yanavyoambukizwa.
- Hadithi fupi huweza kuwa na ujumbe unaowaelezea watu madhara ya magonjwa yanayoambukizwa.
- Hadithi fupi huweza kuzingatia ujumbe anaosisitizia namna bora ya kujikinga dhidi ya magonjwa yanayoambukizwa.
- Hadithi fupi huwapa watu elimu inayowawezesha kupambana na vikwazo vinavyokumba maisha.

### 6.4.5 Utungaji

**Zoezi la 10:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kila mwanafunzi afanye kazi ya kuikamilisha hadithi aliyopewa. Hapa, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wanashiriki. Wanafunzi watano katika darasa wapewe fursa ili wachangie na wengine namna walivyoikamilisha hadithi fupi. Hapa mwalimu achunguze ikiwa wanafunzi wamekamilisha hadithi waliyopewa kwa kuzingatia vipengele vya fani na maudhui pamoja na kichwa cha hadithi fupi.*

# MADA KUU YA 2: Fasihi Katika Kiswahili

2

## MADA NDOGO: TANZU ZA FASIHI ANDISHI KATIKA KISWAHILI

**Uwezo Upatikanao katika Mada:** Kusikiliza, kusoma, kuzungumza na kuandika kwa minajili ya kuelewa lugha kama chombo cha mawasiliano katika jamii.

**Ujuzi wa Awali** Katika shule za awamu (kidato cha 1, 2,3,4,5), wanafunzi walisoma masomo ambayo yanahusu kidogo hii mada na yanaweza kuwasaidia kuelewa "lugha ya Kiswahili": masomo hayo ni:

- Uimarishaji wa stadi ya uandishi na masimulizi kupitia lugha ya Kiswahili: utungaji wa insha. ( mada ya nne, kidato cha tatu)
- Lugha na teknolojia : Kiswahili katika teknolojia ya habari na mawasiliano. (mada ya tano, kidato cha tatu)
- Ukuzaji wa matumizi ya lugha kimazungumzo. (mada ya tatu, kidato cha tatu.)
- Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali (kidato cha pili,)

### Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada

Masuala mtambuka yatakayoingizwa katika mada hii ni haya yanayofuata:

Elimu jumuishi,

Mafunzo kuhusu uzalishaji mali,

Mazingira na maendeleo endelevu,

Elimu kuhusu ufahamu wa ujinsia,

Mafunzo kuhusu amani na maadili.

### Maelekezo kuhusu Kazi

- Mwalimu anawapa wanafunzi mwelekeo wa kutoa majibu kwa kazi.
- Mwalimu atawasaidia kwa kupanga na kuigiza tamthilia: wanafunzi watapanga wao wenyewe lakini mwalimu atakuwa karibu nao kukamilisha kasoro zitakazojitokeza.
- Kuhusu utungaji wa insha na shairi ,wanafunzi watazitunga kwa mwelekeo na mada kutoka kwa mwalimu. Kazi binafsi zitalazimika kufanywa.

## Orodha ya Masomo na Tathmini

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6 | Hadithi fupi | Maarifa na ufahamu: Kubainisha mtindo wa tanzu za fasihi hasa hadithi fupi.<br><br>Stadi: Kujadili mchango wa fasihi andishi katika maendeleo ya kiutamaduni katika jamii husika.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: husika. | 8 |
| 7 | Ushairi katika Kiswahili | Maarifa na ufahamu: Kueleza mchango wa kila tanzu katika maendeleo ya kiutamaduni na kiuchumi ndani ya nchi<br>. 8<br><br>Stadi: Kujadili mchango wa fasihi andishi, hasa hasa shairi katika maendeleo ya kitamaduni,kijamii na kiuchumi katika nchi.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: | |
| 8. | Riwaya | Maarifa na ufahamu:<br><br>Kutaja mojawapo wa aina za riwaya katika Kiswahili.<br>8<br><br>Stadi : kulinganisha tanzu za fasihi andishi kutokana na muundo wa kila tanzu.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kupata mabadiliko ya kuhifadhi na kukuza utamaduni wa nchi kulingana na wahusika wanaojitokeza katika tanzu | |
| 9. | Nafasi ya tamthilia katika jamii | Maarifa na ufahamu: Kubainisha aina za tamthilia<br>8<br><br>Stadi: Kusikiliza kazi za za fasihi kutoka tanzu za fasihi andishi na kutafsiri tabia za wahusika katika tanzu husika..<br><br>Maadili na mwenendo mwema: kuimarisha kazi za sanaa kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani hata kufundisha kuhusu utamaduni na kuuhifadhi. | |

## SOMO LA 7: USHAIRI WA KISWAHILI

### 7.1. Ujuzi wa Awali/ Marudio/Utangulizi

Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi.

Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya. Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu Ushairi katika Kiswahili kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi wajigawe katika makundi na kutazama mchoro ulioko kwenye kitabu cha mwanafunzi.. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: Angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo:

- Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro huu
- Eleza kuhusu mavazi ya watu unaowaona kwenye mchoro huu?
- Eleza hali ya wazazi unaowaona kwenye mchoro huu.
- Kuna uhusiano gani kati ya mchoro na kichwa cha habari?

### 7.2 Zana za Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake,.ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufundisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili, Zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi
- Mwongozo wa mwalimu
- Michoro ya watu wa rika ya wazazi na vijana.

ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum kama wanafunzi wenye ulemavu.

Vifaa hivi vitaangaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu, ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

### 7.3 Mbinu za Kufundishia na kujifunzia

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atatilia mkazo kwenye:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** Kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu hii itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani.

Wanafunzi wanatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi /mazoezi yake binafsi. (Kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani.)
- - **Maswali na majibu:** Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Vile vile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumuuliza mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu.

  Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.
- **Maelezo ya mwalimu:** Mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele

katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

## 7.4. Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi wajibu maswali wanayopewa kuhusu shairi.*

### 7.4.1. Maswali ya Ufahamu

1. Vijana wanashauriwa kuvaa mavazi ya heshima.

2.a. Humaanisha kuwa mavazi ya heshima yanamfanya mtu kupendeza.

.b. Ni kama kusema kuwa mzazi asimuache mtoto kufanya atakalo kwani matokeo mabaya ya mtoto yanamfikia mzazi pia.

3. Wasichana wanashauriwa kuvaa vizuri kwani ndio wamama wa kesho.

4. Mtu ni kiumbe chenye akili na utu, ndiyo sababu inamlazimu kujiheshimu na kuheshimu watu wengine.

5.. Kuvaa vazi la heshima na kujiheshimu.

6 Ni mavazi yanayowabana sana, kuvua ni zahama, na mengine yanayoonyesha magoti wazi wakiinama.

7. Vijana wanavaa nguo zisizo za heshima.

8. Ni kulea watoto vizuri ili wawe na tabia njema na kuvaa nguo za heshima.

### 7.4.2 Msamiati: Kuhusu Ushairi.

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu amuelekeze mwanafunzi atunge sentensi kumi, atumie maneno aliyopewa:*

1. Heshima ni jambo muhimu maishani.
2. Kila mtu anapaswa kuvaa vazi la heshima.
3. Wazazi wachukue tahadhari katika malezi ya watoto.
4. Wasichana hawa wanavaa mavazi ya heshima.
5. Mtoto mzuri anafuata mashauri ya wazazi.
6. Rabuka anapenda viumbe wake.
7. Wazazi wanawalea watoto vizuri.
8. Vijana wavae nguo za heshima.
9. Mtoto yule ana adabu njema.
10. Mavazi yanayombana mtu si mazuri

**Zoezi la 3: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi wanafunzi,wawili wawili mwalimu awaelekeze,wakamilishe sentensi kwa kutumia maneno waliyopewa.*

1. Maungo wazi
2. vijana
3. Rabuka
4. Majirani
5. Heshima
6. Nyuso
7. Mkononi
8. Kuungama
9. Shauri.
10. Nguo

### 7.4.3 Sarufi kuhusu Matumizi ya virai.

Mwanafunzi achunguze kwa makini mifano ya sentensi alizopewa kisha ajibu maswali.

**Zoezi la 4: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ,mwalimu awaelekeze kwa kupigia msitari virai vitenzi alivyopewa katika sentensi.*

1. Watu wale <u>wanavaa mavazi mema</u>
2. Mzazi <u>aliwaona vijana wema.</u>
3. Wasichana <u>wanavaa mikufu shingoni</u>

4. Wazazi wanalea watoto vizuri
5. Rabuka aliumba viumbe wote.
6. Mtoto ana tabia nzuri.
7. Mzee aliambia watoto jambo muhimu.
8. Wanafunzi wanasoma Kiswahili
9. Dada yangu alitunga shairi jipya.
10 Baba na mama wanaenda sokoni.

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwanafunzi atunge sentensi tano kwa kutumia maneno aliyopewa.*

1. Mzazi anawashauri watoto kutoangalia sinema za mapigano.
2. Mama anatimiza dhima yake vema.
3. Jirani yetu ana huruma.
4. Babu anawaonya wajukuu wake.
5. Shemeji yangu ni mtu mwema.

### 7.4.4 Matumizi ya Lugha.

**Zoezi la 6** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wasome kisha wafanye zoezi husika.*

1. Ni mstari mmoja wa shairi.
2. Huitwa ubeti.
3. Tarbia
4. Kituo kibwagizo.
5. Vaa vazi la heshima, uchunge wako murua

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wajibu maswali waliyopewa.*

1. Ngonjera ni shairi lenye malumbano na majibizano kati ya watu wawili au wengi.

2. Ngonjera ni aina ya shairi lenye majibizano na malumbano kati ya watu wawili ama zaidi na upekee wake haiimbwi wakati shairi ni utungo wa kisanii wa kutumia lugha ya mkato na mnato, maneno teule yanayopangwa katika beti kwa kutoa ujumbe.

3. Shairi hili ni ngonjera kwa sababu kuna majibizano na malumbano kati ya daktari na mwalimu.

4. Ni kuonyesha kuwa si vizuri kudanganya..

5. mteja na seremala

**Zoezi la 8:(*Angalia katika kitabu cha mwanafunzi*)**

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao kwa kuhusisha maneno ya A na maana yake Katika sehemu B.

1. c
2. f
3. a
4. d
5. b
6. e
7. g
8. h
9. i
10. j

### 7.4.5 Kuzungumza na Kusikiliza

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao wajadiliane kuhusu

mada waliyopewa.

‘ Ushairi ni chombo muhimu cha kukuza na kuhifadhi utamaduni wa jamii”

### 7.4.6 Utungaji

Mwalimu amuelekeze mwanafunzi atunge shairi la beti mbili kuhusu Kulinda mazingira ya shule yake.

## SOMO LA 8: UFAFANUZI WA RIWAYA

### 8.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi

Ujuzi wa awali kwa wanafunzi katika somo hili unashuhudiwa na mambo yafuatayo :

- Walijifunza somo la fasihi katika kidato cha tano.
- Mitihani yote ya lugha ilikuwa inaligusia jambo hili.
- Walijifunza somo la hadithi fupi linalohusiana sana na hili.

### 8.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Vifaa vihitajiwavyo katika somo hili hutegemea aina ya kila zoezi. Kwa hiyo inambidi mwalimu atarajie zana husika kulingana na mahitaji ya wanafunzi. Mfano wa vifaa vinavyoweza kupendekezwa ni kama vifuatavyo:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Karatasi za manila na kalamu zake husika.
- Vitabu vya riwaya tofauti.

### 8.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia

Mwalimu achague mbinu inayofaa kulingana na aina ya zoezi husika. Kwa mfano:

Katika ufundishaji wa somo hili, mwalimu atumie mbinu zifuatazo:

- **Kazi za kimakundi:** wanafunzi washirikishwe katika mazoezi yanayofanyiwa katika makundi. Mwalimu aunde makundi kulingana na mpango wa zoezi.
- **Mjadala:** wanafunzi wafanye mjadala kulingana na mada zilizopendekezwa katika zoezi.
- **Fikiri – jozi – shiriki:** Baada ya maoni tofauti kutoka kwa wanafunzi, mwalimu anapata habari juu ya ujuzi wa awali wanafunzi wake walio nao kuhusu somo hii.
- **Kazi ya kibinafsi:** mwanafunzi afanye kazi ya kibinafsi wakati wa kufanya zoezi lililopendekezwa kufanywa kibinafsi. Mwalimu asahihishe zoezi hili pamoja na kumwonyesha makosa ya kurekebisha.

**Tanbihi:**

Mwalimu awahudumie kwa upekee wanafunzi wenye mahitaji maalumu kulingana na tatizo walilo nalo.

Kwa mfano:

- Amwaache akae mbele yule aliye na tatizo la kutoona vizuri kwenye ubaoni;
- Atumie lugha ya ishara kwa kumsaidia mwanafunzi aliye na tatizo la kusikia au kusema.

## 8.4. Majibu

### 8.4.1. Kidokezo

*Mwalimu ayaunde makundi matatu ya wanafunzi kulingana na idadi ya wanafunzi. Wanafunzi wajadiliane na wakichague kitabu kimoja walichokisoma. Wazungumzie kuhusu wahusika wake, migogoro pamoja na ujumbe wake kisha wajibu maswali. Kila kundi liwasilishe kazi mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe makosa yatakayojitokeza.*

### 8.4.2. Ufahamu

**Zoezi la 1 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu amwombe mwanafunzi kufanya kazi hii kibinafsi na kushirikiana kwa jozi kwa ajili ya kukamilishana.*

Majibu pendekezo

1. Adili, Rai, Ikibali, Hasidi na Mwivu, Mwelekevu, Huria

2. Kasoro iliyokuwepo nchini Ughaibu ilitokana na kuchelewa kuleta kodi.

3. Kila usiku Adili alikuwa anawapiga manyani.

4. Walipata ajali ya jahazi na mali yao ikapotea.

5 Adili aligawa mali yake na kila ndugu yake akafungua duka na kutajirika zaidi.

6. Kutokana na matendo mabaya waliyomfanyia nduguze Adili, Huria aliwageuza manyani. Alimlazimisha Adili kuwapiga kila siku.

7. Rai aliwaomba ndugu zake Adili kutotenda maovu. Kauli hii ni kweli. Watu wote wanapaswa kuacha kutenda mabaya, wakafanya mema. Ni vizuri kuwafanyia wengine mema na kuacha kuwatendea wengine mabaya.

8. Baada ya kusoma muhtasari wa Riwaya ya Adili na nduguze, nimepata somo kuwa ubaya hushindwa na wema . Katika riwaya hii, inaonekana kwamba watu wema huwa na bahati ya kufanikiwa lakini wale waovu mara nyingi hushindwa kutokana na matendo mabaya.

### 8.4.3. Msamiati

**Zoezi la 2 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi fulani. Kila kundi lipewe msamiati wa kutolea maana na kutunga sentensi binafsi. Baadaye kila kundi liwasilishe kazi yake.*

***Maana pendekezo:***

1. Kulaki : kuenda kupokea mtu au watu.
2. Malipo : jambo afanyalo mtu kulipia au kulipwa kwa kitendo fulani alichofanya.

3. Nyani: mnyama anayefanana na tumbiri lakini mkubwa zaidi mwenye rangi ya kaki ya kijivu na ngoko nyekundu matakoni.

4. Marehemu : mtu aliyefariki

5. Jahazi: chombo cha baharini kilichoundwa kwa mbao, cha kuchukulia abiria na bidhaa.

6. Jabali: mwamba mkubwa

7. Tandu: mdudu mwenye miguu mingi kadiri ya mia moja, huuma na ana sumu.

8. Kutoweka: Kupotea machoni; kukosa kuonekana

9. Kupatanisha: Kusuluhisha ugomvi wa watu wengine.

10. Kutesa: Kutia kiumbe maumivu au machungu kwa muda mrefu.

**Zoezi la 3 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Zoezi hii ifanywe kibinafsi, kisha kwa jozi.*

1—D

2—E

3—B

4—C

5—A

**Zoezi la 4: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kwa jozi wanafunzi washirikiane kujaza sentensi husika. Baadaye mwalimu amchague mwanafunzi atoe jibu lililojadiliwa.*

1. Wanafunz**i wametia nanga** Kwenye somo lao la leo.

**2. Punde si punde** mgonjwa yule atapona.

3. Mtoto yule **amepigwa na kiu** ndiyo maana anahitaji maji ya kunywa.

### 8.4.4. Sarufi: Vishazi Huru

**Zoezi la 5: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, wajadili kuhusu sentensi walizopewa kisha wapige mstari kwenye tungo zenye vitenzi vinavyojitosheleza.*

**majibu**

1. **Adili alipigwa** kwa sababu ya huruma aliyowatendea manyani .
2. Alipofika katika mji wa mawe, **Adili alikutana na Mwelekevu.**
3. **Adili alikuwa** na ndugu wawili walioitwa Hasidi na Mwivu.
4. Rai aliyekuwa mfalme wa ughaibu, **alipendwa sana na raia.**
5. Manyani waliposamehewa, **waligeuka watu.**

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili wasome maelezo muhimu kuhusu kishazi, kisha wajibu maswali kuhusu maelezo waliyoyasoma. Mwalimu awaelekeze katika kusoma, kujibu maswali na kutoa suluhisho kuhusu matokeo ya zoezi linalohusu vishazi.

**Majibu pendekezo:**

1. Kishazi ni tungo inayotawaliwa na kitenzi. Kitenzi hicho kinaweza kuwa kinajitosheleza au hakijitoshelezi katika maana; hasa kishazi huwa ndani ya sentensi kuu.

2. Kuna aina mbili za vishazi yaani kishazi huru na kishazi tegemezi.

3. Mifano mitano pendekezwa ambamo kuna vishazi huru.

    i. **Adili aliokolewa na ndege** aliyempeleka katika nchi ya maji.

    ii. **Asubuhi walienda Ughaibu**, wakaona kwamba kazi yake ilifaulu.

    iii. **Adili aliwaonya ndugu zake** ili wasitende maovu.

    iv. **Adili aliheshimiwa na wazazi wa Huria,** wakampa hundi ya pesa nyingi.

    v. Ndugu zake walipokataa kumuunga mkono, **Adili aliondoka yeye mwenyewe.**

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu amuombe kila mwanafunzi kutazama sentensi zinazopatikana katika kitabu cha mwanafunzi kisha amuombe kila mwanafunzi kupiga mstari kwenye vishazi huru. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kazi hii na awasaidie kufanya zoezi hili kwa ufasaha.*

1. **Wanyarwanda hufanya kila liwezekanalo ili** wajikinge dhidi ya ukimwi.

2. Kila yeyote anayehifadhi mazingira, **anatarajia kuishi maisha mazuri**.

3. **Elimu inakuza maendeleo ya nchi** yanayohitajika.

4. Atakaye kuishi kwa amani, **anaheshimu haki za wengine.**

5. Anayekubali kosa, **yeye husamehewa kwa amani.**

6. Watu wa kijiji chetu ili waishi mahali pasafi, **wao wanafanya kazi kwa bidii.**

7. unaposomewa hadithi, **tunajenga urafiki na ushirikiano.**

8. Mtunzi anapotunga hadithi fupi, a**napata fedha nyingi.**

9. **Alitajirika tena wakati** aliposhirikiana na mkewe.

10. Ukitaka kutajirika, **usiwe mzembe.**

### 8.4.5. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 8** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi kulingana na idadi yao. Kila kundi lipewe riwaya moja ya kusoma na kuifanyia uhakiki kwa kuzingatia vipengele vya fani na maudhui. Kila kundi liwasilishe kazi mbele ya darasa .Baada ya kuwasilisha maoni yao, wanafunzi waelekezwe kwenye maelezo ya ziada kwa ajili ya kuikosoa na kuikamilisha kazi yao.*

**Mapendekezo ya wasilisho la wanafunzi**

Kila kundi litawasilisha kazi kulingana na riwaya waliyoisoma

**Vipengele vitakavyochunguzwa katika Fani**

a) Wahusika: Aina na tabia

b) Mtindo

c) Muundo

d) Mandhari

e) Matumizi ya lugha

**Vipengele vitakavyochunguzwa katika maudhui**

a) Dhamira kuu

b) Dhamira ndogo ndogo

c) Falsafa

d) Ujumbe

e) Migogoro

### 8.4.6. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 9 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu aunde makundi kulingana na idadi yao. Kila kundi lifanye zoezi hili na kuwasilisha mbele ya darasa. Mwalimu awaongoze wanafunzi na kurekebisha.*

**Mwongozo wa majibu**

**1. Umuhimu wa riwaya:**

- Kukuza lugha
- Kuburudisha
- Kuelimisha
- Kukosoa tabia zisizoandamana na maadili ya jamii
- Kuonya, kuelekeza, kunasihi

**2. Tofauti kati ya hadithi fupi na riwaya**

| Hadithi fupi | Riwaya |
|---|---|
| Huwa fupi. Hadithi fupi nyingi huhitaji kuunganishwa pamoja na kuunda kitabu kimoja. | Huwa ndefu . Huunda kitabu kizima |
| Huwa na wahusika wachache | Huwa na wahusika wengi |
| Hurejelea wazo au kisa kimoja tu | Huwa na visa vingi na mawazo mengi yanayojenga wazo kuu |
| Husimuliwa kwa lugha ya moja kwa moja | Masimulizi yake yanaweza kuchanganya visengerenyuma na visengerembele. |
| Hufanyika katika mandhari/mazingira moja tu au chache. | Visa mbalimbali hufanyika katika mandhari mbalimbali |

### 8.4. 6. Utungaji

**Zoezi la 10 (*Angalia katika kitabu cha mwanafunzi*)**

*Hii ni kazi ya kibinafsi. Inaweza kufanyika darasani ama nyumbani. Kila mwanafunzi awasilishe kazi yake kisha mwalimu asahihishe makosa.*

## SOMO LA 9: UFAFANUZI WA TAMTHILIA

### 9.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi

Mada hii inajikita kwenye msamiati kuhusu tanzu ya tamthilia katika jamii. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza habari ili atambue kuwa wote wako katika hali nzuri. Wanafunzi nao wajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu awaulize ikiwa wana ujuzi kuhusu tamthilia.

**Mwalimu anaweza kutumia maswali yafuatayo:**

1. Uliwahi kutazama ama kusikia mchezo wowote wa kuigiza? Kama upo ulikuwa mchezo gani?
2. Wahusika walikuwa kina nani?
3. Eleza mambo mawili yaliyozungumziwa katika mchezo huo
4. Kuna maadili yoyote uliyoyapata kutokana na mchezo huo?
5. Husisha mchezo huo na maana ya neno "tamthilia".

### 9.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Vifaa vitakavyomsaidia mwalimu ni kama hivi:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- Kitabu cha mwanafunzi
- Magazeti na majalida mbalimbali
- Ubao, chaki
- Michoro kuhusu jukwaa.

Inamlazimu mwalimu kuandaa vifaa tofauti vitakavyomsaidia kufanikisha somo lake vizuri bila kusahau wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Ubunifu wa mwalimu katika maandalio ya zana za ufundishaji na ujifunzaji ni muhimu sana.

### 9.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

- **Utumiaji wa wanafunzi katika makundi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu na wanne. Ni vizuri mwalimu kutozidi wanafunzi watano katika kundi moja ili kila mwanafunzi ashiriki katika kazi bila ya kupiga ubwana. Mwalimu anaendelea kuwachunguza kwa makini ili afuate jinsi kazi inavyofanyika katika makundi hayo. Si hayo tu, mwalimu anawasaidia kutumia muda ifaavyo na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yaundwe kwa kuwachanganya wasichana na wavulana. Baada ya kazi katika makundi mwalimu awape kazi binafsi ili ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ameisha elewa somo vizuri tena na kuhakikisha kuwa lengo la somo limetimizwa. Kila mwanafunzi ajibu maswali yake pekee.

- **Mihadhara**: Mwalimu atumie njia ya kuwapa fursa ya kutoa hoja kuhusu benki. Wanafunzi wajitokeze mbele ya wenzao watoe maelezo yao kuhusu mada husika. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzao. Mwalimu aongoze kazi hiyo na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanatega sikio na kuulizwa maswali. Mwalimu ajibu maswali magumu kwa wanafunzi.
- **Maelezo ya mwalimu**: Kulingana na tajiriba ya mwalimu ajue kiwango cha ujuzi wa wanafunzi wake. Mwalimu akigundua tatizo alitatue kikamilifu.

## 9.4. Majibu

**Zoezi la 1: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajibu maswali waliyopewa katika zoezi la1. Mwalimu aelekeze majadiliano ya wanafunzi ili waweze kupata majibu yenye kuwaandaa katika ujifunzaji wa somo kuhusu ufafanuzi wa tamthilia. Baadhi ya majibu yanayoweza kutolewa na wanafunzi ni haya yafuatayo:*

1. Ndiyo. Ulikuwa mchezo wa 'Urunana'.

2. Wahusika walikuwa Bushombe, Kankwanzi, Petero na Lopez

3. Mambo mawili yaliyozungumziwa yalihusu elimu ya wasichana na mpango wa uzazi

4. Ndiyo. Maadili niyoweza kupata ni kama kuheshimu wazazi, kusaidia walio na ulemavu, na kuasidiana ili kujenga jamii, nk.

5.Mchezo huo "Ururnana" ni mchezo wa kuigiza na neno tamthilia hufafanuliwa kama mchezo wa kuigiza ambao unawahusisha wahusika kadhaa wenye kuiga tabia za watu wanaopatikana katika jamii.

### 9.4.1 Zoezi la Ufahamu

**Zoezi la 2: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wanafunzi washirikiane kwa kutoa majibu yao.

2. Onyesho hili linafanyika nyumbani kwa Zainabu.Uhusiano kati ya Aisha na Zainabu ni kwamba Zainabu ni mama yake Aisha

3. Zainabu ni mamamkwe wa Sele.

4. Aisha ni mke wa kisasa, hajali sana mambo ya zama zilizopita. Anaingia ndani na kuwapita Bibi na mama yake bila kuwasalimia. Vile vile hana muda wa kujua bayana matatizo ya mumewe. Bibi yake anapomdadisi kuhusu matatizo ya mumewe, anaonekana kutojali sana kuwa karibu na bwana yake ili ajue fika matatizo yake.

5. Wanawake wa kisasa (siku hizi) hawajishughulishi sana na huduma za nyumbani kwa kuwa wana shughuli nyingine nyingi zisizo za kinyumbani.

6. Bi. Rahma ni mwanamke wa makamo, anajali mila na desturi za enzi zake, ana Imani ya kishirikina. Ana busara. Anawalaumu wanawake wa kisasa kwa kutokuwa na muda wa kujishughulisha na huduma za nyumbani kwao.

7.Wanawake wa zama za kale:

- walijali mila na desturi za jamii.
- walikuwa na muda wa kushughulikia huduma za nyumbani.
- Walikuwa wakiomba ushauri kwa wazazi wao.
- walidai kukandamizwa.
- Wanawake wa zama hizi.
- hawajali mila na desturi za jamii.
- hawana muda wa kushughulikia huduma za nyumbani.
- wanaweka siri mambo yanayowahusu.
- wana usawa wa kijinsia.

8. Bi. Rahma anaona ugonjwa wa Sele kuwa ni ugonjwa usio wa kawaida, unaohitaji waganga wa

Kienyeji wanaojua kupunga upepo na kutoa kafara.

9. Zainabu ni mama yake Aisha.

10. Maadili yaliyomo katika onyesho hili:

- kuheshimu wazazi na watu wengine.
- Kushirikiana kwa mume na mke katika masuala ya kifamilia.
- kuheshimu na kudumisha mila na desturi nzuri za jamii.
- kuachana na mila mbaya kama ushirikina.

### 9.4.2 Msamiati

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika zoezi hili kwa kuwambia wachunguze matumizi ya maneno katika sura ya tatmthilia waliyoisoma ; kisha wahusishe maneno hayo katika sehemu A kwa maelezo waliyopewa katika sehemu B.*

1. Wasiwasi D. dukuduku la moyo

2. Kujuzu E. kushurutisha kufanya jambo

3. Biryani J. chakula kinachotengenezwa kwa wali uliokangwa na kuchanganya na nyama ambayo imekaangwa na masala

4. Pweza F. mnyama wa baharini mwenye mikia minane

5. Maradufu — A. mara mbili ya idadi, ukubwa,ujazo

6. Kugusa — C. kushika kidogo

7. Halahala — G. upesi upesi, haraka haraka

8. Rundo — B. mkusanyiko wa vitu vingi vilivyowekwa pamoja

9. Kunga — H. mambo ambayo hayatakiwi yajulikane

10. Kutapatapa — I. kukosa makini, kuwa na wasiwasi

**Zoezi la 4 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)*:** *Mwalimu aombe wanafunzi kutafuta maana za maneno waliyopewa na kuyatumia maneno hayo katika sentensi. Ikihitajika mwalimu akumbushe wanafunzi kutumia kamusi yao.*

1. Kuandaa: Kufanya kitu au jambo kuwa tayari kutumika.

Mf: Wanawake wa siku hizi hawana muda wa kuandaa chakula.

2. Kufukuzana: kukimbizana mbio kwa kufuata nyuma.

Mf: Sele alionekana kama mtu anayefukuzana na kivuli chake.

3. Ushauri: Maoni anayopewa mtu ili yamsaidie kufika mapatano Fulani na wengie.

Mf: wazazi hutoa ushauri kwa watoto wao.

4. Kafara: sadaka itolewayo kwa mizimu.

Mf: Bi. Rahma alikuwa tayari kutoa kafara ili kumponyesha Sele.

5. Kubishana: kushindana na mtu juu ya jambo linalozungumzwa.

Mf: Watoto hubishan na watoto wao wasipoelewana juu ya matendo yao.

6. Kupuuza: kutotia maanani, kudharau.

Mf: Si vizuri kupuuza ushauri wa wazazi.

7. Ustaarabu:mwenendo unaofungamana na maendeleo ya kimaadili yaliyokubalika katika jamii

Mf: Wenyeji wetu wanahitaji kuwa na ustaarabu wa hali ya juu

8. Kuvunja heshima: kudharau mtu.

Mf: Wazee hudai kuvunjiwa heshima na watoto wao

9.Kitoweo: mboga, mchuzi, nyama, maharagwe, ambayo huliwa pamoja na chakula kingine kama ugali muhogo au ndizi.

Mf: Tumeandaa kitoweo kitamu kwa ajili ya wageni.

10. Kudharau: kuacha kujali, kupuuza.

**Zoezi la 5 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)*:** *Mwalimu aombe wanafunzi kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi kwa kutumia maneno waliyopewa. Ni vyema kuwakumbusha kwamba wanaweza kuchunguza pia matumizi ya maneno hayo katika kifungu cha tamthilia walichosoma.*

1. Hamu ya chakula
2. Mienendo
3. Mapishi
4. Usuli
5. wamepungua

### 9.4.3. Sarufi: Matumizi ya Vishazi

**Zoezi la 5:*(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha awaelekeze katika majadiliano yao kuhusu sentensi walizopewa. Ni vyema mwalimu awape mwongozo ili wanafunzi waweze kulinganisha sentensi kimaana kwa kurahisisha utambuzi wao wa vishazi huru na vishazi tegemezi.*

**Majibu:**

1.

*a. Imani za kishirikina hupingana na matibabu ya kisasa*

*b. alipopewa mawaidha na wazazi waze*

*c. Atakayejiingiza katika matendo yanayopingana na mila na desturizetu*

*d.Atakayejiingiza katika matendo yanayopingana na mila na desturizetu*

2.

Sehemu ya sentensi ya (a) na ile ya sentensi (d) zinaleta maana kamili baada ya kuondolewa katika sentensi kuu

Sehemu ya sentensi ya (b) na ile ya sentensi (c) hazileti maana kamili baada ya kuondolewa katika sentensi kuu

**Zoezi la 7 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)*:** Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili waweze kushirikiana na kutafakari pamoja kuhusu swali walilopewa. Mwalimu atathmini sentensi zilizotolewa na wanafunzi kwa kuwapa maelekezo yanayostahili ili wafanikishe kazi yao.

**Zoezi la 8 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)*:** *Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kuwaomba wabainishe vishazi huru na vishazi tegemezi vilivyotumiwa katika sentensi, kisha awaelekeze kutoa sifa muhimu zinazotofautisha vishazi hivyo.*

1. Bi. Rahma aliwaonya watu kuhusu mila na desturi na watu wote walimsikia.

Kishazi huru kishazi huru

2. Mtu ambaye hayaheshimu mawaidha ya wazazi atapata cha mtema kuni.

Kishazi tegemezi kishazi tegemezi

3. Kabla ya kuingia ndani Bi. Rahma alibisha hodi.

Kishazi tegemezi kishazi huru

4. Anayezungumza na wazee hujua mambo mengi.

Kishazi tegemezi kishazi huru

5. Walioonyesha mwenendo mwema walifanikiwa kujenga familia imara.

Kishazi tegemezi kishazi huru

### 9.1.4. Matumizi ya Lugha: Fani na Maudhui katika Tamthilia

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya watatu watatu, wakumbuke mchezo mmoja uliochezwa na "Itorero Indamutsa" kutoka Redio Rwanda au "Urunana", mwalimu awaelekeze wajadiliane kuhusu maswali waliyopewa.*

1. Tamthilia ni mchezo wa kuigiza ulioandikwa ili uigizwe jukwaani au usomwe kwa kuwasilisha ujumbe.

2. Dhamira zinazoendelezwa sana katika tamthilia ni:

- mapenzi
- kihistoria
- kisiasa
- kiuchumi
- kidini
- kulinda mazingira
- ushujaa
- usawa wa kijinsia
- malezi
- elimu
- kitabia
- kiutamaduni, n.k

3. Wahusika wa tamthilia ni watu na wanaojitambulisha kwa matendo yao.

Wahusika wa hadithi simulizi ni mchanganyiko yaani watu na wanyama na vitu vingine

Vinavyopewa uhai.

4. Zifuatazo ni sifa za tamthilia au mchezo wa jukwaani:

Tamthilia inaigizwa jukwaani

Tamthilia ina wahusika mbali mbali

Tamthilia inajengwa na fani na maudhui

Watazamaji hushirikishwa .

- Matumizi ya mapambo ili kuashiria kubadilika kwa mazingira au wakati.
- Huhusisha aina nyingine za sanaa kama ushairi au nyimbo.
- Matumizi ya lugha, mtindo na muundo, migogoro, n.k

**Zoezi la 10(*Angalia katika kitabu cha mwanafunzi*):***Wanafunzi katika makundi ya watatu watatu, kwa kuelekezwa na mwalimu, wasome maelezo waliyopewa kuhusu tamthilia kwa kulinganisha na maoni yao au kuyakamilisha.*

### 9.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 10: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwanafunzi asikilize tamthilia kwenye Redio na kuizungumzia mbele ya darasa,mwalimu amuelekeze katika mazungumzo hayo.*

Zoezi la 11: Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi ya wawili wawili, washirikiane na wajadiliane kwa kutetea mada mbili teule kati ya :

a) Michezo ya kuigiza ni sanaa ambayo humfaidisha msanii.

b) Matumizi ya madawa ya kulevya ni pingamizi kubwa kwa maendeleo ya nchi

c) Michezo ya kuigiza ni mojawapo ya shule za kuelimisha maadili na mwenendo mwema

d) Michezo ya kuigiza hukuza akili.

### 9.4.6. Kuandika

Mwanafunzi kwa kuelekezwa na mwalimu, atunge sentensi sita zenye vishazi huru na vishazi tegemezi.

Mifano:

1. Mtu anayefanya uasherati anapatwa na magonjwa mbalimbali.
2. Waliofuata mawaidha ya walezi walifanikiwa maishani.
3. Anayeharibu mazingira atapewa adhabu.
4. Mtu anayetumia madawa ya kulevya anapotoka akili.
5. Wanaovaa nguo safi wanaonekana vizuri
6. Atapewa zawadi aliyeshinda katika uandishi wa vitabu.

**Zoezi la 12: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwanafunzi atege sikio kipindi cha Redio Rwanda kitokeacho Jumanne na Jumamosi jioni kuhusu mchezo wa kuigizwa utayarishwao na Itorero Indamutsa kisha aandike muhtasari wake na kuuasilisha mbele ya darasa. Mwalimu amuelekeze katika mawasiliano darasani.*

## 9.5. Muhtasari wa Mada

Mada hii ya kwanza”**Tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili”** ina masomo manne yanayohusiana na mada husika. **Somo la sita** linaelezea kuhusu riwaya na umuhimu wake kwa kujenja utamaduni katika jamii husika pamoja na kujiendeleza kiuchumi. **Somo la saba** linashughulikia umuhimu wa **ushairi** kwa kuimarisha utamaduni na mwenendo mwema katika jamii kama vile kutoa malezi bora kwa watoto. **Somo la nane** linatuelezea kuhusu hadithi fupi na nafasi yake kwa kufundisha jamii kwa njia ya kukuza utamaduni.

## 9.6. Maelezo ya Ziada

**Hadithi Fupi**

Hadithi fupi ni hadithi za kubuni kutoka katika mazingira ambayo huhusishwa na matukio au mambo mbalimbali katika maisha ya watu. Hadithi hizi hukusudiwa kusomwa kuliko kuandikwa.

Hadithi fupi huwa fupi kwa kila kipengele, hadithi fupi huweza kusomwa katika kikao kimoja.

**Fani katika Hadithi Fupi**

Huu ni ufundi wa kisanaa atumiao msanii katika kutoa ujumbe wake kwa wasomaji wa hadithi yake. Fani ni sura ya nje ya hadithi fupi. Fani huwa na vipengele tofauti:

Vipengele vya fani:

- Wahusika
- Muundo
- Mtindo
- Mandhari
- Muda

**Wahusika**

Wahusika ni watu, wanyama, vitu au viumbe wengine wanaopatikana katika hadithi fupi:

**Aina za wahusika**

iii. Wahusika wakuu: Mhusika mkuu ni mhuska moja au wawili ambao hujitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi fupi.

iv. Wahusika wadogo: Ni aina ya wahusika muhimu sana ambao humsaidia mhusika mkuu kuipa hadithi mwelekeo wa kisanaa na kimaudhui.

**Tabia za wahusika**

i. **Wahusika bapa:** Ni aina ya wahusika ambao hawabadiliki kitabia kutoka mwanzoni mpaka mwishoni mwa hadithi fupi.

ii. **Wahusika duara:** Ni wahusika ambao wanabadilika kitabia kutokana na mabadiliko ya mazingira.

iii. **Wahusika foili:** Ni wahusika wenye tabia zinazobadilika kinusu. Wako kati ya wahusika bapa na wahusika duara.

**Muundo:**

Muundo ni namna msanii anavyopanga visa vyake au fikra zake katika hadithi fupi.

Muundo ni mtiririko wa matukio.

**Mtindo**

Mtindo ni namna ambavyo mwandishi huipa hadithi yake sura ya kifani na kimaudhui.

Mtindo ndio unaotofautisha wasanii. Katika mtindo tunachunguza sana matumizi ya lugha.

**Mandhari**

Mandhari ni mazingira na mahali tukio la hadithi fupi lilipotokea. Kuna mandhari ya kubuni na mandhari ya kweli.

**Muda**

Muda ni kipindi cha wakati kinachochukuliwa na hadithi nzima.

**Maudhui katika kazi ya fasihi**

Maudhui ni jumla la mawazo yote yanayozungumziwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu ya mawazo hayo. Maudhui hujumuisha mawazo pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma mwandishi kuandika kazi ya fasihi. Maudhui huwa na vipengele vifuatavyo:

- Dhamira
- Migogoro
- Falsafa
- Ujumbe
- Msimamo wa msanii

**Dhamira**

Dhamira ni wazo kuu linalojitokeza katika hadithi fupi. Dhamira hugawanyika katika makundi mawili. Kuna dhamira kuu na dhamira ndogo.

i. Dhamira kuu: Wazo kuu lililomo hatika hadithi fupi.

ii. Dhamira ndogo:Wazo dogo lililomo katika kazi ya fasihi.

**Falsafa**

Kimsingi, falsafa ni elimu ya asili, busara au hekima.katika hadithi fupi falsafa ya msanii hugusiwa kutokana na jinsi anavyoeleza matatizo ya jamii na jinsianavyotoa suluhisho kwa namna ya busara, amani na utulivu.

**Migogoro**

Migogoro ni hali ya kutokubaliana katika hadithi fupi.

**Ujumbe**

Ujumbe ni mafunzo mbalimbali yanayopatikana katika hadithi fupi. Katika kazi ya fasihi, ujumbe wa msingi hubebwa na dhamira kuu, na dhamira ndogo hubeba ujumbe unaosaidia ujumbe wa msingi.

**Msimamo wa msanii**

Mawazo, dhamira, mafunzo na falsafa huonyesha msimamo wa mwandishi kuhusu masuala mbalimbali. Msimamo wa msanii huonekana wakati anapoamua kufuata na kushikilia jambo Fulani. Jambo hilo linaweza kukataliwa na wengine lakini akalishikilia tu.

**Sifa za hadithi fupi**

- Huwa fupi.
- Huwa na wahusika wachache.
- Hurejelea wazo au kisa kimoja tu.
- Huandikwa kwa lugha ya moja kwa moja.
- Huwa na muundo rahisi kueleweka.
- Hufanyika katika mandhari au mazingira moja tu au chache.
- Huwa na sifa ya kubuniwa.
- Huwa na mhusika mkuu mmoja anayejitokeza sana kuliko wengine katika hadithi.
- Huwa na wazo moja lililopewa uzito kuliko jingine lolote.

**Dhima ya hadithi fupi**

- Hadithi fupi huelimisha.
- Hadithi fupi huburudisha.
- Hadithi fupi huadhibu na hunasihi jamii. Kuna hadithi fupi ambazo hutungwa kwa madhumuni ya kuasa na kuadhibu juu ya mambo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii.
- Hadithi fupi hupiga vita kwa hali na mali mazingira yote ya ujinga, maradhi, njaa na umasikini.
- Kuna hadithi fupi ambazo husaidia katika kujenga misingi ya demokrasia miongoni mwa umma wa wakulima, wafugaji na wafanyakazi wengine.
- Hadithi fupi huwakosoa watu katika vipengele mbalimbali vya maisha yao.

Ushairi ni eneo ambalo linahus kazi za kifasihi ambapo mtunzi hutumia maneno ya mkato na lugha yenye kuvutia na ambayo yamepangwa kwa urari wa mizani na vina maalum.

Kuna aina kuu tatu za ushairi: Mashairi, Ngonjera na Tenzi.

**Mashairi:**

Mtungowa kisanaa wenye mpangilo maalum na kutumia lugha ya mkato na mnato kwa kuelezea hisi na mawazo ya jamii husika na kuwasilisha ujumbe fulani. Mashairi hugawika katika makundi mawili: mashairi ya kimapokeo au mashairi arudhi na mashairi huru. Mashairi arudhi hutungwa kwa kufuata au kuzingatia sheria na kanuni au kaida za utunzi kama vile kuzingatia vina, idadi fulani ya mizani, mishororo na vipande vya mishororo. Kulingana na idadi ya mishororo katika kila ubeti, mashairi huweza kugawika tena katika aina mbalimbali:

1. Tathmina ni shairi lenye mshororo mmoja kila ubeti
2. Tathnia ni shairi lenye mishororo miwili kila ubeti
3. Tathlitha ni shairi lenye mishororo mitatu kila ubeti
4. Tarbia Ni shairi lenye mishoro minne kwa kila ubeti
5. Takhmisa ni shairi lenye mishororo mitano kwa kila ubeti
6. Tasdisa shairi lenye mishororo sita.

**Ngonjera:**

Ngonjera ni shairi lenye malumbano na majibizano kati ya watu wawili au zaidi.

**Tenzi**

Tenzi ni aina ya shairi ambayo ni mtungo mrefu wa kishairi unaoelezea historia au kisa fulani na ambao hauna vina vya kati katika mistari yake bali kila ubeti una vina vya namna moja katika mistari yake isipokuwa mstari wa mwisho wa ubeti.

Kuna mambo mengine muhimu kuhusu shairi. Mishororo ya shairi huwa na majina maalum.

Mwanzo huwa ni mshororo wa kwanza wa ubeti.

Mloto huwa ni mshororo wa pili wa ubeti.

Mlea huwa ni mshororo wa tatu wa ubeti

Kituo huwa ni mshororo wa mwisho wa ubeti

Kuna aina mbili za vituo ambazo ni kituo kimalizio ni kituo ambacho hakirudiwi mwishoni mwa kila ubeti katika shairi. Kituo kibwagizo ikiwa hurudiwarudiwa kwenye mwisho wa kila ubeti. Vipande au sehemu vya mishororo huitwa:

1. **ukwapi : Ni kipande cha kwanza cha mshororo.**
2. **Utao: Ni kipande cha pili cha mshororo.**
3. **Mwandamizi : Ni kipande cha tatu cha mshororo.**

**Maana ya riwaya**

Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni iliyoandikwa kwa maandishi ya nathari inayoeleza ukweli fulani wa maisha. Kazi hii ya riwaya, huhusisha watu binadamu,wanyama ama vitu vingine vinavyopewa uhai kama vile mizimu.

**Aina za Riwaya**

Kunazo aina kadhaa za Riwaya katika Fasihi Andishi:

**Riwaya sahili:** ni aina ya riwaya ambayo visa vyake husimuliwa moja kwa moja na huwa rahisi kueleweka.

**Riwaya changamano**: hii ni riwaya ambayo huhitaji kusomwa kwa makini ili kueleweka. Aghalabu huwa na maudhui mengi na wahusika wengi ambao wanachangia katika tatizo kuu katika riwaya hiyo. Hujengwa kwa taharuki ili kuwavutia hadhira kutazamia jinsi tatizo kuu litakavyotatuliwa. Hutumia mbinu za taharuki na visengere nyuma/mbele.

**Maana ya tamthilia**

- Tamthilia ni mchezo wa kuigiza ulioandikwa ili uigizwe jukwaani kwa kuwasilisha ujumbe kwa jamii.Kuna aina mbili za jukwaa:
- Jukwaa la akilini kama hali ya kujiundia akilini k.v. mchezo unaoigizwa redioni.
- Jukwaa la hadharani, yaani mahali ambapo maonyesho ya tamthilia yanaigiziwa mbele ya watazamaji au wasikilizaji.
- Tamthilia ni mojawapo ya kazi za sanaa ya fasihi andishi ambazo mtindo wake ni wa kimaandishi badala ya kimasimulizi.

- **Wahusika katika tamthilia**

Wahusika au watendaji wa tamthila huwa wanadamu ambao huiga kwenye jukwaa tabia na matendo ya watu wengine wapatikanao katika jamii. Hutofautiana na wahusika katika fasihi simulizi kwa sababu wale hushika vitabia wao wenyewe wakati ambapo wahusika wa fasihi simulizi hujitokeza kwa njia ya masimulizi.

- **Aina za wasika katika tamthilia**

Kama mojawapo ya tanzu za fasihi andishi, tamthilia huwa na wahusika wa aina sita kama ifuatavyo: Wahusika wakuu, wahusika wasaidizi, wahusika wadogo, wahusika bapa, wahusika duara pamoja na wahusika wafoili. Makundi haya ya wahusika yalielezwa wazi katika somo kuhusu hadithi fupi.

- **Aina za tamthilia**

Tamthilia au mchezo wa kuigiza huwa na aina mbalimbali kulingana na dhamira kuu inayoendelezwa. Utaipata tamthilia ya mapenzi, ya kihistoria, ya kisisa, ya kidini, ya kiuchumi, n.k. tamthilia hizi zote huangukia katika moja ya makundi makuu yafuatayo:

- **Tanzia**

Ni aina ya tamthilia iliyojaa, huzuni ndani yake, mikasa, matokeo ya vifo na mateso makali. Mwisho wa hadithi za aina hii huwa ni wa masikitiko, maanguko na hasara kubwa kwa mhusika mkuu au jamii inayoibushwa. Wengine huita aina hii tamthilia simanzi au trejedia.

- **Ramsa**

Tamthilia zenye kuchekesha kutokana na utani, mzaha, kejeli, maneno yaonyeshayo ujinga, n.k. Iwapo hadithi hizi huwa na dhana ya uchekeshaji, lengo lake ni kukosoa jamii, watawala na tabia mbaya na watu binafsi. Aina hii huitwa tena Tamthilia cheshi au komedia.

- **Tanzia – ramsa**

Tanzia – ramsa au simanzi – cheshi ni mchezo wenye sifa za ramsa, lakini ndani ya uchekeshaji wake na tanzia kama vile kifo cha mhusika mkuu au kuanguka kwa jamii. Pengine huitwa Trejikomedia.

- **Sifa za michezo ya kuigiza**

- Unapotaka kuikabili michezo ya kuigiza inabidi uzingatie fani na maudhui yake kama yalivyoelezwa katika hadithi fupi pamoja na riwaya.
- Maudhui ni yaliyomo katika tamthilia. Mwandishi wa tamthilia ana jambo analotaka kulionyesha jamii. Maadili na maonyo huweza kupatikana kutoka katika tamthilia. Maudhui inajengwa na dhamira kuu na dhamira ndogo. Na fani inajengwa na:
- Muundo: tamthilia hujengeka kwa muundo maalum. Huwa na mwanzo unaotujulisha kwa ufupi wa yale ambayo tunatazamia kukutana nayo hapo mbele. Mwanzo unasukumwa na mazungumzo yanayobeba migogoro ili kitendo kifike kwenye kilele na hatimaye mwisho wa mchezo.
- Lugha : Mazungumzo katika tamthilia ni ya moja kwa moja.
- Migogoro: Ni hali ya kutokubaliana kimawazo na kimatendo kati ya wahusika.
- Mtindo: Tamthilia inaweza kuchukua mtindo wa ishara, yaani huweza kuzungumzia kitu ambacho kinawakilisha kitu kingine. Huweza pia kuwa katika hali ya uhalisia. Huweza pia kutumia nyimbo kwa kusisitiza ujumbe.
- Kwa kutegemea mambo hayo mawili, sifa za mchezo wa kuigiza hujitoshereza kama ifuatavyo:
- Wahusika wake huwakilishwa na watendaji ambao hujieleza au hutenda wenyewe.
- Watazamaji au wasikilizaji hushirikishwa.
- Mchezo hutokea kwenye jukwaa mbele ya hadhira.

- Mapambo hutumiwa ili kuashiria kubadilika kwa mazingira au wakati.
- Hutumia mbinu za lugha kama vile chuku, tanakali za sauti, tamathali na nyinginezo.
- Huhusisha aina nyingine za sanaa kama vile ushairi na nyimbo.
- **Umuhimu wa michezo ya kuigiza**
- Kama tanzu zote za fasihi, lengo kuu la tamthilia ni kutoa maadili, maonyo au kurekebisha tabia mbaya za jamii. Licha ya hayo, tamthilia huwa na madhumuni ya kuburudisha, kuelimisha, kukuza uwezo wa kukariri kwa watendaji bila kusahau njia ya kufikia manufaa kiuchumi.

## 9.7. Tathmini ya Mada ya Pili`

Wanafunzi katika makundi ya watatu watatu, mwalimu awaelekeze wajibu maswali waliopewa.

1.

- Kuhifadhi utamaduni
- Kufundisha, kuonya na kukosoa jamii
- Kuinua uchumi n.k

2. Mwalimu atathmini shairi wanalotunga wanafunzi.

3.

- Kufundisha
- Kukosoa
- Kuadili na kuonya
- Kuboresha maisha kwa kujitafutia ajira n.k.

4. -

- Kufundisha jamii
- Kuburudisha
- Kukosoa na kuadili
- Kutoa maarifa
- Kuimarisha uchumi n.k.

## 9.8. Mazoezi ya Nyongeza

### 98.1. Mazoezi ya Urekebishaji

1. Tofautisha aina na tabia za wahusika wa hadithi fupi .

2. Eleza sifa za hadithi fupi.

3. Dhihirisha dhima ya hadithi fupi katika jamii.

5. Kwa kujiegemeza kwenye hadithi fupi uliyoisoma, eleza maana ya dhamira katika hadithi.

6. Tofautisha fani na maudhui.

### 9.8.2. Mazoezi Jumuishi

1.Toa maana ya riwaya

2 . Eleza umuhimu wa tamthilia katika jamii.

3. Eleza maana ya hadithi fupi.

4.Toa maana ya hadithi fupi.

5.Taja na fafanua vipengele muhimu vinavyozingatiwa wakati wa kutunga ushairi wa kimapokeo.

6.Kwa kutumia mifano mwafaka,eleza kinagaubaga tofauti na uhusiano uliopo kati ya riwaya na hadithi fupi.

### .9.8.3. Mazoezi ya Wanafunzi wenye Ujuzi wa Hali ya Juu

1. Eleza tofauti za mbinu za kifani katika hadithi za fasihi simulizi na hadithi za fasihi andishi(Swali hili linahusu kuyalinganisha mambo muhimu kama: Muundo,mtindo,

wahusika,lugha na mandhari).

2. Kwa kujiegemeza mifano mwafaka, eleza kwa marefu maana , sifa za na aina za riwaya.

# MADA KUU YA 3: UBUNAJI

3

## MADA NDOGO: HOTUBA NA UFUPISHO

### Uwezo Upatikanao katika Mada:

Mwanafunzi ataweza kuelewa mtindo wa hotuba na kuuzingatia katika mazoezi ya utungaji pamoja na ufupisho na kujua kuchambua kitenzi kwa njia ya uambishaji.

### Ujuzi wa Awali

Katika Mada zilizotangulia wanafunzi walisoma masomo yenye uhusiano na mada hii kama vile insha za masimulizi au za kubuni, midahalo na mijadala. Ujuzi waliotoa hapo utawasaidia katika:

- Kufanya ubunaji wa kazi za fasihi na zisizo za kifasihi kama vile hotuba
- Ukuzaji wa matumizi ya lugha kimzungumzo.
- Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali (kidato cha nne).

### Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada.

Katika masomo ya mada hii, kuna vifungu, michoro au picha, utumiaji wa msamiati katika sentensi, matumizi ya lugha na mzoezi au kazi na sarufi. Hivyo mwalimu awaongoze wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia masuala mtambuka yafuatayo:

Mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi

Usawa wa kijinsia

Mafunzo kuhusu amani na maadili

Elimu jumuishi

Mazingira na maendeleo endelevu

### Maelekezo kuhusu Kazi

- Mwalimu anatoa mwongozo wa kutoa jibu kwa kazi.
- Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, Wakati huo mwalimu awasaidie kufanikiwa kwa kupitia kazi zingine zilizotayarishwa au masomo ya mada yote.

## Orodha ya Masomo na Tathmini

| Masomo | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (Maarifa, ufahamu, stadi, maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 10 | Maana ya hotuba | **Maarifa na ufahamu:** Kuelewa maana ya hotuba<br><br>**Stadi:** Kutathmini hotuba kulingana na sifa zake.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Ushirikiano katika kazi za ujenzi wa taifa kama vile kazi za umuganda njia mojawapo ya maendeleo ya nchi. | 10 |
| 11 | Muundo wa hotuba | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja sehemu kuu za hotuba na kutaja sehemu kuu zake.<br><br>**Stadi:** Kuendeleza hotuba kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** kuishi kwa amani na maendeleo na umoja wa Wanyarwanda. | 10 |
| 12 | Ufupisho wa hotuba | Maarifa na ufahamu: Kufupisha hotuba kwa kuzingatia mawazo muhimu yanayounda hotuba.<br><br>Stadi: Kufupisha hotuba inayohusika na kulinganisha ufupisho uliotolewa kutoka makundi tofauti.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: Usafi wa mazingira, kuhifadhi taka ifaavyo, kujilinda na kujikinga maradhi yatokanayo na uchafu. | 10 |
| Tathmini ya mada | | | 2 |
| Vipindi vyote vya mada ya kwanza | | | 32 |

# SOMO LA 10: HOTUBA

## 10.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi

Mada hii inajikita kwenye utungaji wa hotuba. Mwalimu aanze somo  kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza habari ili atambue kuwa wote wako katika hali nzuri. Wanafunzi nao wanamwamkia mwalimu kisha mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu ujuzi wa hotuba.

**Mwalimu anaweza kutumia maswali yafuatayo:**

a. Je, mkitaka kufikisha ujumbe fulani kwa watu mnafanya nini?

b. Hotuba ni nini?

c. Elezeni umuhimu wa hotuba.

d. Je, miongoni mwenu kuna aliyewahi kusikiliza au kuandaa hotuba?

## 10.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Vifaa vitakavyomsaidia mwalimu ni kama hivi:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- Kitabu cha mwanafunzi
- Magazeti na majalida mbalimbali
- Ubao, chaki
- Michoro kuhusu hotuba, n.k.

Inamlazimu mwalimu kuandaa vifaa tofauti vitakavyomsaidai kufanikisha somo lake vizuri bila kusahau wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Ubunifu wa mwalimu katika maandalio ya zana za ufundishaji na ujifunzaji ni muhimu sana.

## 10.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia

- **Utumiaji wa wanafunzi katika makundi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu na wanne. Ni vizuri mwalimu kutozidi wanafunzi watano katika kundi moja ili kila mwanafunzi ashiriki kazi bila ya kutegea. Mwalimu aendelee kuwafuatilia wanafunzi kwa makini ili afuate jinsi kazi inavyofanyika katika makundi hayo. Si hayo tu, mwalimu awasaidie wanafunzi kutumia muda ipasavyo na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yaundwe kwa kuwachanganya wasichana na wavulana.  Baada ya kazi katika makundi, mwalimu awape wanafunzi kazi binafsi ili ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ameli elewa somo vizuri tena na kuhakikisha kuwa lengo la somo limefikiwa.  Kila mwanafunzi ajibu maswali yake peke yake.
- **Mihadhara:** Mwalimu atumie njia ya kuwapa fursa ya kutoa hoja kuhusu hotuba. Wanafunzi wajitokeze mbele ya wenzao watoe maelezo yao kuhusu mada husika. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzao. Mwalimu aongoze kazi hiyo na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanatega sikio na kuulizwa maswali. Mwalimu ajibu maswali magumu kwa wanafunzi.

- **Maelezo ya mwalimu**: Kulingana na tajiriba ya mwalimu ajue kiwango cha ujuzi wa wanafunzi wake. Mwalimu akigundua tatizo alitatue kikamilifu.

## 10.4. Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawiliwili, wanafunzi watazame mchoro kwenye ukurasa husika kisha watoe maoni yao kuhusu kifungu "Hotuba ya Meya kwa Wananchi kuhusu Kazi za umuganda".*

### 10.4.1 Zoezi la Ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi washirikiane kutoa majibu ya maswali waliyoulizwa.*

1. Ni ushirikiano katika kazi za umuganda kwa ujenzi wa taifa.

2. Ni meya, mkuu wa mkoa, mkuu wa kikosi cha askari jeshi, mkuu wa askari polisi, katibu mtendaji wa wilaya, na wananchi.

3. Ni mkuu wa mkoa.

4. Kutayarisha barabara, kupanda miti, kujenga masoko, hospitali, shule, n.k.

5. Kunamaanisha kuwa mwananchi anapenda nchi yake kwa kushiriki katika ujenzi wa nchi.

6. Nimepata fundisho la kuwa kazi za umuganda ni muhimu sana. Ni lazima kila raia ashiriki katika kazi zile za umuganda.

7. Inarahisisha kazi za ufanyaji biashara, itarahisisha utalii, inaunganisha eneo moja na jingine, inarahisisha upelekaji wa wagonjwa kutoka zahanati kwenda hospitali, inarahisisha utalii, inarahisisha matembezi, inaepusha ajali, n.k.

8. Wananchi wanahimizwa kushirikiana katika kazi za umuganda, kufanya kazi kwa nguvu, kulinda miundo mbinu iliyojengwa.

### 10.4.2 Msamiati kuhusu Kifungu cha Habari

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafuzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusisha maneno kutoka sehemu A na maana yake kutoka sehemu B*

**Majibu:**

1 = a, 2 = b, 3 = c, 4 = j, 5 = g, 6 = d, 7 = h, 8 = e, 9 = i, 10 =f.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika utungaji wa sentensi walizounda kwa kutumia msamiati waliopewa. Mwalimu achunguze kuwa wanafunzi wanatumia msamiati huo kwa njia ifaayo.*

**Kwa mfano:**

1. Kazi za umuganda zinatoa mchango mkubwa katika ujenzi wa taifa.
2. Askari jeshi hulinda usalama wa nchi.
3. Yeye ni askari polisi anayechunga usalama barabarani.
4. Ni tabia nzuri kukaribisha wageni kwa furaha.
5. Meya aliwashukuru walioshiriki katika kazi za umuganda.
6. Tutajenga taifa letu tukifanya kazi kwa nguvu.
7. Kazi inayofanyika kwa bidii huzaa matunda.

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kwa kushirikiana katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze kwa kujaza sentensi wakitumia maneno waliyopewa:*

1. mikoa
2. Katibu mtendaji
3. ilitengenezwa
4. Ujenzi wa taifa letu
5. Rahisi
6. Kupanda miti
7. Kukata nyasi
8. Mmonyoko wa ardhi
9. Asanteni
10. Kazi

### 10.4.4. Sarufi : Uambishaji wa Vitenzi:

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili wachunguze mifano ya sentensi walizopewa kwa kutambua viambishi awali na vya wakati vilivyomo. Mwalimu awaelekeze ikiwa kuna tatizo awasaidie.*

u-na-pend-a

u- : kiambishi awali nafsi ya pili / umoja

-na- : kiambishi cha wakati / wakati uliopo

Mnapenda : m-na-pend-a

m- : kiambishi awali nafsi ya pili / wingi

-na- : kiambishi cha wakati / wakati uliopo

Anapenda : a-na-pend-a

a- : kiambishi awali nafsi ya tatu / umoja

Wanapenda : wa-na-pend-a

Wa- : kiambishi awali nafsi ya tatu / wingi

-na- : kiambishi cha wakati / wakati uliopo

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze kunyambua na kuonyesha kiambishi awali na kikanushi*

1. a-na-fany-a

a- : kiambishi awali nafsi ya tatu / umoja

2. wa-ta-pand-a

Wa- : kiambishi awali nafsi ya tatu / wingi

3. hu-ju-i :

hu- : kikanushi / nafsi ya pili umoja

4. ha-kun-a :

ha- : kikanushi / nafsi ya tatu umoja

5.u-li-kat-a

u- : kiambishi awali nafsi ya pili / umoja

6. ni-na-pend-a

Ni- : kiambishi awali nafsi ya kwanza / umoja

7. si-wez-i

Si- : kikanushi / nafsi ya kwanza umoja

8. m-ta-fany-a

m- : kiambishi awali nafsi ya pili / wingi

9. tu-ta-jeng-a

Tu- : kiambishi awali nafsi ya kwanza / wingi

10. ha-ki-vunj-i

Ha- : kikanushi / nafsi ya tatu umoja

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kazi hii ni binafsi, mwalimu amuelekeze mwanafunzi kuonyesha nyakati zilizotumiwa katika sentensi alizopewa.*

1. Wakati uliopita

2. Wakati uliopo

3. Wakati wa mazoea

4. Wakati uliotimilika

5. Wakati wa mazoea

6. Wakati ujao

7. Wakati uliopo

8. Wakati uliopo

9. Wakati uliopita

10. Wakati uliotimilika

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaongoze kubadilisha sentensi katika nyakati walizopewa.*

1. Barabara hii ilitusaidia katika nyanja mbalimbali

2. Kitabu hiki kinaandikwa na walimu wa Kiswahili

3. Rwanda yetu imejengwa na sisi wenyewe

4. Wasichana na wavulana wote wanapaswa kwenda shuleni

5. Wanafunzi husomea darasani

6. Baba amelipa fedha za bima ya afya

10.4.5. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 9:*****(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawiliwawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswaali waliopewa kuhusu maelezo.*

1. Hotuba ni maelezo maalumu yanayotolewa na mtu mmoja mbele ya kundi la watu.

2. Hotuba hutolewa kwa lengo la kutaka kuhimiza kazi, kufanya kampeni fulani, kutoa taarifa fulani kwa watu.

3. Aina za hotuba ni:

- Hotuba za mahubiri: Ni hotuba za mafundisho ya kidini zitolewazo makanisani na misikitini.
- Hotuba za kisiasa: ni zile zihusuzo taarifa ya serikali kama kuwahimiza watu na kuwaalika kutenda jambo fulani.
- Mihadhara: Ni mafundisho ya mwalimu shuleni anapofundisha kundi la wanafunzi hasa hasa wa vyuo vikuu.

4. Sifa muhimu za hotuba:

- Ukweli wa taarifa

- Ufasaha wa lugha
- Mantiki nzuri
- Kujua vizuri aina ya watu wanaotolewa hotuba, kazi zao, umri, n.k.

### 10.4.6. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 10:** *(ukurasa wa 108)*

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujadili kuhusu mada walizopewa." Umuhimu wa Hotuba". Baada ya majadiliano, wanafunzi wawasilishe mbele ya wenzao.*

### 7. Kuandika: Utungaji

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwanafunzi atunge hotuba yenye aya tatu kuhusu " Kufunga mwaka wa shule".*

*Mwalimu atathmini namna wanafunzi wanavyoandika hotuba na kuwasaidia ikiwa wanakutana na tatizo.*

## SOMO LA 11: MUUNDO WA HOTUBA

### 11.1 Utangulizi/Marudio

Mwalimu aanze somo kwa kuamkiana na wanafunzi wake. Mwalimu ajue hali za wanafunzi na baadaye awaulize maswali machache kuhusu somo lililopita kuhusu maana ya hotuba. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kujibu maswali hayo na kuwachangamsha kidogo hivi akielekeza maswali yake kwenye somo jipya. Baadaye, mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, awape vitabu vya Kiswahili kisha awaombe kufanya kazi hii:

**Angalieni vizuri mchoro na kujibu maswali yanayofuata:**

- Watu unaowatazama kwenye mchoro huo wanafanya nini?
- Eleza shughuli ambazo watu hao wanafanya.
- Kuna uhusiano wowote kati ya mchoro huo na kichwa cha habari hapo chini?

### 11.2 Vifaa vya Kujifunzia

Mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji ambazo zitamsaidia ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo lake. Mwalimu atumie jumla au mojawapo ya vifaa hivi:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,

- Michoro au picha za watu ambao wanafanya mdahalo au mjadala.
- Kompyuta
- Projekta ya kuonyesha picha au video kutoka mtandao ikiwa ipo au mahali pengine.
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo kwa kutilia mkazo hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule na upatikanaji wa vifaa hivyo. Mwalimu kwa ubunifu wake, anaweza kuandaa vifaa mbalimbali vingine vya kumsaidia kufanikisha somo lake.

## 11.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake hivi akitilia mkazo mbinu ambazo zinafuata:

**a)Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wane na awape kazi ya kufanya. Ni vizuri kutozidi idadi ya watu watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini kazi inavyofanyika katika makundi kwa kuhakikisha matumizi mazuri ya muda na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana. Baada ya kazi, mwalimu aombe makundi kuwasilisha matokeo kwa darasa. Kazi katika makundi itiliwe mkazo kwa kuwasaidia wanafunzi kushirikiana na kujifunza kutoka kwa wenzao.

**b)Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake. (Asome kifungu cha habari mwenyewe au afanye zoezi mwenyewe).

**c)Maswali na majibu**: Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kuuliza maswali na kujibiwa. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzao iwezekanavyo. Mwalimu ajaribu kuweka maswali na majibu katika hali ya majadiliano kati yake na wanafunzi ama wanafunzi kati yao wanafunzi. Mwalimu ajibu maswali ambayo wanafunzi wote wanashindwa kujibu vilivyo. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali na wao wamjibu, na vile vile wanafunzi wamwulize mwalimu na wanafunzi wengine wajibu, mwisho wake mwalimu naye atoe majibu yake.

**d)Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi, kisha atambuwe ujuzi unaohitaji maelezo yake binafsi. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee vya kutosha wanafunzi wake somo kwa kusisitizia kasoro aliyoitambua. Ni vizuri kufanya hivi kwa kuwapa pia wanafunzi fursa ya majadiliano kuhusu maelezo yake.

## 11.4 Majibu ya Maswali

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Majibu katika kitabu cha Mwalimu*

*Wanafunzi wajibu maswali haya wakiongozwa na mwalimu pale ambapo itaonekana hawakuelewa namna ya kuyajibu*

### 11.4.1 Maswali ya Ufahamu

**Zoezi la 2(a)*:(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1.Mgeni wa heshima alikuwa Mkuu wa Kamisheni ya Umoja na Maridhiano.

2.Mkutano ambamo kulitolewa hotuba hii ulifanyikia kwenye Uwanja wa Amahoro.

3.Vyeo vya waheshimiwa waliokuwepo katika mkutano ni Mheshimiwa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na Waheshimiwa wengine wasiotajika kifunguni.

4.Katika kifungu cha habari, maneno "Mnyarwanda ni mtu mmoja" yanamaanisha kwamba kila mwananchi anajisikia Mnyarwanda kuliko mambo mengine na Wanyarwanda wote lazima wawe na mwelekeo mmoja kwa kulindaa amani, usalama na maendeleo.

5.Serikali ya Rwanda iliamua kujenga nchi kwenye msingi wa umoja na maridhiano kwani nchi ilikuwa na matatizo mengi yakiwemo vifo vya Wanyarwanda zaidi ya milioni moja katika mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi mnamo mwaka 1994.

6.Kulingana na historia ya Rwanda ubaguzi ni jambo baya sana kwa kuwa ubaguzi ulitesa nchi, ukawa kilele cha mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi watu na ukimbizi wa Wanyarwanda wengi katika nchi jirani.

7.Methali "Umoja ni nguvu" inahusiana kabisa na kifungu kwa sababu Serikali ya Rwanda ilijengea kwenye umoja na maridhiano na kufanikiwa. Hivi sasa Wananchi wana mwelekeo mmoja, wanafuatilia amani, usalama na maendeleo kama mtu mmoja. Mambo hayo yote yaliwezekana kutokana na umoja.

8.Utaratibu wa Ndi Umunyarwanda una malengo ya kuwapa Wanyarwanda fursa ya kufikiria unyarwanda yaani uhusiano wao, utamaduni wa kupenda nchi, kuilinda na kuiendeleza kwenye cheo cha juu iwezekanavyo.

9.Mambo muhimu matatu ya kimaendeleo ambayo hufanywa katika utaratibu wa Ndi Umunyarwanda ni kumpasa kila Mnyarwanda kuzingatia uhusiano wetu kama wananchi kwa kuendeleza umoja wetu, kupenda kuilinda na kuiendeleza nchi pamoja na kujiepusha na ubaguzi wowote ili tuwe na amani ya kutosha.

10.Kwa ufupi, utaratibu wa Ndi Umunyarwanda unahusu uimarishaji wa umoja wa Wanyarwanda ambao utatuwezesha kujiendeleza kwa muda wa kudumu, kila mwananchi anatarajiwa kujisikia Mnyarwanda kuliko mambo mengine na Mnyarwanda yeyote lazima awe na mwelekeo mmoja kwa kufuatilia amani, usalama na maendeleo.

### 11.4.2. Msamiati

**Zoezi la 2(b):** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1.Nitatunga hotuba nzuri siku ya kuanzisha rasmi Shirika la Umoja na Maridhiano shuleni kwetu.

2.Kwa minajili ya usalama wa Rwanda, tunapaswa kuishi kwa amani na kuilinda nchi yetu pamoja ili maisha yaendelee kuwa mazuri.

3.Wanajeshi, askari polisi, askari mgambo pamoja na watu wengine wanatarajiwa kuungana mkono kwa kulinda wananchi.

4.Ndi Umunyarwanda ni utaratibu wa kutilia nguvu umoja wa Wanyarwanda na kuimarisha maridhiano kati yao.

5.Wafanyamadhambi walikuwa wengi baada ya mwaka wa 1994 lakini mahakama za Gacaca zilifanya kazi nzuri kwa hali ya juu.

6.Watu zaidi ya miliyoni moja waliuawa katika mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi.

7.Kutokana na kwamba nchi yetu iliumia sana, ni lazima Rwanda ijengee msingi wake kwa siasa ya umoja na maridhiano.

Wahenga walisema jambo zuri na imara sana kwamba umoja ni nguvu.

8.Taratibu kadhaa za ngazi ya kitaifa huanzishwa mara nyingi na Mheshimiwa Rais.

10.Ni jambo muhimu sana kujua kwamba maendeleo yangu, yako na yake ndiyo maendeleo ya nchi yetu.

**Zoezi la 3:** *(ukurasa wa 112)*

*Husisha maneno katika sehemu A na maana yake katika sehemu B*

**Majibu:** 1j, 2a, 3g, 4b, 5c, 6d, 7e, 8f, 9h, 10i. (wanafunzi wanaweza pia kutumia mishale)

### 11.4.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi Awali Utendewa na Mzizi

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Onyesha viambishi tendewa (yambwa) katika vitenzi ambavyo vimepigiwa msitari:*

1.Tumeuona: tu-me-u-ona

2.Wanavipenda: wa-na-vi-penda

3.waliuona: wa-li-u-ona

4.Aliyamwaga: a-li-ya-mwaga

5.Nitalitembelea: ni-ta-li-tembelea

6.Walivitoa: wa-li-vi-toa

7.Tunaifurahia: tu-na-i-furahia

8.Inayamiliki: i-na-ya-miliki

9.Tunampenda: tu-na-m-penda

10.Nilikikalia: ni-li-ki-kalia

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Toa mizizi (kiini) ya vitenzi vilivyopigiwa msitari katika sentensi zinafuatazo:*

1.Nimekula: -l-

2.wanaweza: -wez-

3.walitembelea: -temb-

4.wanavaa: -va-

5.watakuja: -j-

6.inanyesha: -nyesh-

7.mnafurahi: -furahi-

8.wanataka: -tak-

9.Tunasonga: -song-

10.yalivaa: -va-

11.yanatembea: -temb-

### 11.4.4 Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali hapo chini*

1.Hotuba inatarajiwa kuwa na anwani ama kichwa chake, utangulizi, kiini au mwili na mwisho.

2.Katika kuanza hotuba yake, mhutubi hutoa mwanga ama picha ya habari inayokusudiwa kuzungumzwa. Anawatambua waliohudhuria mkutano kwa majina au vyeo vyao kuanzia kwa yule wa cheo cha juu hadi wa chini na kuwasalimia.

3.Habari yenyewe hutolewa katika sehemu ya mwili ama kiini cha hotuba kwa kuwa ndicho kinazingatia ujumbe wote au mawazo yote ambayo yanatarajiwa kutolewa katika hotuba.

4.Mwisho wa hotuba una maumbile ya kujumlisha mawazo yote yaliyozungumziwa kwa maelezo fasaha na ni vizuri ifungwe kwa picha inayofanana na ile ya utangulizi ili kumbukumbu ya habari ibaki katika mawazo ya wasikilizaji.

5.Hotuba nzuri huzingatia sifa zinazofuata: Ukweli wa habari na taarifa, ufasaha wa lugha, mantiki nzuri, nidhamu, sauti ya kusikia wazi na ishara zinazoeleweka.

### 11.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Kwa kushirikiana na wenzako, jadili mambo yafuatayo:**

1.Hoja zinazoweza kutolewa kwenye mada "Hotuba inaweza kuharibu na kujenga taifa" ni kama hizi:

- Hotuba mbaya inaweza kuleta ubaguzi kati ya wananchi, inaweza kusababisha vifo vya watu na hata mauaji ya kimbari, inaweza kusababisha uzembe na mwisho wake ikaleta umaskini. Hotuba mbaya yaweza kuleta ugomvi kati ya nchi moja na nchi nyingine na vilevile kukawa vita yenye kuleta kwa wakati wake vifo vya watu, ukimbizi, njaa na maradhi tofauti.
- Kwa upande mwingine, hotuba nzuri huleta umoja wa wananchi na hata ikiwa wananchi hao walikuwa na utengamano fulani. Hotuba nzuri huimarisha taifa kwani huwa msingi wa maendeleo kwa kushawishi wananchi kufanya kazi kwa bidii. Ni moja ya misingi ya kuishi kwa amani na usalama ndani ya nchi na kati ya nchi na nchi nyingine.

2.Hoja zinazoweza kutolewa kwenye mada "Mnyarwanda ni mtu mmoja" ni kama hizi:

- Kila mnyarwanda anapaswa kuimarisha umoja wa Wanyarwanda.
- Kila mnyarwanda anatarajiwa kujisikia Mnyarwanda kuliko kujisikia mambo mengine.
- Ni lazima kwa Wanyarwanda wote kuwa na mwelekeo mmoja kwa kufuatilia amani, usalama na maendeleo.
- Wanyarwanda wanapaswa kufikiria uhusiano wao yaani unyarwanda (utamaduni wa kupenda nchi yao, kuilinda nchi na kuiendeleza kwenye cheo cha juu iwezekanavyo) badala ya kufikiria mambo mengine ya kuwatatanisha.
- Wanyarwanda wote wanalazimika kuishi kama ndugu na kusaidiana inapohitajika ili waweze kujiendeleza kwa muda wa kudumu.

### 11.4.6. Kuandika

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Soma hotuba iliyopo hapo juu na kuifupisha katika aya moja yenye mistari sita.*

Mheshimiwa Mkuu wa Kamisheni ya Umoja na Maridhiano alitoa hotuba hii kwenye uwanja wa Amahoro akianzisha rasmi Utaratibu wa Ndi Umunyarwanda. Waheshimiwa Spika wa Bunge, Waziri wa Elimu, Mkuu wa Mkoa na wengine pamoja na mabibi na mabwana walikuwepo. Mhutubi alizungumzia hotuba za ubaguzi kama nguvu za ubaguzi ulioleta ukimbizi na vifo vya Wanyarwanda wengi na hata mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi. Basi, Serikali ya Rwanda ilijengea nchi kwa umoja na maridhiano. Utaratibu wa Ndi Umunyarwanda aliouanzisha rasmi unahusu uimarishaji wa umoja wa Wanyarwanda, uhusiano na maendeleo yao kama mtu mmoja, pamoja na kuepuka ubaguzi kwa kujenga amani na usalama wa kudumu.

## SOMO LA 12: UFUPISHO WA HOTUBA

### 12.1. Ujuzi wa Awali/ UtanguliziA

Mada hii inajikita kwenye msamiati kuhusu ubunaji. Katika masomo yaliyotangulia somo hili wanafunzi walisoma masomo yanayohusiana na somo hili kama vile maana ya hotuba na muundo wa hotuba. Masomo haya yatamwezesha mwanafunzi kuelewa sawa somo la ufupisho. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwajulia habari ili atambue kuwa wote wako katika hali nzuri. Wanafunzi nao wamwamkie mwalimu kisha mwalimu awaulize ikiwa wana ujuzi kuhusu ufupisho wa hotuba.

**Mwalimu anaweza kutumia maswali yafuatayo:**

a. Je, umewahi kuhudhuria hotuba yoyote?

b. Umegunduwa nini kuhusu mpangilio wa mawazo ya hotuba hiyo?

c. Je,ufupisho wa hotuba hufanyika vipi ?

d. Eleza kwa ufupi umuhimu wa kujua kufupisha hotuba.

### 12.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji

Vifaa vitakavyomsaidia mwalimu ni kama hivi:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- Kitabu cha mwanafunzi
- Magazeti na majalida mbalimbali
- Ubao, chaki
- Michoro unaoonyesha watu wanaokaa katika ukumbi wa mazungumzo.

Inamlazimu mwalimu kuandaa vifaa tofauti vitakavyomsaidia kufanikisha somo lake vizuri bila kusahau wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Ubunifu wa mwalimu katika maandalio ya zana za ufundishaji na ujifunzaji ni muhimu sana ili aweze kulenga shabaha yake.

### 12.3. Mbinu za Kujifundishia na Kujifunzia

- **Utumiaji wa makundi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu na wanne. Ni vizuri mwalimu kutozidi wanafunzi watano katika kundi moja ili kila mwanafunzi aweze kushiriki kazi. Mwalimu aendelee kuwafuatilia kwa makini ili afuate jinsi kazi inavyofanyika katika makundi hayo. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanatumia muda ifaavyo pamoja na kutoa msaada panapohitajika. Makundi haya yaundwe kwa kuwachanganya wasichana na wavulana kwa kuendeleza usawa wa kijinsia darasani

- **Kazi binafsi:** Baada ya kazi katika makundi mwalimu awape wanafunzi kazii ili ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ameisha elewa somo vizuri na ahakikishe kuwa lengo la somo lake limetimizika. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.
- **Mihadhara**: Mwalimu atumie njia ya kuwapa fursa ya kutoa hoja kuhusu ufupisho wa hotuba. Wanafunzi wajitokeze mbele ya wenzao watoe maelezo yao kuhusu mada husika. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzao. Mwalimu aongoze kazi hiyo na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanatega sikio na kuulizwa maswali. Mwalimu ajibu maswali magumu kwa wanafunzi.
- **Maelezo ya mwalimu**: Kulingana na tajiriba ya mwalimu ajue kiwango cha ujuzi wa wanafunzi wake na namna ya kuwasaidia wakati wowote msaada unahitajika. Mwalimu akigundua tatizo alitatue kikamilifu.

### 12. 4 Majibu

**Zoezi tangulizi la somo:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawiliwili, Mwalimu awaelekeze wajibu maswali yatayowaingiza katika somo jipya. lihusulo ufupisho wa hotuba. Ikiwa wanahitaji msaada mwalimu awasaidi*

Majibu pendekezo:

1. Ni kwa kupima kiwango cha ujuzi wa mwanafunzi kuhusu habari aliyosoma.

2. Ufupisho unalazimu anayetarajia kuufanya kusoma na kuelewa sana habari ambayo anafupisha ili asiongeze ama asipunguze maana ya habari ya awali. Kwa hiyo ufupisho unamsaidia mwanafunzi kwa kuelewa.

3. Hatua za kufanya ufupisho:

(i) Lazima kukisoma na kukielewa kifungu kilichotolewa

(ii). Chagua taarifa na maneno maalum

(iii). Unganisha mawazo makuu na habari ya awali na yaeleweke kwa kudondoa.

(iv). Muhtasari kama inavyotakiwa katika lugha inayoeleweka.

(v). Linganisha usawa wa ufupisho na habari ya awali. Mara nyingi huwa 1/3 wa habari ya awali.

#### 12.4.1 Ufahamu

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili mwalimu awaelekeze wanafunzi wafanye zoezi la ufahamu , Ikiwa wanafunzi wanauhitaji msaada mwalimu awasaidie.**

**Majibu yaliyopendekezwa:**

1. Ni kutoa ujumbe fulani kwa hadhira.

3. Kuzingatia usafi wa mazingira mahali pote.

4. Usafi wa mazingira ni uondoshaji wa uchafu katika mazingira ya binadamu. Huambatana na utunzaji wa mazingira pia. Usafi wa mazingira humuepusha binadamu na maambukizi ya magonjwa mbalimbali.

5. Ni njia ya kujilinda na kujikinga magonjwa kama vile ya matumbo na kuharisha

6. Wanaweza kusababisha magonjwa mbalimbali ya kuambukiza kama minyoo, kipindupindu, kuharisha na magonjwa mengine ya tumbo

7. Moshi wa taka hupanda angani na kusababisha mabadiliko ya hali ya hewa.

8. Ukosefu wa mvua na kuenea kwa jangwa na ukame.

9. Methali hizi zina maana zifuatazo:

(i) Maji yakimwagika hayazoleki: Ni kusema kuwa jambo likiharibika huwa limeharibika hata kama likitengenezwa hubaki na kasoro. Kwa hiyo kinga ni bora kuliko tiba.

(ii) Usipoziba ufa utajenga ukuta: Humaanisha kuwa ukiacha kutatua tatizo mwonzoni, na jambo hilo likaendelea kukuwa na kuwa hatari, utashindwa kulirekebisha hata ukilirekebisha utapoteza muda nguvu nyingi.

(iii) Kinga ni bora kuliko tiba: Ni vizuri kujikinga na kujilinda kuliko kupambana na madhara fulani.

10. Uhusiano uliopo kati ya methali Kinga ni bora kuliko tiba ni kuwa makala yale yanawahimiza watu kujilinda na kujikinga madhara kabla yake kujitokeza.

### 12.4.2 Msamiati

**Majibu penedekezo:**

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuunganisha maneno na maana yake kwa kutumia mishale.*

**Majibu:**

1.i
2.j
3.h
4.c
5.d
6.f
7.e

8.g

9.b

10.a

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kila mwanafunzi atunge sentensi zenye maana, mwalimu amwelekeze na kumtolea msaada ikiwa unahitajika.*

**Zifuatazo ni sentensi zilizopendekezwa :**

1.Bidii huzaa matunda.

2.Viongozi wa shule yetu wanatufundisha kujitegemea.

3.Kila raia anatolewa mwito wa kupiga vita magonjwa yasababishwayo na uchafu.

4.Uchafu ni chanzo kikuu cha magonjwa ya kuharisha.

5.Nyasi zilizochipuka kando na makazi lazima zikatwe.

6.Si vizuri kutupa mabaki ya chakula nje ya jalala.

7.Jalala ni shimo linalochimbiwa kwa kuweka nyasi.

8.Maganda ya matunda yasiyotupwa huonekana kama uchafu.

9.Mama aliosha vyombo vya mekoni

10Kulinda mazingira ni kujilinda sisi wenywe.

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kujaza sentensi na kuwatolea msaada ikiwa unahitajika.*

**Majibu yaliyopendekezwa :**

1.Usafi wa mazingira

2.Tiba

3.Choo

4.Iliyosafishwa,

5.Wanashirikiana,

6.Popote

7. Jalalani

8. Busitani

### 12.4.3. Sarufi

**Majibu pendekezo yaliyop[endekezwa:**

( i.) U-na-fany-ik-a:U-: Kiambishi awali

-ki-: Kiambishi cha kati wakati

-fany-: Mzizi wa kitenzi

-ik-: Kiambishi tamati kauli tendea

(.ii).A-li-tup-i-a: A-: Kiambishi awali

-li-: Kiambishi cha kati wakati

-tup-: Mzizi wa kitenzi

-i-: Kiambishi tamati kauli tendea.

-a kiishio.

-a: kiishio

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze wanafunzi ikiwa wanahitaji msaada awasaidie.*

**Majibu yaliyopendekezwa:**

1. Pig-: Mzizi wa kitenzi

-a: kiambishi tamati- kimalizio

2. Hifadh-:Mzizi wa kitenzi

-iw-: Kiambishi tamati ,kauli ya kutendewa

-a: kiishio/kimalizio

3.: **Kimb**-: :mzizi wa kitenzi

-il-: kiambishi tamati,kauli ya kutendea

-a : Kiishio/kimalizio

**4. Shiriki**-: Mzizi wa kitenzi

-an-: kiambishi tamati ,kauli ya kutendeana

-a : kimalizio/kiishio

**5. Chemsh-:** Mzizi wa kitenzi

-iw-: kiambishi tamati, kauli ya kutendewa

-a: kimalizio/kiishio

**6. Mwag**-: Mzizi wa kitenzi

-ik-: kiambishi tamati, kauli ya kutendeka.

-a: kimalizio/kiishio

7. **Kat**-: Mzizi wa kitenzi

-w-: kiambishi tamati

-a: kimalizio/kiishio

8 .**Timiz**-: Mzizi wa kitenzi

-ik-: kiambishi tamati ,kauli ya kutendeka.

-a: kimalizio/kiishio

9. **Chom-:** Mzizi wa kitenzi

-w-: kiambishi tamati, kauli ya kutendwa.

-a: kimalizio/kiishio

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze, wafanye zoezi ikiwa wanahitaji msaada awashughulikie*

**Majibu yaliyopendekezwa:**

1. Washirikiane
2. Huhifadhiwa
3. Kutupia
4. kukatwa
5. Vianaondolewa
6. Kuharibu
7. Wanaochoma
8. Unasababisha

### 12.4.4 Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 7** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze wanafunzi na ikiwa wanahitaji msaada awasaidie.*

1.Kinahusu usafi wa mazingira.

Kufanya usafi mahali popote na kupiga vita uchafu, kujilinda 2.kusababisha hali ya hewa inayoweza kuleta madhara kama ukame,

3.Kifungu hiki Kinga ni bora kuliko tiba, hapa ni ufupisho wa kifungu kinacholingana na theluthi 1/3 ya habari ya awali. Lakini kingali kinazingazitia ujumbe wa awali bila kupunguza wala kupotosha.

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze, wafanye zoezi ikiwa wanahitaji msaada awasaidie.*

**1. Hatua za kufanya ufupisho:**

(i). Lazima kukisoma na kukielewa kifungu kilichotolewa

(ii). Chagua taarifa na maneno maalum

(iii). Unganisha mawazo makuu na habari ya awali na yaeleweke kwa kudondoa.

(iv). Muhtasari kama inavyotakiwa katika lugha inayoeleweka.

(v) Linganisha usawa wa ufupisho na habari ya awali. Mara nyingi huwa 1/3 wa habari ya awali.

**2. Mambo muhimu yanayozingatiwa wakati wa kufupisha habari :**

(a). Kusoma habari husika zaidi ya mara moja.

.(b) Chagua mawazo makuu yanayojitokeza katika habari kisha uyaandike

(c) Andika ufupisho wako kwa kuzingatia kwa makini mawazo makuu

(d).Zingatia urefu kulingana na maelezo uliyopewa.

3. Anayetarajia kufupisha habari huisoma zaidi ya mara moja ili aweze kuielewa na kufanya ufupisho bila ya kuongeza wala kupotosha ujumbe wa habari ya awali.

**Zoezi la 9 : *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze, wafanye zoezi ikiwa wanahitaji msaada awasaidie.*

1.bidii

2 Fanya juu chini.

3.Tupige vita

4.Mbinu zozote

5 Kupiga mswaki.

6.Kuwa na imani

**Zoezi la 10: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwanafunzi awaelekeze wafanye zoezi walilopewa.*

1.Uchafu ≠ Usafi

2.Shindwa ≠ Shinda

3.Lala ≠amka

4.Huzunika ≠Furahi

5.Mwaga ≠Zoa

6.Acha ≠endelea

7Afya mbaya ≠ afya njema

8.Kipipa kichafu. ≠ kipipa safi

**Majibu**

**1.b**

**2.c**

**3.a**

**4.e**

**5.d**

**6.g**

**7.h**

**8.f**

### 12.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wajadili kwa kuhusisha methali walizopewa na mazingira ya afya kama vile "Kinga ni bora kuliko tiba" Ni kumaanisha kuwa inazalimu watu kujikinga badala ya kupata tiba wakati mtu alipokumbwa na magonjwa.*

### 12.4.6 Kuandika: Kufupisha Kifungu cha Habari

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwanafunzi binafsi, mwalimu amwelekeze afupishe kifungu cha habari alichokisoma kwa kufuatilia maelezo ya ufupisho bora, ikiwa anahitaji msaada mwalimu amsaidie.*

**Muhtasari wa Mada**

Mada ya tatu "**UBUNAJI**" ina masomo matatu yanayohusiana na mada husika.**Somo la kwanza** linawahimiza watu kushirikiana katika kazi kama zile za umuganda kwa kujijengea taifa kwa kutumia nguvu zetu kupitia kwa hotuba. **Somo la pili** linatia mkazo kwa umoja wa Wanyarwanda na kuishi kwa amani kama njia ya maendeleo ya raia .**Somo la tatu** linawahimiza watu kuwa na usafi wa mazingira, kuhifadhi taka, kujilinda na kujikinga maradhi zitokanazo na uchafu.

**Maelezo ya ziada**

Hotuba ni maelezo maalumu yanayotolewa na mtu mmoja mbele ya kundi la watu. Hotuba inaweza kutolewa kwa madhumuni ya kutaka kuhimiza kazi, kufanya kampeni fulani, kutoa taarifa fulani kwa watu. Aina za hotuba ni:

a) Mahubiri: Ni hotuba za mafundisho ya kidini, zinazotolewa makanisani, misikitini, n.k.

b) Hotuba za kisiasa: Ni hotuba zihusuzo taarifa ya serikali kama vile kuwahimiza watu na kuwaalika kutenda jambo fulani, n.k.

c) Mihadhara: Ni hotuba au mafundisho ya mwalimu shuleni anapofundisha kundi la wanafunzi na hasa wanafunzi wa vyuo vikuu.

**Sifa za hotuba:**

- Ukweli wa habari na taarifa

- Kujua vizuri aina ya watu unaotolea hotuba, umri wao, kazi zao, n.k.
- Ufasaha wa lugha ili iweze kupendeza na kueleweka vizuri
- Nidhamu au adabu njema ya mzungumzaji mwenyewe asimamapo mbele ya watu
- Mantiki nzuri au mfuatano mzuri wa mawazo
- Sauti ya kusikika vizuri
- Kuvaa vizuri.

**Hotuba ina sehemu zifuatazo:**

1. Anwani: Anwani, mada au kichwa cha hotuba huchukua mada ya hotuba. Hiki ndicho kichwa chake hotuba.

Mfano: Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Rwanda kuanzisha nye sikukuu ya mashujaa.

2. Utangulizi: Mazungumzo katika utangulizi yanatoa mwanga ama picha ya habari inayokusudiwa kuzungumzwa. Anza hotuba yako kwa kuwatambua waliohudhuria mkutano). Wataje kwa majina au vyeo vyao kuanza yule wa cheo cha juu hadi wa chini, mabibi na mabwana. Kumbuka kwamba huhitaji kuwasalimia. Kuwatambua kwa majina ya pekee kunatosha.

Mfano: Waziri wa Elimu, Gavana wa Jimbo la Kusini, Mkuu wa Wilaya ya Nyanza, Wanachama wa kikundi hiki cha Elimu Bora, mabibi na mabwana. Ni matumaini yangu kwamba nyote mna afya nzuri.

3. Mwili/Kiini: Hakikisha kuwa kuna mtiririko wa hoja kuanzia mwanzo hadi mwisho. Ujumbe wako wote unapaswa kuwa katika usemi halisi wala si wa taarifa. Panga mawazo kufuatana na uzito ama umuhimu wake. Wazo muhimu lazima lianze kuzungumziwa kwa ukamilifu halafu lifuatiwe na mawazo mengine, nayo kwa kikamilifu.

4. Mwisho: Hapa mazungumzo yajumlishe mawazo yote yaliyozungumziwa kwa maelezo fasaha. Ni vizuri kwa hotuba kufungwa kwa picha inayofanana na ile ya utangulizi ili kumbukumbu ya habari ibaki katika mawazo ya wasikilizaji.

**Maana ya ufupisho**

Ufupisho ni ustadi ama ufundi wa kuielewa habari na kuweza kuielezatena habari hiyo kwa maneno machache kuliko yaliyotumiwa awali.Anayeyaeleza hapunguzi hata kidogo kulingana na maana yake ya asili.

Kufupisha habari yoyote inamlazimu kuisoma sana na kuweza kuisimulia kwa mambo machache bila ya kupotosha ama kuongeza kuhusu maana yake ya awali. Kazi hii hupima kiwango cha ufahamu wa mtu katika kazi za utungaji.

Kufupisha habari hulingana na maelezo ya yule aliyeanda kazi hiyo.

Kuna wanaoomba kufupisha habari kulinga na idadi fulani ya mambo,aya fulani, idadi ya sentensi fulani lakini kwa jumla ufupisho mzuri unakuwa theluthi(1/3)ya habari ya awali.

☞**Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kufupisha haba**

Kusoma habari husika zaidi ya mara moja.

Chagua mawazo makuu yanayojitokeza katika habari kisha uyaandike

Andika ufupisho wako kwa kuzingatia kwa makini mawazo makuu

Zingatia urefu kulingana na maelezo uliyopewa.

☞**Hatua za kufanya ufupisho:**

1. Lazima kukisoma na kukielewa kifungu kilichotolewa
2. Chagua taarifa na maneno maalum
3. Unganisha mawazo makuu na habari ya awali na yaeleweke kwa kudondoa.
4. Muhtasari Kama inavyotakiwa katika lugha inayoeleweka.
5. Linganisha usawa wa ufupisho na habari ya awali. Mara nyingi huwa 1/3 wa habari ya awali.

**Tathmini ya Mada ya 3**

**1.Hatua zinazofuatiliwa kwa kufupisha habari:**

1. Lazima kukisoma na kukielewa kifungu kilichotolewa
2. Chagua taarifa na maneno maalum
3. Unganisha mawazo makuu na habari ya awali na yaeleweke kwa kudondoa.
4. Muhtasari kama inavyotakiwa katika lugha inayoeleweka.
5. Linganisha usawa wa ufupisho na habari ya awali . Mara nyingi huwa 1/3 wa habari ya awali.

**2.Kuna aina mbalimbali za hotuba baadhi yake ni hotuba ya**

a) Mahubiri: Ni hotuba za mafundisho ya kidini, zinazotolewa makanisani, misikitini, n.k.

b) Hotuba za kisiasa: Ni hotuba zihusuzo taarifa ya serikali kama vile kuwahimiza watu na kuwaalika kutenda jambo fulani, n.k.

c) Mihadhara: Ni hotuba au mafundisho ya mwalimu shuleni anapofundisha kundi la wanafunzi na hasa wanafunzi wa vyuo vikuu

**3 Viambishi vya vitenzi vilivyopigiwa msitari:**

a**) a-na-som-e-a: a-:** Kiambishi awali nafsi ya tatu,umoja

-**na**-: kiambishi kati wakati

-**som**-: mzizi

**-e**-: Kiambishi tamati kauli tendea

**-a**: Kiishio ama kima

**b) i-ta-timiz-ik-a:** i-: kiambishi awali nafsi ya tatu ,umoja

-ta-: Kiambishi kati wakati

-timiz-: mzizi

-ik-: kiambishi tamati kauli tendeka

-a: Kiishio ama kimalizio

**C. si-ta-ku-let-e-a: si**-: kikanushi nafsi ya kwanza,umoja

-ta-: Kiambishi kati wakati

-ku-: Kiambishi awali tendewa

-let-: mzizi

-e-: Kiambishi tamati kauli tendea

-a: Kiishio ama kimalizio

**- ku-ku-tayarish-i-a:. ku**-: kiambishi ngeli.

-ku-: Kiambishi awali tendewa

-tayarish-: mzizi

-i-: Kiambishi tamati kauli tendea

-a: Kiishio ama kimalizio

d**. ya-na-hifadh-iw-a: ya**-: kiambishi ngeli

-na-: Kiambishi kati wakati

-hifadh-: mzizi

-iw-: Kiambishi tamati kauli tendewa

-a: Kiishio ama kimalizio

**e.tu-na-m-pend-a: tu**-: kiambishi awali nafsi ya tatu, umoja

-na-: Kiambishi kati wakati

-m-: Kiambishi awali tendewa

- pend-: mzizi

-a: Kiishio ama kimalizio

**f. A-li-ji-tafut-i-a:. A**-: Kiambishi awali nafsi ya tatu

-li-: Kiambishi kati wakati

-ji-: Kiambishi rejeshi

-tafut-: mzizi

-i-: Kiambishi tamati tendea

-a:. Kiishio ama kimalizio

4 Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili mwalimu awaelekeze ,walinganishe muundo wa hotuba na ule wa insha zingine, walinganishe kwa kuzingatia mawazo muhimu kama vile kuhusu hotuba iwe na sehemu muhimu nne ambazo ni ulinganisho kati ya muundo wa hotuba na ule wa hadithi: Kuhusu hotuba, Mwalimu awakumbushe kuzingatia mawazo makuu kama inavyofanyika katika hadithi, Wazingatie tena sehemu za hotuba kama:

1. Anwani: Anwani, mada au kichwa cha hotuba huchukua mada ya hotuba

2. Utangulizi: Mazungumzo katika utangulizi yanatoa mwangaa ama picha ya habari inayokusudiwa kuzungumzwa. Ni matumaini yangu kwamba nyote mna afya nzuri,

3 Mwili/Kiini: Hakikisha kuwa kuna mtiririko wa hoja kuanzia mwanzo hadi mwisho. Ujumbe wako wote unapaswa kuwa katika usemi halisi wala si wa taarifa. Panga mawazo kufuatana na uzito ama umuhimu wake. Wazo muhimu lazima lianze kuzungumziwa kwa ukamilifu halafu lifuatiwe na mawazo mengine, nayo kwa kikamilifu.

4. Mwisho: Hapa mazungumzo yajumlishe mawazo yote yaliyozungumziwa kwa maelezo fasaha. Ni vizuri kwa hotuba kufungwa kwa picha inayofanana na ile ya utangulizi ili kumbukumbu ya habari ibaki katika mawazo ya wasikilizaji

5.Kulingana na muundo wa hadithi nayo huweza kuwa na sehemu nne kama tulivyoelezea hapo juu mwanafunzi aonyeshe kuwa ukilinganisha muundo wa hotuba na hadithi utaweza kugundua tofauti kuhusu fani yaani wahusika, muundo ni tofauti,miundo hutofautiana .

6.Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wafanye zoezi la kuonyesha aina zote za viambishi vya vitenzi walivyosoma na wajiegemeze mifano inayoeleweka. Wanapohitaji msaada mwalimu awasaidie watimize vizuri kazi hiyo.

7. Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wafanye utafiti kwa kutambua na kugundua ikiwa kuna hatua zingine za kufanya ufupisho, Ikiwa wanahitaji msaada mwalimu awasaidie

8. Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze watunge hotuba kuhusu mada waliyopewa "Ushirikiano wa kijinsia katika malezi ya watoto", wanafunzi wafuatilie mawazo makuu na kuyaingiza katika muundo wa hotuba kulingana na maelezo waliyotolewa.

Kama vile waonyeshe mchango wa mzizi wa kiume na yule wa mzazi wa kike na ushirikiano wa michango hiyo miwili kwa kuwatafutia watoto chakula,kuwalipia bima ya matibabu,kuwapeleka shuleni na kuwalipia karo yaani kuwapa elimu inayofaa, kuwafundisha nidhamu,n.k.

Mwanafunzi binafsi, mwalimu amwelekeze asome na kuelewa vizuri kifungu alichopewa hapo juu, baadaye afupishe kifungu cha awali, atumie theluthi ya kifungu cha awali, asiongeze wala asipunguze ujumbe wa habari ya awali. Ikiwa wanafunzi wanahitaji msaada mwalimu awasaidie.

## 12.5. Mazoezi ya Nyongeza

### 12.5.1. Mazoezi ya Urekebishaji

1. Toa maana ya hotuba.
2. Hotuba inaundwa na sehemu gani? Eleza
3. Katika utungaji wa hotuba, ni sharti kichwa kisadifiane na maudhui. Jadili
4. Hadhira hutiliwa mkazo na hatibu au mtoaji hotuba katika uandaaji wa hotuba. Jadili

### 12.5.2 Mazoezi Jumuishi

1. Katika hotuba, hadhira ina nafasi gani?
2. Kwa nini tunafanya ufupisho?
3. Eleza waziwazi kazi za viambishi vilivyomo katika sentensi hapo chini:

a) Mkufunzi wa timu ile alichezesha wachezaji mashuhuri.

b) Nyumba hii ilijengeka vizuri

ch) Ni vizuri kupendana kwa watu wote.

d) Mama aliwapikia chakula watoto wake chakula chenye protini.

e) Majirani walimlimia nyanya shamba lake.

f) Ng’ombe hufugwa kwa wingi nchini Rwanda.

### 12.5..3. Mazoezi ya Wanafunzi Wenye Ujuzi wa Hali ya Juu

1. Tunga hotuba kuhusu mada ifuatayo: “Elimu kwa wote.”
2. Baada ya kutunga hotuba hiyo, fanya ufupisho wake kwa kufuatilia hatua za ufupishaji.

# MADA KUU YA 4: Ukuzaji Wa Matumizi Ya Lugha Kimazungumzo

4

## MADA NDOGO: MIDAHALO NA MIJADALA

Uwezo Upatikanao katika Mada: Kuongoza midahalo na mijadala na kushiriki katika kazi za majadiliano kwa kuzingatia mada zilizotolewa kujadiliwa na kuchambua maneno ya Kiswahili kwa njia ya uambishaji.

### Ujuzi wa Awali

Katika mada zilizotangulia wanafunzi walisoma masomo yenye uhusiano na mada hii kama vile, katika kidato cha nne walisoma kuhusu midahalo na mijadala, insha na utungaji wa barua katika kidato cha tano. Ujuzi huu utasaidia wanafunzi katika:

- Ukuzaji wa matumizi ya lugha kimzungumzo.
- Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali (kidato cha nne, cha sita na pengine)

### Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada

Mwalimu ataingiza masuala mtambuka katika masomo ya mada hii yafuatayo :

Usawa wa kijinsia

Mazingira na maendeleo endelevu

Mafunzo kuhusu amani na maadili

Mila na desturi ya uchunguzi wa viwango

Elimu jumuishi

Mafunzo kuhusu uzalishaji mali

### Maelekezo kuhusu Kazi

- Mwalimu anatoa mwongozo wanafunzi kufanya mijadala na midahalo.
- Wanafunzi watafanya mijadala na midahalo mara nyingi katika makundi.
- Katika kutotautisha na kuhusiaha mijadala na midahalo mwalimu anaweza kutumia kazi binafsi mara nyingi.

## Orodha ya Masomo na Tathmini

| Masomo | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza(Maarifa, ufahamu, stadi, maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 13 | Mdahalo | Maarifa na ufahamu: Kuwa na ujuzi wa kutunga midahalo, kufuata mwenendo ufaao wakati wa kutoa hotuba katika makundi na kutumia lugha fasaha.<br><br>Stadi: Kutofautisha pande zinazoshiriki katika midahalo na mijadala, kusuluhisha majadiliano na kutumia lugha fasaha.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: Ushirikiano, urafiki, heshima katika midahalo, n.k. | 11 |
| 14 | Mijadala | Maarifa na ufahamu:Kuwa na ujuzi wa kutunga mijadala, kufuata mwenendo unaofaa wakati wa kutoa hoja katika makundi, kutumia lugha fasaha katika majadiliano, n.k.<br><br>Stadi: Kutumia lugha fasaha, kutoa suluhisho katika mijadala na kutofautisha pande zinazoshiriki katika mijadala.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: Ushirikiano, kuwa na heshima katika majadiliano, urafiki, kuwa na tabia nzuri katika jamii. | 11 |
| 15 | Uhusiano tofauti kati ya mdahalo na mjadala | Maarifa na ufahamu: Kuwa na uwezo wa kutofautisha midahalo na mijadala na matumizi ya lugha fasaha.<br><br>Stadi:  Kutumia lugha sahihi na kutofautisha pande zinazoshiriki katika midahalo na mijadala.<br><br>Maadili na mwenendo mwema: Ushirikiano, urafiki, sera ya “Ndi Umunyarwanda” na kuwa na heshima.. | 10 |
| Tathmini ya mada | | | 2 |
| Vipindi vyote vya mada ya nne | | | 34 |

# SOMO LA 13: MDAHALO

## 13.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi

Mada hii inajikita kwenye ukuzaji wa lugha katika mazungumzo. Mwalimu aanze somo na kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza habari ili atambue kuwa wote wako katika hali nzuri. Wanafunzi nao wanamwamkia mwalimu kisha mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu ujuzi wa mdahalo.

**Mwalimu anaweza kutumia maswali yafuatayo:**

a. Je, mliwahi kusikiliza na kushiriki katika mdahalo?

b. Mdahalo una umuhimu gani?

c. Elezeni wahusika wa mdahalo.

## 13.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Vifaa vitakavyomsaidia mwalimu ni kama hivi:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- Kitabu cha mwanafunzi
- Magazeti na majarida mbalimbali
- Ubao, chaki
- Michoro kuhusu midahalo, n.k.

Inamlazimu mwalimu kuandaa vifaa tofauti vitakavyomsaidia kufanikisha somo lake vizuri bila kusahau wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Ubunifu wa mwalimu katika maandalio ya zana za ufundishaji na ujifunzaji ni muhimu sana.

## 13.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

- **Utumiaji wa wanafunzi katika makundi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu na wanne. Ni vizuri mwalimu kutozidi wanafunzi watano katika kundi moja ili kila mwanafunzi ashiriki kazi bila ya kupiga ubwana. Mwalimu aendelee kuwachunguza kwa makini ili afuate jinsi kazi inavyofanyika katika makundi hayo. Si hayo tu, mwalimu anawasaidia kutumia muda ifaavyo na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya aundwe kwa kuwachanganya wasichana na wavulana. Baada ya kazi katikaa makundi mwalimu awape kazi binafsi ili ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ameisha elewa somo vizuri tena na kuhakikisha kuwa lengo la somo limetimizwa. Kila mwanafunzi ajibu maswali yake pekee.
- **Mihadhara:** Mwalimu atumie njia ya kuwapa fursa ya kutoa hoja kuhusu midahalo. Wanafunzi wajitokeze mbele ya wenzao watoe maelezo yao kuhusu mada husika. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzao. Mwalimu aongoze kazi hiyo na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanatega sikio na kuulizwa maswali. **Mwalimu ajibu maswali magumu kwa wanafunzi.**

- **Maelezo ya mwalimu**: Kulingana na tajiriba ya mwalimu ajue kiwango cha ujuzi wa wanafunzi wake. Mwalimu akigundua tatizo alitatue kikamilifu.

## 13.4. Majibu

zoezi la 1: ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, watazame mchoro kwenye ukurasa husika kisha watoe maoni yao.*

### 13.4.1 Majibu kuhusu Ufahamu

Zoezi la 2: ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswali kuhusu ufahamu.*

1. Ni "Hali ya maisha ya vijana wa leo ni bora zaidi kuliko ile ya vijana wa karne zilizopita".

2. Upande wa utetezi na upande wa upinzani.

3. Mtetezi wa kwanza anasema kuwa vijana wa leo wanapata elimu wangali wadogo hadi vyuo vikuu na kujiendeleza wao binafsi na jamii kwa ujumla, wanasomea kando na makao yao na wanajifunza nidhamu na adabu.

4. Kuna mchezo wa mpira wa miguu yaani kandanda, mpira wa wavu, mpira wa kikapu, michezo ya riadha, mbio za miguu, mbio za magari, n.k..

5. Teknolojia inaweza kuwa chanzo cha mienendo mibaya na tabia mbaya kwani miongoni mwa vijana wa leo huitumia kwa kuangamiza maisha yao badala ya kuyaboresha.

6. Surua au shurua, polio, pepopunda na magonjwa ya kisukari.

7. Vijana wa kale walijiburudisha kwa kushiriki katika michezo kama miereka, majigambo, kutupa mikuki, kuruka, mchezo wa" intore", kuvutana, mbembea za kienyeji, n.k.

8. Michezo humfanya mtu kujilinda magonjwa yatokanayo na ukosefu wa mazoezi ya michezo.

9. Ndoa huvunjika kwa sababu ya kusalitiana na uchumba hufanyiwa kwenye simu na mitandao ya kijamii bila kutuata mila na desturi za jamii ambazo zillimshirikisha mshenga katika ndoa.

10. Vijana wa kale walikuwa wanavaa kulingana na wakati wao, mavazi yao yalitengenezwa katika ngozi za wanyama, nyuzi na magome ya miti. Lakini mavazi mengi ya vijana wa leo ni ya kupotosha na kudhahilisha wanayoyavaa kwani kuna wasichachana wanaovaa nguo zenye kitovu wazi, mgongo wazi, sketi fupi sana na zinazowabana matako na nyonga. Wavulana nao wanavaa suruali zilizochanika magotini na zinazoning'inia kwenye matako.

### 13.4.2 Msamiati

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafuzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuunganisha maneno ya safu A na maana yake katika safu ya B*

**Majibu:**

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| 1. Uzalendo | g) hali ya mtu kuipenda nchi yake na kuamini utamaduni wake, kuiokoa hata kuwa tayari kuifia. |
| 2. Unyago | h) ngoma ya kuwafundisha wali mila za kabila lao. |
| 3 .Mwenendo | d) Matendo ya mtu yanayojirudiarudia au tabia |
| 4. Shule za chekechea | b) shule za watoto wadogo wasiozidi miaka mitano |
| 5. Shahada | e) karatasi maalum anayopewa mtu baada ya kupata mafunzo fulani katika chuo ili kuthibitisha kwamba amemaliza au amefaulu mitihani yake |
| 6. Miridadi | b) enye kupendeza |
| 7. Nidhamu | f) adabu |
| 8. Faraka | i) utenganisho au uachaji |
| 9.Ushujaa | j) uhodari au ujasiri |
| 10. Burudani | c) Shughuli inayofanywa kwa ajili ya kufurahisha na kuchangamsha watu |

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika utungaji wa sentensi walizoziunda kwa kutumia msamiati waliopewa. Mwalimu achunguze kuwa wanafunzi wanatumia msamiati huo kwa njia ifaayo.*

**Kwa mfano:**

1. Wanafunzi watakaofaulu vizuri wataendelea na masomo ya chuo kikuu.
2. Michezo ya riadha hufanya miili yetu kuwa katika hali nzuri.
3. Mbio za miguu ni mchezo unaofurahisha sana.
4. Kila mtu anapaswa kuvaa maridadi.
5. Ni lazima watoto wote wachanjwe chanjo dhidi ya ugonjwa wa polio.
6. Udaktari ni kazi muhimu maishani mwetu.
7. Ukimfuata mwalimu darasani hutakuwa na mfadhaiko wowote.

8. Kufaulu mitihani inahitaji kusoma kwa bidii.
9. Mwenyekiti anasimamia zoezi la kupiga kura katika mdahalo.
10. Elimu haina mwisho.

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwanafunzi kwa kuelekezwa na namwalimu, ajaze sentensi kwa kutumia maneno aliyopewa*

1. Mvivi
2. Karne
3. Wasikilizaji
4. Surua
5. Upinzani
   Utetezi
6. Mwanamwali
7. Vitovu wazi
8. Utafiti

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili, mwalimu awaelekeze kwa kupanga maneno waliyopewa ili waunde sentensi sahihi.*

1. Watoto wanapaswa kusaidia wazazi wao
2. Ni vizuri kuwaonyesha vijana makosa yao na kuwaadhibu kwa upendo.
3. Mwana wa mwenzako ni wako.
4. Usikubali kushindwa hata siku moja.
5. Kila raia apande miti kwa kulinda mazingira.
6. Mapenzi si kuwanunulia vitu vya bei ghali.
7. Adabu ni dhahabu.

### 13.4.3. Sarufi: Uambishaji wa Maneno

Zoezi la 6: ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili wachunguze mifano ya majina waliyopewa kisha wayaweke katika wingi. Mwalimu awaelekeze ikiwa kuna swali awasaidie.*

1. Mwenyekiti – wenyeviti
2. Msemaji - wasemaji
3. Kiatu – viatu
4. Mchezo – michezo
5. Mgonjwa – wagonjwa

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika majina ya dhahania yanayotokana nay ale yaliyoandikwa kwa rangi iliyokoza.*

1. Udaktari
2. Uzalendo
3. Upendo
4. Ualimu

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwanafunzi kwa kuelekezwa na mwalimu, aandike sentensi alizopewa katika hali ya udogo*

1. Kigari chake ni kizuri
2. Kijiji chetu kina usafi
3. Kishamba chake ni kikubwa
4. Kisabuni kinatumiwa kufua kinguo
5. Kivulana hiki kinapenda kuchezea kimpira

**Zoezi la 9:** *(ukurasa wa 144)*

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze kwa kuandika sentensi walizopewa katika hali ya ukubwa.*

1. Jichwa lake linamuuma
2. Jiatu lake limepotea
3. Ni vizuri kutega jisikio jisemaji
4. Jiduka lake linaja jisahani
5. Jitanda hili lilitengenezwa jana
6. Jifagio litanunuliwa kesho

### 13.4. 4 Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 10:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kusoma maelezo waliyopewa na kujibu maswali waliopewa.*

1. Wajibu wa katibu ni kuandika hoja zilizotolewa na wazungumzaji, kusoma muhtasari wa hoja zilizotolewa na pande mbili na kutangaza matokeo ya kula zilizopigwa mwishoni mwa mdahalo.

2. Wahusika wa mdahalo ni:

- Mwenyekiti ambaye hufungua na kuendesha mdahalo, kuwapa wasemaji nafasi ya kuzungumza na kupigisha kula;

- Wazungumzaji wakuu wanaotetea mada (watetezi) na wazungumzaji wakuu wanaopinga mada(wapinzani)

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswali kuhusu mdahalo*

1. Wahusika wa mdahalo ni mwenyekiti, wazungumzaji wakuu kwa upande wa utetezi na wazungumzaji wakuu kwa upande wa upinzani na katibu.
2. Mdahalo ni majadiliano baina ya watu wengi juu ya jambo moja maalumu.
3. Ni upande wa upinzani na upande wa utetezi.

### 13.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 12:** *(ukurasa wa 145)*

*Wanafunzi katika makundi ya watatu watatu, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuchagua mada moja na kutunga mdahalo kisha wauasilishe mbele ya wenzao. Wanafunzi wanafuata kanuni za utungaji wa mdahalo:*

- Kuchagua mada
- Kutafuta mawazo makuu muhimu yatakayozungumziwa
- Kupanga mawazo hayo kimantiki
- Kuchagua mwenyekiti, wazungumzaji wakuu na katibu
- Kutunga mdahalo
- Kuuwasilisha mbele ya hadhara
- Kufanya muhtasari wa hoja zilizotolewa
- Kusoma hoja zilizotolewa na pande mbili
- Kupiga kura
- Kutangaza matokeo ya kura
- Kuwashukuru washiriki na kufunga mdahalo.

Kuhusu “ Umuhimu wa mdahalo kwa wanafunzi”, kuna mawazo pendekezo kama vile:

- Kuwawezesha wanafunzi kuchagua na kupanga mawazo vyema;
- Kuwa na uwezo wa kuzungumza hadharani;
- Kuwa na uwezo wa kuongoza mazungumzo;
- Kuwa na uwezo wa kutoa suluhisho kwa jambo fulani,n.k.

Kuhusu “ Ueneaji wa teknolojia katika njia ya maendeleo”, mapendekezo ya mawazo:

Teknolojia hutumiwa katika sekta mbali mbali kama vile: elimu, afya, kilimo na ufugaji, kazi za ofisini, ufanyaji biashara, utalii, n.k.

### 13.4.6 Kuandika: Utungaji

Katika makundi ya wanafunzi kulingana na wahusika wa mdahalo, mwalimu awaelekeze kutunga mdahalo kuhusu mada waliyopewa "NDOA YA KALE ILIKUWA BORA KULIKO NDOA YA LEO" na kwa kufuatilia kanuni za utungaji wa hotuba.

- Mapendekezo ya mawazo:
- Kuchagua mshenga
- Kuchagua mchumba
- Kuposa
- Sikukuu ya harusi n.k.

## SOMO LA 14: MJADALA

### 14.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi

Mada hii inajikita kwenye msamiati kuhusu utumiaji wa lugha kimazungumzo. Katika masomo yaliyotangulia somo hili, wanafunzi walisoma masomo yenye uhusiano wa karibu sana na somo hili kama vile maana ya hotuba na mdahalo. Ujuzi uliopatikana katika masomo haya utawawezesha wanafunzi kuelewa vizuri somo hili la mjadala. Mwalimu ataanza somo na kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza habari ili atambue kuwa wote wako katika hali nzuri. Wanafunzi nao wanamwamkia mwalimu kisha mwalimu awaulize ikiwa wana ujuzi wowote kuhusu mjadala.

**Mwalimu anaweza kutumia maswali yafuatayo:**

a. Je, umewahi kuushiriki mjadala wowote?
b. Nani ambaye huongoza mjadala?
c. Mjadala una muhimu gani kwa mwanafunzi?
d. Ni lugha gani inayohitajika kutumiwa katika mjadala.

### 14.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji

Vifaa vitakavyomsaidia mwalimu ni kama hivi:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- Kitabu cha mwanafunzi
- Magazeti na majarida mbalimbali
- Ubao, chaki.tarakilishi
- Michoro kuhusu watu wanaokaa katika ukumbi wa mazungumzo na mtu mbele yao..

Inamlazimu mwalimu kuandaa vifaa tofauti vitakavyomsaidia kufanikisha somo lake ifaavyo bila kusahau wanafunzi ambao wana ulemavu fulani. Ubunifu wa mwalimu katika maandalio ya zana za ufundishaji na ujifunzaji ni muhimu ili aweze kulenga shabaha.

## 14.3. Mbinu za Kujifundishia na Kujifunzia

- **Utumiaji wa wanafunzi katika makund**i: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu na wanne. Mwalimu asizidi wanafunzi watano katika kundi moja ili kila mwanafunzi ashiriki vizuri kazi bila ya kupiga ubwana. Mwalimu anaendelea kuwachunguza kwa makini ili afuate jinsi kazi inavyofanyika katika makundi hayo. Si hayo tu, mwalimu anawasaidia kutumia muda ifaavyo pamaoja na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yaundwe kwa kuwachanganya wasichana na wavulana ili washirikiane kimahojiano kwa hiyo mambo ya usawa wa kijinsia hutendeka. Baada ya kazi katika makundi mwalimu awape kazi binafsi ili ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ameisha elewa somo vizuri na kuhakikisha kuwa lengo la somo limetimizwa. Kila mwanafunzi ajibu maswali yake pekee.
- **Mihadhara**: Mwalimu atumie njia ya kuwapa fursa ya kutoa hoja kuhusu mjadala. Wanafunzi waandee mijadala wajitokeze mbele ya wenzao washirikiane kwa kutoa hoja ama kuongoza mijadala kuhusu mada husika. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzao. Mwalimu aongoze kazi hiyo na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanatega sikio na kuulizwa maswali. Mwalimu ajibu maswali magumu kwa wanafunzi.
- **Maelezo ya mwalimu**: Kulingana na tajiriba ya mwalimu ajue kiwango cha ujuzi wa wanafunzi wake na namna ya kuwasaidia wakati wowote msaada unahitajika. Mwalimu akigundua tatizo alitatue kikamilifu.

## 14.1. Mapendekezo ya Majibu ya Ufahamu

**Majibu ya ufahamu**

**Zoezi la 1: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Majibu katika kitabu cha mwalimu*

*Wanafunzi wajibu maswali haya wakiongozwa na mwalimu pale ambapo itaonekana hawakuelewa namna ya kuyajibu*

### 14.4.1 Kusoma na Ufahamu

**Zoezi la 2: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaelekeze wanafunzi wajibu maswali kuhusu ufahamu. Ikiwa wanahitaji msaada mwalimu awasaidie.*

1. Ni kiongozi wa mjadala na ambaye ndiye huruwahusu wanaotoa hoja zao
2. Tabia ya desturi ya kujitegemea inaanzia katika familia yenyewe
3. Viwanda vidogo haweza kupatikana mahali popote, pato lake huwa ni la kiasi kidogo na kutumia watumishi wachache wakati viwanda vikubwa hutumia idadi kubwa la watumishi, pato lake ni la kiwango kikubwa, hutumia mitambo mingi mikubwa na mzito kwa kutengeneza bidhaa zake. Mara nyingi hujengwa katika miji.

4. Katika mjadala kunatajwa malighafi kama ngozi za wanyama wa mifugo na nyuzi.

5. Kwa kurahisisha mikakati ya kujiendelea, Taifa la Rwanda lilianzisha na kuendesha program mbalimbali katika sekta tofauti kama vile kuboresha sekta ya kilimo na ufugaji, Elimu, viwanda, Afya.Teknolojia, Usawa wa kijinsia na zinginezo..

6.”Mtegemea cha nduguye hufa masikini” Ni kumaanisha kuwa ajingee uwezo na tabia ya kujitafutia suluhisho ya matatitizo yanayomkumba baadala ya kutegemea misaada kutoka nje.

7. Viwanda vya kuteneza nguo nchini vina manufaa mengi kwa raia wa nchi ya Rwanda kama vile raia huvaa nguo mpya baadala ya kuvaa mitumba,raia wameajiriwa katika viwanda vinavyotengeneza nguo hapa nchini na kupewa mishahara na kukidhi mahitaji ya familia zao.

8. Malighafi inayoweza kutumiwa kwa kutengeneza mikanda na mikoba ni ngozi za wanyama wa mifugo, nyuzi zinazotokana na mimiea.

9.” Usawa wa jinsia ni kitu muhimu katika maendeleo ya jamii.” Kuanzia katika familia inalazimu mwanamume na mwanamke kuwa na ushirikiano katika kila jambo lolote lenye kujenga na kukuza maendeleo ya familia. Umoja huo kuwasaidia kujenga tabia nzuri ya ya kuishi katika amani ,upendo na maendeleo na jamii nzima ikaendelea .

10. Ninapata maadili ya kujenga tabia ya kuwa na desturi ya kujitegemea pamaja na kutekeleza hayo.

### 14.4.2 Msamiati kuhusu Mjadala

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze, watunge sentensi kwa kutumia mamneno waliyopewa. Wakihitaji msaada mwalimu awasaidie.*

1 Kujitegemea ni tabia nzuri maishani.

2 Kila familia inalenga kuimarisha uchumi wake.

3 Anayefanya kazi zenye ufanisi huwa tajiri sana.

4 Teknolojia inarahisisha kazi

5 Kiongozi wa mjadala alimkaribisha mshiriki kutoa hoja.

6 Viwandani wanatumia malighafi kutengeneza bidhaa mbalimbali

7 Kazi zenye ufanisi huleta matokeo yanayotarajiwa.

8 Usawa wa jinsia ukifanyika vyema familia inajitegeme na kuendelea sana.

9 Kiwanda hiki kinatengeneza bidhaa zenye kiwango bora.

10 JohTunapasawa kusadia kupanga mradi ya kilimo na ufugaji.

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika majozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi, wajibu maswali waliyopewa,ikiwa wanahitaji msaada mwalimu awasaidie.*

1. b
2. c
3. d
4. a
5. h
6. f
7. e
8. g
9. j
10. i

### 14.4.3 Sarufi: Uambishaji wa maneno kuhusu vivumishi na Vitenzi

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ,wanafunzi watatu watatu,mwalimu awaelekeze,watunge sentensi kwa kutumia maneno mwaliyopewa na kujiegemeza kwenye mfano waliopewa.*

1 Usafi unahitajika nchini

2 Mto ule una urefu wa maili kumi na tano.

3 Ubora wa kazi ni pato.

4 Usawa wa kijinsia ni jambo muhimu katika maendeleo.

5 Amina amejiepusha na uhaba wa kazi kwa kujitafutia ajira.

6 Siku hizi shule za ufundi zinasaidia kujitegemea.

7 Nimejulikana pote sio kutokana na utajiri wangu mkubwa.

8 Ukubwa wa tembo unatisha sana.

9 Udogo wa kitu haulingani na umuhimu wake.

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika majozi,Mwalimu awaelekeze wanafunzi wasome maelezo kuhusu uambishaji wa vitenzi na wayajibu maswali husika kwa kuonyesha viambishi kwa njia ya namna ya kuapa maneno mapya.,na kufafanua maana ya uambishaji.. Msaada ukihitajika mwalimu awasaidie.*

***Majibu yaliyopendekezwa: mfano***

(i) Maelezo haya hapo juu yanahusu uambishaji wa vivumishi na vitenzi.

(ii) Wanafunzi, wajibu swali hili kwa kuonyesha namna ya kuambisha vivumishi na kupata maneno mapya. Ikiwa kuna tatizo linalojitokeza mwalimu awatolee msaada.

(iii) Uambishaji wa vitenzi Uambishaji ni utaratibu wa kuambatisha viambishi mbalimbali kwenye mzizi wa kitenzi.

**Zoezi la 7: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi, wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze, watunge sentensi kwa kutumia maneno waliyounda kutotokana na uambishaji wa vitenzi.*

***Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Ushirikiano wa kijinsia ni jambo muhimu katika maendeleo ya jamii
2. Uendelezaji wa tabia ya kujitegemea utafanya wengi kuwa tajiri.
3. Uenezaji wa teknolojia unarahisisha maendeleo.
4. Uimarishaji wa desturi za kujitegemea ni lazima kwa kila mtu.
5. Ukulima bora unahitaji ustadi na maadili kuhusu kilimo.
6. Ufugaji wa ng'ombe za kisasa unatajirisha wafugaji.
7. Ukuzaji wa tabia ya kujitegemea unaboresha maisha yetu.
8. Utengenezaji wa bidhaa katika viwanda hunufaisha wananchi.

### 14.4.4 Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 8: . *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi, wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze,watunge sentensi kwa kutumia maneno waliyounda kutotokana na uambishaji wa vitenzi.*

***Majibu yaliyopendekezwa:***

(i) Mdahalo huwa na pande mbili: upande wa utetezi wa mada na upande wa. Upinzani wa mada iliyotolewa. Mdahalo huwa na katibu wakati mjadala huwa na kiongozi akiongoza washiriki wanaotoa hoja zao tu hasa hoja huweza kupingana. Namna ya kukaa katika mdahalo ni tofauti na katika mjadala.

(ii) Eleza umuhimu wa mjadala kwa mwanafunzi.

- Hukuza uwezo wa kitaaluma, fikra na hali ya udadisi pamoja na kushawishi hadhara.
- Huwezesha mtu kujitambua binafsi kipaji chake cha kuchangia hoja na wengine.
- Hutufanya tuzoee kuheshimu hoja za wengine, kuwasikiliza na kuachiria nafasi ya kutoa maoni yao.
- Hutufanya kuheshemu na kutumia muda ifavyo katika mazungumzo.
- Husaidia mtu kukuza uwezo wa kupanga mawazo katika mazungumzo.
- Anayehudhuria hukuza uwezo wa kuyachagua mawazo, kuiunga mada na pia kupinga kauli fulani

3.Kiongozi wa mjadala huteua mada inayovutia washiriki, kuongoza mjadala kwa kuruhusu washiriki waliohudhuria..

4.Katika uandishi wowote, umilisisi wa lugha na mbinu zake ni jambo muhimukwani inamlazimu mwandishi kuielewa lugha sana anayoitumia pamoja na mbinu za lugha hiyo anayoitumia..

5. "Mjadala unasadikika ni kumaanisha kuwa mjadala uwe na ukweli ili wasomaji waweze kusadiki kuwa mjadala huo una ukweli.

**Zoezi la 9 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi, wanafunzi watatu watatu, mwalimu awaelekeze,watunge sentensi kwa kutumia maneno waliyounda kutokana na uambishaji wa vitenzi.*

***Majibu yaliyopendekezwa:***

1. Matendo
2. Vimeundwa
3. Desturi
4. Bure
5. Amejitajirisha
6. Usawa
7. Habari
8. Pesa
9. Kufanya
10. Ufanisiza

**Zoezi la 10: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwanafunzi binafsi, mwalimu amwelekeze achague mada kati ya zile mada alizopewa kisha aandee mjadala, . Afuate maelezo na kanuni za utungaji kwa kuzingatia mawazo makuu yanayopatikana katika uundaji wa mjadala. Ikiwa anahitaji msaada mwalimu amsaidie.*

### 14. 4.6. Utungaji:.

**Zoezi la 9: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwanafunzi binafsi, mwalimu amwelekeze achague mada kati ya zile alizopewa, atunge kifungu cha habari cha aya zisizopungua tano. Afuate maelezo na kanuni za utungaji kwa kuzingatia mawazo makuu. Ikiwa anahitaji msaada mwalimu amsaidie.*

## SOMO LA 15: UHUSIANO NA TOFAUTI KATI YA MIDAHALO NA MIJADALA

### 15.1 Utangulizi/Marudio

Baada ya mwalimu kuamkiana na wanafunzi na kujua hali yao, mwalimu awaulize maswali machache kuhusu somo lililopita kuhusu mjadala na somo lililolitangulia kuhusu mdahalo. Mwalimu wa furaha na uchangamfu.. Aidha, awaweke wanafunzi katika makundi ya wanne wanne na apokee majibu ya wasimamizi wa makundi katika hali iliyo sawa na ile ya mjadala. Maswali haya yamsaidie:

***Angalieni vizuri mchoro na kujibu maswali yanayofuata:***

- Kwenye mchoro wa kwanza kuna watu.Watu hao wanafanyaje?
- Mchoro gani unahusika na mdahalo? Kwa nini?
- Mchoro upi unahusika na mjadala? Kwa sababu gani?

### 15.2 Vifaa vya Kujifunzia

Mwalimu atafute zana za ufundishaji ambazo zitamsaidia ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo lake. Atumie jumla au mojawapo ya vifaa hivi:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Michoro au picha za watu ambao wanafanya mdahalo au mjadala.
- Kompyuta
- Projekta ya kuonyesha picha au video kutoka mtandao ikiwa yupo au mahali pengine.
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo kwa kutilia mkazo hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa mbalimbali vingine vya kumsaidia kufanikisha somo lake. Akumbuke kuwa vifaa hivi huandaliwa kulingana na mazingira ya shule na upatikanaji wake.

### 15.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Mwalimu atilie pia mkazo mbinu zifuatazo:

**Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**

Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya watu wawili, watatu, wanne. Ni vizuri kutozidi idadi ya watu watano katika kundi moja ili kuepuka uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelea kuangalia kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi. Ahakikishe wanafunzi wanatumia muda vizuri na atoe msaada pale unapohitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.

Baada ya kazi, mwalimu aombe makundi kuwasilisha matokeo mbele ya darasa. Kazi katika makundi itiliwe mkazo kwani husaidia wanafunzi kushirikiana na kujifunza kutoka kwa wenzao.

**Kazi binafsi kwa mwanafunzi**

Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake. (Asome kifungu cha habari mwenyewe au afanye zoezi mwenyewe).

**Maswali na majibu**

Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kuuliza maswali na kujibiwa. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzake iwezekanavyo. Mwalimu ajaribu kuweka maswali na majibu katika hali ya majadiliano kati yake na wanafunzi ama wanafunzi na wanafunzi. Mwalimu ajibu maswali ambayo wanafunzi wote wanashindwa kujibu vilivyo. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali na wao wamjibu, na vile vile wanafunzi wamwulize mwalimu na wanafunzi wengine wajibu, mwisho wake mwalimu naye atoe majibu yake.

**Maelezo ya mwalimu**

Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake, kisha atambuwe ujuzi unaohitaji maelezo yake binafsi. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee vya kutosha wanafunzi wake somo kwa kusisitizia kasoro aliyoitambua. Ni vizuri kufanya hivi kwa kuwapa pia wanafunzi fursa ya majadiliano kuhusu maelezo yake.

## 15.4 Majibu

**Zoezi la tangulizi**

*Majibu katika kitabu cha mwalimu*

*Wanafunzi wajibu maswali haya wakiongozwa na mwalimu pale ambapo itaonekana hawakuelewa namna ya kuyajibu*

### 15.4.1 Maswali ya Ufahamu

**Zoezi la 1 :** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

***Jibu maswali haya kutoka kifunguni***

1. Wahusika ambao wanashiriki katika mdahalo ni mwenyekiti, katibu, wapinzani, watetezi na hadhira.

   Upande wa utetezi huitetea mada iliyopo na hushikilia mawazo yenye kuunga mkono mada hiyo wakati ambapo upande wa upinzani nao hulenga kutafuta hoja na mifano ya kuthibitisha maoni yao kwa kupinga mada na maoni ya watetezi ili kuwaridhisha wasikilizaji washiriki. Mwenyekiti huanzisha mdahalo na kuuongoza.

Anahakikisha kwamba kuna kuheshimiana (nidhamu) katika maendeleo ya mdahalo na kuwachagua wasemaji bila kuonyesha upendeleo wowote, akawapangia wasemaji muda wa kutumia, akamkaribisha katibu kumsaidia kuendesha zoezi la kupiga kura na kutoa muhtasari wa mambo yaliyozungumziwa, na mwishoni mwa mdahalo huufunga.

Wajibu wa katibu katika mdahalo ni kuandika muhtasari wa hoja zinazotolewa na wasemaji wa pande zote mbili, kuisomea hadhira na kutangaza matokeo ya kura zilizopigwa wakati ambao wajibu wa hadhira ni kufuata malumbano kati ya watetezi na wapinzani na kupiga kura.

2. Mjadala hushirikisha watu katika kundi dogo au kubwa ambao wana suala la kuzungumzia na kulitolea mwelekeo wa kiujumla. Mjadala hushirikisha mwenyekiti na hadhira.

Wajibu wa mwenyekiti ni kuanzisha mjadala na kuuongoza. Anahakikisha kwamba kuna nidhamu wakati wa kutoa hoja, akachagua wasemaji bila kuonyesha upendeleo wowote, akawapangia muda wa kutumia, akakumbusha mambo muhimu, yaliyozungumziwa na kuufunga mjadala kwa kuwashukuru waliohusika katika mjadala huo.

Wajibu wa hadhira ni kutoa hoja kulingana na anavyofikiria suala kila msemaji bila kushikilia upande wowote.

3. Uhusiano ni kwamba mdahalo na mjadala huhusisha watu wengi wanaojadiliana kuhusu jambo fulani. Kuna mada ambayo hutolewa mawazo, kuna kiongozi wa kuanzisha na kuendeleza mambo mpaka mwisho. Mdahalo na mjadala huwa na malengo sawa ya kukuza utamaduni wa kuheshimiana, kukuza matumizi fasaha ya lugha na matamshi yake bora, kukuza uwezo wa kusema hadharani na kuwapa watu fursa ya kuelewana na wengine mbalimbali pamoja na kumwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapoandika insha au habari.

4. Kuna mambo muhimu yanayotofautisha mdahalo na mjadala: taratibu zinazozingatiwa katika utekelezaji wa mazungumzo yenyewe hutofautiana. Mada za mdahalo na mjadala hutofautiana kwani lengo la mada za mijadala ni kutafuta suluhisho kwa jambo linaloikabili jamii fulani, ilhali mdahalo huhitaji wapinzani na watetezi ambao huwania kuibuka na ushindi. Mdahalo huhusisha pande mbili za utetezi na upinzani ambapo mjadala huhusisha kundi moja tu. Mdahalo una kiongozi mmoja lakini mjadala huhusisha mwenyekiti aliye na katibu.

5. Manufaa ya kufanya mazoezi mengi ya midahalo na mijadala kwa wanafunzi ni kujizoeza kutumia lugha ya Kiswahili, kukuza uwezo wa wanafunzi hao wa kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa ufasaha, kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri na kujizoeza kujiegemeza mifano kamili kila anapotoa hoja zake.

### 15.4.2. Msamiati Kuhusu Kifungu cha Habari

*Zoezi la 2:* **(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)**

*Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo*

1. Katibu: Kesho nitakwenda kumtafuta katibu wa shule yetu.
2. Mwenyekiti: Mwenyekiti wa shirika letu ni mtu mpole na mwerevu sana.
3. Kikomo: kilicho na mwanzo kina kikomo.
4. Ufasaha: Uzingatiaji wa ufasaha wa lugha hurahisisha mawasiliano kati ya wazungumzaji.
5. Nidhamu: Ni vizuri kwa kila mtu kuwa na nidhamu katika maisha yake ya kila siku.
6. Mdahalo: Kwa ajili ya kukuza ufasaha wa lugha, tunapenda kufanya midahalo shuleni kwetu.
7. Maoni: Tafadhali wenzangu, tusikilize kwanza maoni yake kabla ya kumuuliza.
8. Kutetea: Wakati mwingine tutatetea hoja kwamba maji safi yawafikie Wananchi wote.
9. Makundi: Kazi ya makundi husaidia wanafunzi kujua mengi kutoka kwa wenzao.
10. Muhtasari: Mwishoni mwa mdahalo, katibu huipatia hadhira muhtasari wa hoja zilizotolewa.

***Zoezi la 3:* (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)**

*Husisha neno katika sehemu A na maana yake katika sehemu B*

Majibu: 1j, 2d, 3f, 4a, 5c, 6e, 7h, 8i, 9g, 10b.

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia maneno yanayofaa*

1. Mwanafunzi wa lugha anajizoeza kutumia **matamshi** bora wakati wa mdahalo.
2. Katibu wa mdahalo **anaandika** hoja zilizotolewa na wachangiaji.
3. Mdahalo humpasa mshiriki kuwa na moyo wa **kuheshimu** mawazo ya wengine.
4. Mjadala ni **majadiliano** yanayohusisha watu wengi.
5. Washiriki wa **mjadala** ni lazima watoe maoni yao bila kuegemea upande wowote.
6. Midahalo na mijadala humsaidia mwanafunzi kutambua **kiwango** chake katika lugha.
7. Katika **mdahalo**, mwenyekiti ndiye ambaye anachagua atakayesema.
8. Kila mtu aliyealikwa anaombwa **kushiriki** katika majadiliano.
9. Anayeshiriki katika mazungumzo anakuza utumiaji wa **lugha.**
10. Kuelewa mada ni chanzo cha kutoa maoni mazuri.

### 15.4.3. Sarufi

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Unda vielezi kutoka kwenye vivumishi ambavyo vimepigiwa mstari, kisha utunge sentensi kwa kutumia kielezi hicho*

**Mfano**: Angalia watoto wale **wema.**

Wema: **vema**

Wanafunzi wangu hufanya mtihani **vema.**

1. baya: vibaya

Kabano aliupiga mpira vibaya

2. kali: vikali

Gatete alimpia shoti vikali akaumia mikono.

3. wazuri: vizuri

Eti mtoto wangu, alisoma vizuri shuleni na hivi sasa nataka kumpa zawadi.

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*A. Tumia kiambishi awali -ki kuunda vielezi kutoka nomino hizi.*

*B. Tunga sentensi mpya ukitumia vielezi upatavyo.*

1. **mfalme**: kifalme
2. **Mzee:** kizee
3. **waume**: kiume
4. **msichana:** kisichana
5. **jeshi:** kijeshi

### 15.4.4 Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali hapo chini*

1. Wapinzani hutaka kushawishi hadhira katika mdahalo kwa sababu ya kuwataka wakubaliane na mawazo yao kuhusu jambo linalozungumziwa ili wapate ushindi dhidi ya watetezi.

2. Katibu hana kazi yoyote katika mjadala kwani mwenyekiti ndiye huyaongoza maendeleo yake toka mwanzo hadi mwisho.

3. Mwenyekiti huwa na majukumu mengi katika mjadala kuliko katika mdahalo. Majukumu ya kipekee katika mjadala ni kwamba yeye hutoa muhtasari wa hoja zilizotolewa ambapo kazi hiyo hufanywa na katibu katika mdahalo. Yeye huzusha mawazo na kusimamia zoezi la kupiga kura kwa ajili ya kupata uamuzi.

4. Umuhimu wa mdahalo kwa washiriki wake ni kuwasaidia kushiriki katika utetezi au upinzani wa jambo ambalo linazungumziwa na kuwazoeza wasikilizaji kupinga au kutetea maoni na hoja za wengine.

5. Mada za mjadala huwa na maumbile ya kuhitaji ufafanuzi kutokana na mchango wa mawazo ya wengi kiujumla. Mawazo hayo lazima yahusiane na jamii kwa namna fulani. Mara nyingi mjadala huwa na mada zinazoikumba jamii.

### 15.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*1. Mwalimu anawasaidia kwanza wanafunzi kujenga makundi ya ushirikiano*

Hoja nne zinazoweza kutolewa kuhusu mada "Majadiliano huimarisha utamaduni wa amani" ni kama hizi:

1. Majadiliano huimarisha utamaduni wa amani .Majadiliano huhimiza watu kutoa maoni yao kwa kuheshimiana.

2. Majadiliano hurahisisha upatikanaji wa suluhisho la tatizo fulani katika jamii.

3 . Majadiliano huzoeza watu kuzungumzia shida mbalimbali kwa amani badala ya kutosikilizana kutokana na hali kwamba kila mtu hubaki na msimamo wake tu.

2. *Mwalimu atatumia makundi, jozi au kazi za kipekee.*

Baadhi ya hoja zinazoweza kutolewa kutetea mada "Ndoa za zamani nchini Rwanda ni nzuri kuliko ndoa za kisasa" ni hizi zifuatazo:

1. Ndoa za zamani ni nzuri kwa sababu zilikuwa rahisi kufanyika pasipo gharama kubwa (watu waliolewa bila wenza wao kutumia mali nyingi).

2. Ndoa za zamani zilidumu kwa muda mrefu kwani sheria za talaka (kutenganisha mme na mkewe) hazikuwepo.

3. Katika ndoa za zamani wazazi waliwasaidia watoto wao kufunga ndoa kwa kuwachagulia mme au mke. Vile vile maharusi hawakuongozwa na msisimko wao kwani wazazi walifikiria sana jambo hilo.

Baadhi ya hoja zinazoweza kutolewa kupinga mada hii ni kama hizi:

1. Watu walikuwa na desturi ya kuoana bila kupendana wao peke yao. Hali hii huweza kuzusha matatizo magumu sana mpaka ndoa zikavunjika.

2. Wanawake walinyanyaswa ovyo na waume zao na maoni yao hayakupewa nafasi.

3. Kwa kuwa wazazi ndio waliochagulia wavulana wao wake, wake hao mara kadhaa walichangiwa na waume zao pamoja na akina baba mkwe.

### 15.4.6. Kuandika

**Zoezi la 9**: ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu anaweza kuwasaidia wanafunzi wake kuunda mada inayohusiana na desturi ya kujitegemea ama wanafunzi wakajiundia mada hiyo wenyewe. Baadaye, mwanafunzi mmoja atatunga mjadala wa ukurasa mmoja kuhusu mada hiyo. Wanafunzi wanaweza kuutunga wawili wawili au zaidi ya wawili lakini mwalimu aongeze idadi ya kurasa kulingana na idadi ya wanafunzi.

## Muhtasari wa Mada ya Nne

Mada hii ya nne "**Ukuzaji wa matumizi ya lugha kimazungumzo"** ina masomo matatu yanayohusiana na mada husika. **Somo la kumi na tatu** linawawezesha wananafunzi kushiriki katika midahalo na kuiongoza, kutoa hoja kuhusu mada iliyotolewa, kuwa na uwezo wa kuongoza majadiliano na kuwa na uzoefu wa kuwasilisha hadharani. **Somo la kumi na nne** linashughulikia umuhimu wa kuwawezesha wanafunzi kujenga uwezo wa kuchambua mawazo muhimu katika mazungumzo, kuandaa na kuongoza mazungumzo ya aina mbalimbali hata kupata uamuzi juu ya jambo fulani maishani mwao. **Somo la kumi na tano,** mwanafunzi atakuwa na uwezo wa kutofautisha midahalo na mijadala na insha nyingine.

**Maelezo ya Ziada**

Mdahalo ni majadiliano baina ya watu wengi juu ya jambo moja maalumu. Kuna mada inayozungumziwa, wazungumzaji wakuu wanaotetea mada (upande wa utetezi) na wazungumzaji wakuu wengine wanaopinga mada (upande wa upinzani). Aghalabu huwa wazungumzaji wakuu wawili kwa kila upande.

Mwenyekiti wa mdahalo ana wajibu wa kufungua na kuendesha mdahalo, kuwapa wasemaji nafasi ya kuzungumza, kusimamia upigaji wa kura na kufunga mdahalo.

Katibu wa mdahalo ndiye huandika hoja zinazotolewa na wazungumzaji mbalimbali, kufanya na kusoma muhtasari wa hoja zilizotolewa na pande mbili mwishoni mwa mdahalo na kutangaza matokeo ya kura zilizopigwa.

**Maana ya mjadala**

Mjadala ni mazungumzo yanayohusu mada mahususi ambayo hufanywa kwa kujenga hoja na kuongozwa na mtu mmoja au watu wawili.

**Sifa za mjadala.**

1. **Suala lililo wazi la mjadala**. Jambo au mada inayojadiliwa ni lazima liwe wazi na lenye kuvutia.

2. **Mpangilio na muumano wa hoja**: Kwa kutoa hoja, inalazimu kuzipanga ifaavyo. Kila hoja ikiwa na maelezo yake bila ya kuchanganya changanya hoja.

3. **Msimamo dhahiri** : Mwandishi hutoa hoja kwanza au kudokeza msimamo mwanzo kisha mwandishi akatoa sababu za kuchukua msimamo fulani.

**4. Mjadala unaosadikika**: Mwandishi wa mjadala amsadikishe msomaji kwa kutumia mbinu alizochagua ifaavyo, zile zenye ithibati ambazo humwezesha msomaji kuhakikisha ukweli wa jambo alilosoma. Matumizi ya takwimu yanahitajika kwa kutilia mkazo na kuonyesha kinyume cha upande mwingine

**5. Sauti inayokubalika**: Maandaalizi ya mjadala yanamlazimu kuteua na kuyatumia maneno ya kumvutia watakaousoma ili yawatie kukubalinana kuhusu mada iliyozungumziwa au kuandikiwa. Inamlazimu tena matumizi ya lugha yenye heshima hata ikiwa kuna upinzani wa mada lugha yenye matusi na kudharau isitumiwe.

**6. Ufarisi wa lugha na mbinu zake**: Mwandishi atumie lugha teule na mbinu zake kwa kuwalenga wasomaji kama lugha ni muhimu sana katika kila kazi yoyote ya uandishi.

**Umuhimu wa Mjadala.**

Hukuza uwezo wa kitaaluma, fikra na hali ya udadisi pamoja na kushawishi hadhara.

Huwezesha mtu kujitambua binafsi kipaji chake cha kuchangia hoja na wengine.

Hutufanya tuzoee kuheshimu hoja za wengine, kuwasikiliza na kuachiria nafasi ya kutoa maoni yao.

Hutufanya kuheshmu na kutumia muda ifaavyo katika mazungumzo.

Husaidia mtu kukuza uwezo wa kupanga mawazo katika mazungumzo.

Anayehudhuria hukuza uwezo wa kuyachagua mawazo, kuiunga mada na pia kupinga kauli fulani.

**Uhusiano kati ya mdahalo na mjadala**

Mdahalo na mjadala huhusisha watu wengi wanaojadiliana kuhusu jambo fulani. Kuna mada ambayo hutolewa mawazo, kuna kiongozi wa kuanzisha na kuendeleza mambo mpaka mwisho. Mdahalo na mjadala huwa na malengo sawa ya kukuza utamaduni wa kuheshimiana, kukuza matumizi fasaha ya lugha na matamshi yake bora, kukuza uwezo wa kusema hadharani na kuwapa watu fursa ya kuelewana na wengine mbalimbali pamoja na kumwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapoandika insha au habari.

**Tofauti kati ya mdahalo na mjadala**

**Mdahalo** huhusisha pande mbili: upande wa utetezi na upande wa upinzani. Huwasaidia wanafunzi kushiriki katika utetezi au upinzani wa jambo fulani. Unaongozwa na mwenyekiti pamoja na katibu. Katika mdahalo, wazungumzaji hushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo yao kuhusu jambo fulani. Mdahalo huzoeza watu kusikiliza, kupinga au kutetea maoni na hoja za wengine.

Kwa upande mwingine, **mjadala** ni mazugumzo juu ya jambo husika katika makundi madogo au makubwa. Unaongozwa na mwenyekiti mmoja wa kuzusha mawazo, kuhakikisha kwamba kuna kuheshimiana kati ya washiriki na kutoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa mwishoni. Mjadala huhusika na mada ambazo zinahitaji ufafanuzi kutokana na mchango wa mawazo ya wengi.

Anayetoa hoja yake, anaweza kukubali au kupinga maoni ya mwenzake kwa kutoa mchango wake wa kutatua tatizo linalojadiliwa.

**Tathmini ya Mada ya Nne**

1. Sifa zinazotofautisha mdahalo na mjadala.

**Mdahalo** huhusisha pande mbili: upande wa utetezi na upande wa upinzani. Huwasaidia wanafunzi kushiriki katika utetezi au upinzani wa jambo fulani. Unaongozwa na mwenyekiti pamoja na katibu. Katika mdahalo, wazungumzaji hushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo yao kuhusu jambo fulani. Mdahalo huzoeza watu kusikiliza, kupinga au kutetea maoni na hoja za wengine.

Kwa upande mwingine, **mjadala** ni mazugumzo juu ya jambo husika katika makundi madogo au makubwa. Unaongozwa na mwenyekiti mmoja wa kuzusha mawazo, kuhakikisha kwamba kuna kuheshimiana kati ya washiriki na kutoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa mwishoni. Mjadala huhusika na mada ambazo zinahitaji ufafanuzi kutokana na mchango wa mawazo ya wengi. Anayetoa hoja yake, anaweza kukubali au kupinga maoni ya mwenzake kwa kutoa mchango wake wa kutatua tatizo linalojadiliwa.

2. a.Kwanza kuchagua mada
   b. Kupanga mawazo makuu ya kuzungumizia
   c. Kuchagua mwenyekiti, wazungumzaji wakuu kwa pande zote mbili, kuchagua katibu.
   d. Kuandaa mdahalo
   e. Kuuwasilisha mbele ya watu
   f. Kupiga kura
   g. Kutangaza matokeo ya kura
   h. Kufunga mdahalo

3. Katika Bunge la Taifa la Rwanda mdahalo una umuhimu sana kwani wabunge wanafanya kazi zao kwa kujadiliana kuhusu mambo mbalimbali na kabla ya kutoa uamuzi hupitia njia ya kupiga kura ili waimarishe maisha bora ya raia.

4. Kuhusu mjadala kuna kiongozi na kundi la watu ambalo analiongoza kwa kuwapa nafasi ya kutoa hoja wakati katika mdahalo mwenyekiti ndiye kiongozi ambaye huwapa fursa wazungumzaji wa kila pande ikiwa upande wa upinzani au wa utetezi kwa kutoa hoja zao. Zaidi ya hayo mwenyekiti husimamia upigaji wa kura na kutangaza matokeo ya kura na kufunga mdahalo. Kuna pia katibu anayeandika hoja zote zinazotolewa katika mdahalo. Wasemaji wa upande wa utetezi hutetea mada wakati wa upinzani huipinga mada.

5. Mdahalo na mjadala zote ni shughuli zinazoweza kufanikisha maadili na mwenendo mwema kutokana na kuelimisha jamii

6. Wahusika wa mdahalo ni : Mwenyekiti ambaye huongoza ; Watetezi na wapinzani wanaofanya kazi ya kutoa hoja kulingana na upande wao ; Katibu huandika hoja zote zilizotolewa wakati katika mjadala kiongozi huongoza mazungumzo juu ya jambo au mada iliyotolewa na wasemaji wakatoa hoja zao.

7. Mwalimu awaelekeze wanafunzi, wajiandae kwa ajili ya mdahalo kuhusu mada wanayopewa"Mahari ni ishara ya upendo siyo mauzo" Ikiwa wanahitaji msaada mwalimu awasaidie.

8. Mwalimu awaelekeze wanafunzi, watunge mjadala kuhusu mada wanayopewa"Elimu ndio msingi madhubuti wa maendeleo endelevu" Ikiwa wanahitaji msaada mwalimu awasaidie.

**Mazoezi ya Nyongeza**

**Mazoezi ya Urekebishaji**

1. Eleza maana ya mdahalo.
2. Eleza kazi ya kila mhusika katika mdahalo.
3. Jadili kuhusu tofauti kati ya mdalo na mjadala.
4. Unda majina kutoka maneno uliopewa hapo chini:

a) Wanafunzi **wanasoma** lugha ya Kinyarwanda, Kiingereza na Kifaransa.
b) Vitabu hivi **viliandikwa** na walimu.
c) Maji **safi** ni bora maishani mwa mtu.
d) **Wema** hauozi .
e) Ni **vizuri** kulinda mazingira.

**Mazoezi ya Jumuishi**

1. Linganisha wahusika wa mdahalo na wahusika wa mjadala

**Mazoezi ya Wanafunzi wenye Ujuzi wa Hali ya Juu**

1. Tunga mdahalo wa kursa tatu kuhusu mada hii "Ngozi ivute ingali mbichi."

# MAREJEO


MASEBO, N. C. (2002). *Kiswahili Kidato cha Tatu na Nne Maendeleo ya Kiswahili, Fasihi, Sarufi, Matumizi, Utungaji na Ufahamu*. Dar es Salaam: NYAMBARI NYANGWINE PUBLISHERS

Massamba D.P.B., Kihore, Y. K., Hokororo, J.I. (2009). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mlaga. W. K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne* ya 21. Heko Publishers Ltd. Dar es salaam.

Ndalu, A., S. M. (2013). *Johari ya Kiswahili Rwanda Kidato cha Nne Kitabu cha mwanafunzi.* Kigali: East African Publishers Rwanda Ltd.

NIYOMUGABO, C. (2013). *Mafunzo ya kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi.* Kigali: Fountain Publishers Rwanda Ltd.

NIYIRORA E., NDAYAMBAJE L. (2012). *Kiswahili Sanifu kwa Shule za Sekondari.* New Delhi: Tan Prints (India) Pvt.Ltd.

NIYOMUGABO, C. (2013). *Mafunzo ya Kiswahili kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha* 6.Kigali: Fountain Publishers Rwanda Ltd.

Nkwera, F.V.M. (1979). *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

NTAWIYANGA, S., Muhamud A, Kinya J na Sanja L, (2018), *Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Mchepuo wa Lugha, Kidato cha Sita. Nairobi*, Longhorn Publishers.

TUKI. (2006). *English Swahili Dictionary 3rd Edition*. Dar es Salaam: Book Printing Services Ltd.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.*Nairobi: Oxford University Press.

Wizara ya Mafunzo ya Msingi na Sekondari (1987). *Kitabu cha Kiswahili III* B. Kigali: Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari.

Wizara ya Mafunzo ya Msingi na Sekondari (1987). *Kitabu cha Kiswahili IV-V B. Kigali: Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari.*